CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SHULE YA FANI NA SAYANSI YA KIJAMII

IDARA YA KISWAHILI

MIELEKEO NA MTINDO WA SHAFI ADAM SHAFI KATIKA RIWAYA ZA *KULI* NA *HAINI*

ELIZABETH WAMBUI GATHENYA

C50/CE/11305/2008

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA LENGO LA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

MEI, 2018

UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KINGINE.

Mtahiniwa

…….. …….

Sahihi **Tarehe**

ELIZABETH WAMBUI GATHENYA

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WA KAZI HII KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

…….. …….

Sahihi **Tarehe**

PROFESA CATHERINE NDUNGO

Idara ya Kiswahili

…….. …….

Sahihi **Tarehe**

BWANA JAPHET MUTEGI MUKOBWA

Idara ya Kiswahili

SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai alionijalia na siha njema, uwezo na nguvu za kuyafikisha masomo yangu kiwango hiki. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wa kazi hii, Profesa Catherine Mwihaki Ndungo na Bwana Japhet Mutegi Mukobwa. Kwa uongozi wao, kazi hii ilipata mwongozo. Asanteni, Jalali awajalie mema. Aidha, nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili, Profesa K. King‟ei, Dkt R. Wafula, Profesa J. Gakuo, Dkt J. Onyango, Dkt P. Y na Dkt M. Osore. Nimefaidika pakubwa kwa kunielekeza na kunishauri kila nilipohitaji ushauri wao. Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu Helina, Stella, Barasa, Birir, Josline, John Kim na Mwangi kwa ushirikiano na msaada wao. Shukrani. Namshukuru mume wangu Charles Gathenya Thuo na wanangu Patrick, George, Esther na Leah waliojitolea juu chini kunisaidia nilipokuwa nikisoma kwa kunihimiza kuendelea Mungu awabariki sana. Nawaombea baraka za Mola awawezeshe kupiga hatua kubwa katika elimu yenu zaidi ya hapa nimefika. Hatimaye, nawashukuru wote walionipa msaada wa aina yoyote, ambao umechangia katika kufanikisha kazi hii, hasa Rephaiah aliyenichapia kazi yote, Profesa Ngerenwa, Reverent Njamunge, Bi. Martha Chomba, Bi. Margaret Mugo, Rita na Perpetua kwa maombi yao. Mwenyezi Mungu awashushie baraka tele maishani mwenu.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu marehemu baba yangu niliyempenda sana Solomon Muugi Ng‟ang‟a na mama yangu kipenzi changu cha moyoni Leah Ngombi Muugi. Mlinihimiza nisome kwa bidii tangu nilipokuwa mchanga. Mliponipeleka shuleni. Nayashuhudia matunda ya jitihada zenu. Asanteni.

ABSTRACT

This is an analysis of how the style in two works of Shafi Adam Shafi were influenced by his attitudes. This work analyses the style and attitudes of the writer by using foregrounding and deviation as styles of writing. The choosen texts are *Kuli* (1979) and *Haini* (2002). This novels were choosen randomly because there was usage of the two writing styles which could be used in this research. The research dealt with foregrounding and deviation of words and meaning in the novels. Then the attitudes of the writer socially, historically, economically and revolutionary orientation of the author emerges in the text. The research was directed by two theories which include; Solialist Realism Theory which analysis the context and attitudes that influenced the writer while writing. Its tenets also assisted in the analysis. The other theory used is the Stylistic Theory. The tenets of this theory as stated by Leech (1969) were used to analyse the writing styles of deviation and foregrounding in the texts. The research was done in the library where the data collected through reading was analysed and presented through descriptive method.

IKISIRI

Utafiti huu umechanganua mtindo na mielekeo kwa kushughulikia matumizi ya uchimuzi na ukiushi katika riwaya teule za mwandishi Shafi Adam Shafi. Utafiti unazingatia riwaya mbili teule za *Kuli* (1979) na *Haini* **(**2003). Uteuzi wa riwaya hizo ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio kwa kuwa zilidhihirisha mtindo wa mwandishi kupitia matumizi ya uchimuzi na ukiushi ambazo zingetosheleza mahitaji ya utafiti huu. Utafiti ulizingatia matumizi ya uchimuzi na ukiushi wa maneno na maana katika riwaya husika. Aidha, mielekeo ya mwandishi ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi inajitokeza. Utafiti huu uliongozwa na nadharia changamano. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na nadharia ya Kimtindo. Mihimili ya nadharia ya Kijamaa ilifaa utafiti huu kwa kuchanganua mazingira na mielekeo ya mwandishi. Nayo mihimili ya nadharia ya Kimtindo kama alivyoeleza Leech (1969) ilitumika katika kubainisha aina za ukiushi wa uandishi wa riwaya husika. Mihimili ya nadharia ya Kimtindo ilimwongoza mtafiti katika ufasiri wa ujumbe wa riwaya teule. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ambapo uchanganuzi ulizingatia mielekeo ya mwandishi, uchimuzi na ukiushi wa msamiati na maana katika riwaya zote mbili.

YALIYOMO

UNGAMO ..... **ii**
SHUKRANI ..... **iii**
TABARUKU ..... **iv**
ABSTRACT ..... **v**
IKISIRI ..... **vi**
FASILI YA ISTILAHI ..... **x**
UFUPISHO ..... **xi**
SURA YA KWANZA **1**
1.0 Utangulizi 1
1.1 Usuli wa Utafiti 1
1.1 Suala la Utafiti 2
1.2 Maswali ya Utafiti 3
1.3 Malengo ya Utafiti 3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada 4
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti 5
1.6 Misingi ya Nadharia 6
1.6.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa 6
1.6.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa 8
1.6.3 Nadharia ya Kimtindo 9
1.6.4 Mihimili ya Nadharia ya Kimtindo 12
1.6.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada 13
1.7 Mbinu za Utafiti 18
1.7.1 Uteuzi wa Sampuli 18
1.7.2 Ukusanyaji wa Data 18
1.7.3 Uchanganuzi wa Data 19
1.7.4 Uwasilishaji wa Data 19
1.8 Hitimisho 19
SURA YA PILI: MAZINGIRA NA MIELEKEO **20**
2.0 Utangulizi 20
2.1 Mtunzi na Mazingira Yake 20

2.2 Mazingira Yaliyomwathiri katika Uteuzi Wake wa Mielekeo 20
2.2.1 Mazingira na Mielekeo ya Kijamii..... 21
2.2.2 Mazingira na Mielekeo ya Kiuchumi 28
2.2.3 Mazingira na Mielekeo ya Kihistoria 40
2.2.4 Mazingira na Mielekeo ya Kimapinduzi 52
2.3 Hitimisho 57
SURA YA TATU: UCHIMUZI NA UKIUSHI WA MANENO 58
3.0 Utangulizi 58
3.1 Mtindo katika Riwaya za *Kuli na Haini*..... 59
3.2 Mlazo kama Mbinu ya Ukiushi..... 68
3.3 Ukiushi na Uchimuzi wa Maneno..... 74
3.4 Dhana ya Lafudhi..... 76
3.5 Dhana ya Misemo na Nahau..... 78
3.5.1 Misemo na Nahau katika Riwaya ya Kuli 78
3.5.2 Misemo na Nahau katika Riwaya ya Haini 80
3.6 Dhana ya Methali 83
3.6.1 Methali katika Riwaya ya Kuli 83
3.6.2 Methali katika Riwaya ya Haini..... 84
3.7 Uradidi wa Maneno..... 87
3.7.1 Uradidi katika Riwaya ya Kuli..... 87
3.7.2 Uradidi katika Riwaya ya Haini..... 91
3.8 Ukiushi na Uchimuzi wa Kisintaksia 94
3.8.1 Urefu wa Sentensi 94
3.8.2 Usambamba na Uradidi katika Sentensi..... 96
3.9 Hitimisho 102
SURA YA NNE: UKIUSHI NA UCHIMUZI WA MAANA..... 103
4.0 Utangulizi 103
4.1 Dhana ya Sitiari..... 103
4.1.1 Sitiari katika Riwaya ya Kuli..... 104
4.1.2 Sitiari katika Riwaya ya Haini 104
4.2 Dhana ya Tashibihi..... 106

4.2.1 Tashibihi katika Riwaya ya Kuli 106
4.2.2 Tashibihi katika Riwaya ya Haini 108
4.3 Dhana ya Tabaini 110
4.3.1 Tabaini katika Riwaya ya Kuli 110
4.3.2 Tabaini katika Riwaya ya Haini 111
4.4 Dhana ya Tanakali 114
4.4.1 Tanakali katika Riwaya ya Kuli 114
4.4.2 Tanakali katika Riwaya ya Haini 115
4.5 Dhana ya Tashihisi 117
4.5.1 Tashihisi katika Riwaya ya Kuli 117
4.5.2 Tashihisi katika Riwaya ya Haini 118
4.6 Dhana ya Jazanda 120
4.6.1 Jazanda katika Riwaya ya Kuli 120
4.6.2 Jazanda katika Riwaya ya Haini 122
4.7 Dhana ya Ishara 125
4.7.1 Ishara katika Riwaya ya Kuli 126
4.7.2 Ishara katika Riwaya ya Haini 127
4.8 Hitimisho 127
SURA YA TANO: HITIMISHO 128
5.0 Muhtasari na Matokeo ya Utafiti 128
5.1 Utangulizi 128
5.2 Muhtasari wa Utafiti 128
5.3 Matokeo ya Utafiti 131
5.4 Changamoto ya Utafiti 134
5.5 Mchango 134
5.6 Mapendekezo ya Utafiti 134
5.7 Hitimisho 135
MAREJELEO 136

FASILI YA ISTILAHI

Mielekeo - Kuligana na Althusser (1968), hii ni dhana inayotumiwa kuelezea mtazamo au mkabala anaochukua msanii au unaochukuliwa na jamii kuhusiana na jambo, tukio, suala au wahusika fulani.

Mtindo - Kwa mjibu wa Ngara (1982), mtindo ni namna ambavyo mwandishi hujieleza kwa kutumia lugha kama nyenzo kuu ya mawasiliano.

Nyenzo - Vifaa vya kufanyia shughuli fulani.

Uchimuzi - Kuligana na Kazungu (1982), hii ni mbinu ya kuyadokeza mambo fulani au sifa fulani katika kazi ya kifasihi kwa namna ya waziwazi na kuyafanya yajitokeze waziwazi ya kilinganishwa na mengine. Hii ni mbinu inayotumiwa kusisitiza mambo fulani yanayoonekana kuwa muhimu au yenye uzito katika kazi fulani ya kifasihi.

Ukiushi - Kuligana na Njuguna (2015), ni neno linalotokana na kitenzi "kiuka". Kukiuka ni kutozingatia desturi, kanuni au kaida fulani. Kwa hivyo, ukuishi wa lugha ni kule kutozingatia ukawaida au kanuni zilizokubalika kitaaluma katika maandishi au mazungumzo.

Mtoto - Ni dhana tata na hususan tunapojaribu kuweka mipaka ya miaka ya utotoni. Hunt (1994) anaelezea kwamba mtoto ni mwanadamu ambaye hajakomaa kiakili na yuko chini ya miaka kumi na minane. Utafiti huu unayachukulia maelezo yaliyo tolewa na Tucker (1981), kwamba mtoto ni binadamu ambaye ana umri kati ya miaka saba aanzapo masomo katika shule ya msingi na miaka kumi na mitatu anapobaleghe.

UFUPISHO

ACRWC - African Charter on the Rights and Welfare of the Child.

BAMVITA - Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania

C.G.A - Clove Growers Association

CRC - Convention on the Rights of the Child

FXB - Francois Xavier Bagnoud

TANU - Tanzania African National Union

TCRF - Tanzania Child Rights Forum

TUKI - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

UNICEF - United International Nations Children Fund

UWAVITA - Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania

WHO - World Health Organization

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchangua mada, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia, yalioandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, ukusanyaji wa data, uteunzi wa sampuli, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

1.1 Usuli wa Utafiti

Tangu kuumbwa kwa mwanadamu lugha ndicho kipawa anachokitumia ili kuelezea hisia zake, tajriba za maisha na fikira alizonazo ubongoni mwake, (Bakhtin, 1981). Mwanadamu anaweza kuelezea matukio muhimu katika maisha yake kiutunzi. Miongoni mwatukio hizo ni riwaya ambazo ni tunzo za fasihi. Fasihi hutumia lugha kwa ufasaha kama malighafi na kuumba kazi kama vile hadithi, riwaya, tamthilia, ushairi na utenzi.

Njogu na Chimera (1995), wakinukuu Roman Jakobson wanaeleza kwamba, fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimakusudi. Aidha, wanaeleza kwamba lugha inayotumiwa katika kazi ya fasihi inapendeza, inavutia na kutamanisha kuitafakari maradufu. Mawazo haya yanatiliwa nguvu na mawazo ya wanamuundo wa Kirusi Victor Shklovsky na Boris Tomashevsky wanaosema kwamba fasihi ni matumizi maalum ya lugha.

Hartman na Stork (1973), wanaelezea ukiushi kama istilahi inayotumika kurejelea usemi wowote usioambatana na sarufi au semantiki ya kawaida katika lugha sanifu. Sarufi katika muktadha huu unachukuliwa kuwa sheria za lugha zinazozingatiwa katika

matumizi ya kawaida ya lugha. Maoni yake yanaungwa mkono na Clysenaar (1976) anapofafanua ukuishi kama upotoshi wa matarajio yanayohusu viwango mbalimbali ya lugha.

Utafiti huu unalenga kuonyesha mielekeo ya mwandishi na mtindo wake unavyojitokeza katika riwaya teule. Ukiushi na uchimuzi zikiwa mojawapo za mbinu za kimtindo na uandishi wa riwaya. Utafiti huu umechunguza namna mbinu hizi zinavyojitokeza katika kazi ya mwandishi.

1.1 Suala la Utafiti

Uchunguzi wa tafiti ambazo zimefanywa ulibainisha kwamba hazikuchanganua mielekeo na mtindo katika riwaya teule. Ni bayana kuwa utafiti huu utaliziba pengo hilo.

Ni muhimu kuchambua mielekeo ya mwandishi ili kubainisha mambo yaliyojitokeza katika jamii yake yakampa ari katika uandishi. Watafiti wa awali walizingatia maudhui, mtindo na wahusika, mtindo na upokezi pia uhalisia na mtindo. Utafiti huu umezingatia matumizi ya mielekeo na mtindo katika riwaya za mwandishi Shafi Adam Shafi. Unachunguza jinsi anavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa wasomaji kupitia mielekeo yake ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapindunzi.

Katika mtindo mwandishi alitumia uchimuzi na ukiushi wa maneno na maana. Watafiti wa awali kama vile Weche (2000), amechambua vitabu vya fasihi kwa Kingereza vya Ezekiel Alembi kwa kuzingatia "mtindo na upokezi" naye Wanyama (2007), ameshughulikia "maudhui na mtindo" katika utendi wa Wabukusu "*Khuswala kumuse"*. Pia, Kairu (2005), ametumia nadharia ya kimtindo alipotafiti uhalisia na mtindo wa Ken Walibora.

Utafiti huu unazingatia mitindo ya uchimuzi na ukiushi wa maneno kwa kutumia mlazo, lafudhi, misemo, methali, uradidi wa maneno na kisintaksia. Pia, umechanganua ukiushi na uchimuzi wa maana kwa kuzingatia sitiari, tashibihi, tabaini, tanakali, tashihisi, jazanda na ishara.

Utafiti huu unabainisha jinsi mbinu hizi zilivyomsaidia mtunzi kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa wasomaji. Ukiushi na uchimuzi ni mbinu zinazohusu matumizi ya lugha kwa kutozingatia kanuni za lugha hiyo. Pia, utafiti huu unachukulia kuwa kwa kuchunguza jinsi mtunzi alivyokiuka matumizi ya lugha ya kawaida, lengo lake linaeleweka kwa undani zaidi.

Utafiti huu utayajibu maswali yafuatayo;

1.2 Maswali ya Utafiti

i. Mwandishi ameathiriwa na mazingira yapi katika utunzi wake?

ii. Ni mielekeo ipi iliyomwathiri mwandishi katika utunzi wake?

iii. Mwandishi ametumia mtindo upi katika utunzi wake?

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kutimiza malengo yafuatayo;

i. Kuchanganua mazingira ya mwandishi yalivyoathiri utunzi wake.

ii. Kuchanganua mielekeo ya mwandishi katika utunzi wake.

iii. Kuchambua mtindo wa mwandishi kupitia mbinu za uandishi za ukiushi na uchimuzi.

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Riwaya hizi zina taharuki ya hali ya juu ya kutaka kujua hatima ya baadhi ya wahusika kama vile Hamza katika riwaya ya *Haini* baada ya kuyapitia matatizo chungu nzima alipotiwa mbaroni bila kosa lolote akapigwa nusura afe. Naye mhusika Rashidi katika riwaya ya *Kuli* aliyezaliwa katika ufukara, akakua kwa shida baadaye akawa mtetezi wa wanyonge hatimaye akafungwa jela kwa ajili ya kuwatetea wanajamii yake. Riwaya hizi zinadhihirisha mambo halisi yanayowapata wanajamii. Wengi wao huuawa na wengine hufungwa jela bila sababu yoyote. Kwa hivyo, utafiti huu utayaweka wazi mambo yanayowapata watu walio katika jamii ya kisasa wanaonyanyaswa, kuteswa, kudhulumiwa na hata kuuawa wanapozitetea haki zao.

Azma kuu ya kuufanya utafiti huu wa riwaya teule za mwandishi Shafi Adam Shafi ni kuchanganua jinsi alivyozisanii riwaya zake na kuwasilisha maudhui yake kwa ustadi wa kipekee. Katika riwaya ya *Haini,* mwandishi alinuia kuyaweka wazi mateso wanayopitia wafungwa mle gerezani. Wao huteswa kwa hupigwa kinyama. Wengi wao huwa washukiwa tu, lakini hudhulumiwa, hudhalilishwa, hupigwa hadi baadhi yao hufa kwa makosa yasio yao. Nao wanaotekeleza maovu huwa huru na huendeleza uovu wao. Jambo la kutia moyo ni kuwa mwishowe wanyonge wanajitolea kujinasua kutoka kwa shida zao kwa kuutupilia mbali uongozi usiowafaa kwa kumuua kiongozi wao. Kwa hivyo, binadamu hawezi kuvumilia shida zozote bila kugundua njia ya kujinasua kwa kutumia mapinduzi.

Katika riwaya ya *Kuli* anafafanua jinsi binadamu hutumiwa kufanya kazi kama punda kisha hulipwa ajira isiyomfaa. Isitoshe, asisaidiwe apatapo ajali kazini na asipewe fursa

ya kutetea haki yake ya kuongezewa ajira. Wafanyakazi wanapopigwa risasi kwa kudai nyongeza ya mshahara ni jambo la kushangaza. Mwishowe wanapanga mgomo bila kujali matokeo yake.

Aidha, kuziweka bayana riwaya za *Kuli* na *Haini* zenye usimulizi zilizopewa uhai mpya kwa ubunifu anapoyahuisha mapinduzi yanayoashiria ukombozi kama anavyosema Daiches (1981). Vilevile, tulinuia kumfanyia uchunguzi mwandishi wa awali aliyeziandika riwaya nyeti zilizowahamasisha watu kuhusu mambo yaliyowakabili katika jamii kama vile kunyanyaswa na jinsi wangeyatumia mapinduzi kujikimboa.

Riwaya za *Kuli* na *Haini* zina umuhimu wa kifasihi na kisiasa, riwaya hizi ni baadhi ya riwaya adhimu za Kiswahili. Zinaakisi hali halisi ya mambo yaliyotokea katika jamii. Riwaya hizi ni kumbukumbu ya matukio muhimu yaliyotokea duniani na hivyo zinasaidia kuhifadhi historia muhimu toka kizazi hadi kizazi. Historia hii ni urithi mkubwa wa jamii zinazofahamu Kiswahili. Pia, tumechagua mtindo kwa maoni yetu, mtindo ndicho kigezo cha kudhihirisha ubora wa kazi ya sanaa. Isitoshe, utafiti huu umechangia kuongezea hadhi fasihi ya Kiswahili kwa jumla kwa kudhihirisha kwamba zipo riwaya maarufu Afrika.

Kitaaluma utafiti huu utawafaa watafiti chipukizi watakaotafiti riwaya zingine za wasanii tofauti ili kudhihirisha umahiri wa wasanii wa riwaya za Kiswahili. Wasomi wa lugha watafaidika watakapourejelea utafiti huu kama mwongozo.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia riwaya za *Kuli* (1979) na *Haini* (2003) za mwandishi Shafi Adam Shafi. Kuna kazi nyingi zilizoandikwa lakini tumeteua riwaya mbili tofauti za

mwandishi mmoja japo ziliandikwa katika mazingira tofauti. Utafiti huu haujashughulikia riwaya zote za mwandishi bali zilizoteuliwa. Kwa hivyo, sentensi kadhaa zimechanganuliwa kubainisha matumizi ya mielekeo na mtindo wake. Utafiti unadhihirisha kuwa mwandishi alitumia mbinu za uchimuzi na ukiushi. Vilevile, kubainisha mielekeo ya mwandishi katika kazi zake.

1.6 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umetumia nadharia mbili, nadharia ya Uhalisia wa kijamaa na nadharia ya Kimtindo. Uteuzi wa nadharia hizi umetokana na sababu kuwa riwaya za mwandishi Shafi Adam Shafi zinazingatia masuala ya kijamii. Nadharia moja haingeweza kushughulikia masuala yote yaliyozingatiwa na mwandishi**.** Wanauhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wanapendelea wahusika, mandhari na matukio ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii.

1.6.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa

Hii ni nadharia ya kutunga na kuhakiki kazi za kifasihi inayotumiwa kuonyesha jamii katika uyakinifu wake na kuonyesha hatua zake za kimabadiliko. Baadhi ya wahakiki wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa ni Marxim Gorki (1972), Baxandall (1972), Terry Eagleton (1976), James C.V. (1973) na Bisztray (1978), mawazo yao yamekuwa na umuhimu mkubwa katika mapambano ya wanajamii ya kutaka kuboresha hali yao ya maisha. Mapambano haya ni baina ya matabaka mawili. Wachochole wanashirikishwa katika kuzalisha mali lakini faida yote inawaendea mabepari. Hali hii ndio inayoleta

mkinzano katika jamii na hautaisha mpaka mfumo wa uzalishaji mali uwe mikononi mwa wafanyakazi walio wengi.

James (1973) anasema iwapo msanii atawakilisha maisha, hawezi kushindwa kuona na kuonyesha kinachoyaelekeza katika ujamaa. Basi hii itakuwa sanaa ya kijamaa yaani uhalisia wa kijamaa. Uhalisia wa kijamaa kwa hivyo umejikita katika Umarx na Ulenin ambao unampa mwandishi na msanii uwezo wa kufahamu kwa undani na kwa udhahiri sheria zinazotawala maendeleo ya kijamii.

Popkin (1993) anaelezea jinsi mwandishi hutoa hali ya ukweli na kihistoria inayosawiri uhalisia katika jamii. Kisha, hujaribu kuwaelimisha umma jinsi ya kujikomboa kutoka kwa matatizo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, athibitishe suluhu ya matatizo haya kama mapinduzi yatakayoleta usawa katika jamii.

Berman (2012) anaiona ajira kama njia ya kuwanyanyasa watu. Wafanyakazi wanaifanya kazi kwa ujira duni ilhali wanafanya kazi saa nyingi. Waajiri hutaka faida kubwa bila kujali wafanyakazi.

Baxandall (1972) anaelezea kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi za kijamii na haiwezi kujitenga na maswala ya kijamii. Fasihi pia sharti ichangamshe hadhira yake na izingatie historia ya jamii husika.

Nadharia hii ina ufaafu wa uchambuzi wa kazi hii kwani inachanganua mielekeo ya mtunzi na jinsi ilivyomwathiri katika utunzi wake. Pia, inazingatia mambo halisi katika mazingira ya mwandishi yaliyomfaa katika utunzi wake. Nadharia hii pia ina upungufu wake unaopatikana kwa kuwa imekolea itikadi sana hivi kwamba masuala ya kisanaa

yanapuuzwa. Lugha inayotumiwa inaweza kuwa kavu ikakosa matumizi ya kunga za kifasihi kama vile sadfa, taharuki na tamathali za usemi. Upungufu huo wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa utafidiwa na nadharia ya kimtindo kwani inayahimiza matumizi ya lugha inayovutia wala sio kavu, iwe lugha yenye kunga zote za lugha.

1.6.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa

Kulingana na waandishi hawa uhalisia wa kijamaa unahusishwa na misimamo ifuatayo:

1. Pamoja na kusawiri matukio kihistoria, wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. Hufanya hivi kimakusudi au bila kufahamu la mno ni kwamba tabaka la wanyonge hujifungata masombo kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi.
2. Uhalisia wa kijamaa huzingatia maslahi ya wachochole. Hawa ni mafukara wa ulimwengu wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela.
3. Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu kama wahusika ambao hutumiwa kama vipasa sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao.
4. Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamaanisha kwamba mtu atakuwa mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.
5. Lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii. Ni lugha rahisi inayoeleweka na watu wote.

6. Wahusika wa kimaendeleo. Hawa ni wahusika wanaonuia kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), wahusika wa kimaendeleo ni wale wanaonuia kuipindua na kubadilisha hali yao ya maisha. Wao wana nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao.

Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi inapaswa kumsaidia binadamu ajikomboe na apate matumaini maishani. Vilevile, iwe ni ya kiyakinifu na isaidie katika kuielekeza jamii kutoka katika uozo hadi maisha mazuri zaidi. Mfumo mpya ambao hauna matabaka utaweza kufufuliwa kupitia mabadiliko hayo.

1.6.3 Nadharia ya Kimtindo

Nadharia ya Kimtindo iliasisiwa na Buffon (1930) anayesema kuwa mtindo ni jinsi mwandishi anavyotumia lugha kupitisha ujumbe. Anaelezea kuwa mtindo ndio unaomtambulisha mwandishi.

Umtindo mpya ulioasisiwa na Fowler (1975) unaonyesha jinsi mpangilio wa maneno wa kisintaksia unavyoongoza utaratibu wa usomaji ili kupata maana. Leech (1981) anasema kuwa mtindo ni njia ambayo lugha hutumiwa kama mali ya mtu binafsi. Aidha, mtindo ni matumizi ya lugha kupitia uteuzi unaotumiwa na mwandishi mmoja katika uandishi wa matini ya aina fulani. Kwa hivyo, mtindo huhusu uteuzi wa lugha. Mwandishi anastahili kutumia sifa zake za kimtindo zinazomtambulisha katika uteuzi wake wa msamiati, jazanda, tamathali za usemi, miundo ya sentensi na wasifu wa kisarufi.

Mwandishi pia aweze kuzua usemi wenye uwezo wa kushawishi na kuteka makini ya hadhira. Akifanya hivyo ataipamba lugha hiyo na kuifanya iwe na mvuto mkubwa wa kisanaa na kiumbuji. Mtindo pia hutegemea jinsi msomaji atakavyoelewa anachosoma kulingana na ubunifu wake mwenyewe. Msomaji ndiye anayesoma kilichoandikwa na mwandishi. Kwa hivyo, ni sharti aweze kufikiria kwa undani zaidi anayosoma ndipo aelewe anachokusudia mwandishi, kitakachomwezesha kung`amua tatizo na suluhisho la suala hilo katika jamii yake. Uchaguzi wa mtindo hutegemea vile vipengele vya uteuzi wa kiisimu unaohusiana na njia tofauti za kuchunguza maudhui sawa.

Lodge (1972) anaelezea kuwa mtindo ni jinsi ya kujieleza. Mwandishi anayaeleza mambo ya kawaida kisanaa ili yalete maana ya undani. Uteuzi wa tamathali za usemi hutegemea mtindo wa msanii binafsi. Mtindo wa msanii mmoja hutofautiana na wa msanii mwingine. Hii ndiyo sababu kazi ziwe za waandishi tofauti kwani „mtindo ni mtu.“ Tunaafikiana na anayosema Lodge kuwa mtindo ni mtu, kwa sababu mwandishi Shafi Adam Shafi amedhihirisha mtindo wake wa usanii. Umahiri wake wa uteuzi wa tamathali za usemi na matumizi ya mbinu za ukiushi na uchimuzi umeifanya kazi yake iwe ya kugusa hisia za msomaji, naye anapatwa na hamu ya kujua kitakachotokea baada ya kuwa na taharuki. Riwaya zake za *Kuli* na *Haini* zinadhihirisha usanii wake kwani ameelezea kisanii masuala nyeti ya kijamii kwa nia ya kuwahamasisha na kuwasisimua wasomaji na wasikilizaji wake.

Turner (1984) naye anaelezea kuwa mtindo ni sehemu ya isimu inayozingatia tofauti katika matumizi ya lugha ya fasihi. Sio mtindo wa maneno tu bali ni mwingiliano wa maneno. Mwandishi Shafi Adam Shafi ameyapanga maneno aliyotumia katika kazi yake

kwa makini yakaupata mwingiliano unaotoa maana anayokusudia. Mwingiliano huu ndio unaoipa kazi yake upekee, kwa jinsi anavyoyateua maneno yanayomwezesha kuelezea hadithi yake vilivyo.

Haynes (1995) anasema mtindo ni uchunguzi wa makini wa maneno katika matini unaozingatia jinsi tunavyoangalia tunachozungumza au tunachoandika. Mtindo pia ni mpangilio wa ruwaza za matini kwa ujumla. Maoni yake ni kuwepo kwa uchunguzi makini wa maneno katika uandishi na ruwaza za matini. Maoni yake yanawiana na utafiti huu kwani mtindo wa mwandishi Shafi Adam Shafi una sifa za kimtindo zinazohusiana na uteuzi wake wa makini wa maneno ili yawiane na dhamira yake, hivyo basi hupata uwiano katika matini.

Leech (1969) anasema kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji. Lugha ni chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Nadharia ya Kimtindo husisitiza uwiano kati ya ujumbe wa lugha. Ina msingi katika dhana kwamba lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwani hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi. Wazo hili linalandana na mada ya utafiti huu kwani kupitia ubunifu mkubwa wa matumizi ya mbinu za lugha ya mwandishi Shafi Adam Shafi ameweza kudhihirisha mtindo wake. Kwa kuibusha maudhui halisi kwa wanajamii kupitia fasihi yake ambayo ni kioo cha kujiangalia ili waone waishivyo, wanavyotaka kuishi na vile ambavyo anapendekeza waishi. Anachoelezea Leech kuhusu tajriba ya mwandishi atakayowasilisha kwa wasomaji ni kile anachokijua anachochota kutoka kwa ghala la wanajamii wake.

Tajriba ya mwandishi Shafi Adam Shafi inajitokeza wazi kutokana na yale yaliyomkabili yeye na jamii yake kwa ujumla. Katika riwaya ya *Kuli* anaelezea kuhusu kazi ya ukuli ambayo ndiyo iliyopatikana katika mazingira yake. Katika riwaya ya *Haini* anayaelezea yaliyotokea huko Unguja. Kwa hivyo, tajriba yake iliathiri pakubwa uandishi wake hasa maudhui na dhamira yake. Lugha aliyotumia ni kama chombo tekelezi cha kuwahamasisha wanajamii wote sio tu wa pwani umuhimu wa kuyakabili mambo yatakayowapata hasa dhuluma za aina yoyote ile.

1.6.4 Mihimili ya Nadharia ya Kimtindo

Mtindo una nafasi kubwa tu katika kazi ya fasihi. Humtambulisha mtunzi wa fasihi kwa sababu ndio anaotumia kuwavutia wasomaji wake. Hiki ndicho kipengele kinachotenganisha kazi nyingine za kisayansi na kazi zingine za kawaida, bila mtindo kazi za kifasihi zisingepata mashabiki wengi. Kwa hivyo, mtindo ndio huibua hisia na kuwafanya wasomaji wapende zaidi kusoma kazi za msanii husika.

Ifuatayo ni mihimili ya Nadharia ya Kimtindo

1. Matumizi ya lugha huwa rahisi au magumu. Maneno yanatumiwa kiufundi.
2. Matumizi ya dayalojia katika kusimulia hadithi.
3. Matumizi ya nafsi ya kwanza, ya pili na hata ya tatu katika usimulizi.
4. Wahusika hukua na kutambulishwa na pia hubadilika katika hadithi.
5. Hisia za mwandishi zinaonekana, zikionyesha dhihaka, mapenzi, matumaini, ukali au kejeli.

6. Kuna mpangilio wa sura au matukio katika hadithi. Sura fupi fupi au ndefu, nyingi zilizopangwa kwa nia fulani.
7. Kuna matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi, sitiari, tashihisi na kadhalika kwa wingi.
8. Uteuzi wa msamiati uliotumika huleta mvuto kwa msomaji kwa kumtia ari ya kusoma.

Tunapozungumzia dhana ya mtindo tunakuwa tunarejelea mwandishi husika, maana kwamba ubinafsi wake ndicho kile kinachoonekana kwenye kazi yake. Tunarejelea mtindo wa mtunzi tunaposema lugha yake inavutia, ina sitiari nyingi au taswira nyingi. Dhana ya mtindo ni namna mtunzi anavyopangilia kazi yake kifani na kimaudhui, yaani namna anavyotumia lugha kupanga visa na matukio, uteuzi wa mandhari, falsafa anayoiwasilisha, ujumbe, dhamira na kadhalika.

1.6.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

William (1958) anasema mielekeo ni kipengele cha maono. Sayansi ya mawazo na uchanganuzi wa mawazo asilia. Mawazo yanayochanganuliwa yakawa yale ya awali ili kuwa na hisi. Ni jambo lisiloepukika kuwa wakulima wengi wadogo hawaelewani na matajiri na wale wa tabaka la kati. Maadamu matajiri ni wachache inamaanisha kuwa maslahi yao yanatofautiana na yale ya wakulima wengi walio maskini na wale wanaolipwa mishahara ya chini.

Althusser (1968) anaelezea kuwa mielekeo ni mawazo yanayounda utambuzi wa miundo ya jamii. Mielekeo inawakubalia watu kufikiria kuwa wanaweza kujiamulia wenyewe jinsi mambo yanavyoendelea maishani mwao. Matukio hayo yanadhihirika katika

mtafaruku wa kitabaka baina ya makundi mbalimbali ya watu. Haya hujitokeza kupitia harakati za kimapinduzi dhidi ya watawala.

Jameson (1981) anasema kwamba ile migogoro ambayo hupatikana katika jamii hutokea kwa sababu za mvutano wa kijamii, kiuchumi na tamaa kati ya watu wa matabaka tofauti. Mapambano yanaweza kuwa katika: vurugu kama vita vinavyotokea kwa sababu ya raslimali na malipo ya kazi, ukosefu wa usalama kazini na kushurutishwa kwa tishio la kufutwa kazi.

Khaemba (1999) katika tasnifu yake ya "Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi" katika riwaya za *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* anaelezea kwamba Uhalisia wa kijamaa hupambanua maisha kama vitendo na uzalishaji ambao lengo lake ni maendeleo bila kizuizi cha uwezo wa binadamu dhidi ya nguvu za mazingira.

Nadharia hii ilizuka pale wanajamii walipongundua kwamba mahitaji ya jamii yanatawaliwa na mahitaji ya kiuchumi na wala si fikra za watu ama majaliwa. Uhalisia wa kijamaa inaelezea jinsi jamii ilivyo na huonyesha mikinzano iliyomo katika jamii na chanzo chake. Nadharia hii inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kuunda jamii mpya itayokuwa bora zaidi.

Kamunde (1983) katika tasnifu yake ameshughulikia "Unyonge wa Uchumi" uliomo katika tabaka la chini katika jamii. Aidha, anajadili kiburi cha watukufu katika riwaya ya *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), na *Dunia Mti Mkavu* **(**1980). Kamunde anakusudia kuwajadili wahusika mbalimbali na jinsi wanavyodhihirisha unyonge wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kutokana na uhakiki huu, uhalisia wa kijamaa unadhihirika

zaidi katka riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (1980). Katika riwaya hii, wahusika wanajaribu kuboresha hali yao ya maisha kwa kufuata mwelekeo wa uhalisia wa kijamaa.

Jambo hili linashadidiwa katika uhakiki wa Mazrui (1984) anapojadili namna maudhui ya mapinduzi yanavyojitokeza katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (1980) kwa kutumia nadharia ya Kimarx. Utafiti huu wa Mazrui utatufaa tutakapochanganua mielekeo ya mwandishi kiuchumi na kijamii.

Kimani (1997) ametumia nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa kujadili maudhui ya kimapinduzi katika riwaya za visiwani hususan zilizotungwa na waandishi Shafi Adam Shafi, Mohamed Said Mohamed na Said Ahmed Mohamed. Uhakiki wa Kimani unajadili utabaka, migogoro inayotokea katika haya matabaka, chanzo cha migogoro na kulipuka kwa mapinduzi. Uhakiki huu utatuongezea ujuzi kuhusu mapinduzi na faida yake huko visiwani. Kazi hii inawiana na ya Kimani, kwani mwandishi Shafi Adam Shafi anaelezea jinsi migogoro ilivyojitokeza huko bandarini na viwandani. Jambo hilo liliwafanya waafrika kuwatumikia waajiri kisha kulipwa mishahara duni.

Hussein (1971) ameuhakiki "Ufundi wa Abdulla (1960) katika **Mzimu wa Watu wa Kale."** Kwanza, alieleza mbinu ya maelezo inayotoa picha kamili ya kinachoelezwa. Kwa mfano, Abdulla (1960) anapoeleza kuhusu chumba huandika kama anayekiona chumba chenyewe huku akiandika. Anasema hii humfanya msomaji akione chumba mbele yake. Mbinu hii huleta raha ya usomaji. Maoni yake yatatufaa katika kubaini mbinu za masimulizi na maelezo kwa undani zaidi. Utafiti huu utatufaa kwani tutazingatia jinsi mwandishi Shafi Adam Shafi alivyochora taswira.

Weche (2000) amechambua vitabu vya fasihi kwa Kiingereza vya Ezekiel Alembi kwa kuzingatia “mtindo na upokezi.” Anatoa maoni kwamba, vitabu hivyo vina ufundi mkubwa katika uandishi na hivyo kuwavutia watoto. Kazi yake imetufaa hasa kwa upande wa uhakiki wa kimtindo. Tofauti ya kazi yake na hii ni kwamba ameshugulikia fasihi ya Kiingereza, ilhali utafiti huu umeshughulikia mwandishi wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti wake umegusia vipengele vichache vya kimtindo tofauti na utafiti huu ambao utazama zaidi katika matumizi ya mbinu za kuwasilisha kazi inayohakikiwa.

Kamau (1992) amezingatia “Ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla” kwa kuchunguza mbinu za ubunifu na zile za uhamishaji wa maana. Utafiti huu utatufaa kwani umezingatia mbinu za lugha ambazo hutumika kuelezea mtindo wa mwandishi. Utafiti wake ulitufaa kwa namna mbavyo utatuekekeza kujua mbinu za uandishi kwenye riwaya. Baada ya kuzijua mbinu hizi ambazo zimo kwenye riwaya teule na ambazo zimetokana na riwaya.

Osore (1994) amehakiki kiisimu riwaya za Suleiman Mohammed katika viwango vitatu; sintaksia, semantiki na isimu-amali kwa kuziweka riwaya hizo katika miktadha ya kijamii na kihistoria. Aidha, alichunguza jinsi matumizi ya methali yanavyosaidia kuendeleza maudhui na mwishowe alilinganisha mitindo ya waandishi katika riwaya zote. Utafiti huu utatufaa tutakapoangalia mtindo alioutumia mtafiti. Utafiti wake unawiana na huu pale ambapo alionelea kuwa kuna mambo kadhaa yanayomwathiri mwandishi wakati anapoiandika kazi yake. Kwa mfano, mikinzano ya kitabaka na ya kimapinduzi kama inavyojitokeza katika kazi hii.

Wanyama (2007) ameshughulikia maudhui na mtindo katika utendi wa Wabukusu *"Khuswala Kumuse."* Katika mtindo alibainisha mtindo wa uwasilishaji katika utendi huo. Utafiti huu utatufaa tutakapochunguza mtindo wa uwasilishaji aliotumia mwandishi Shafi Adam Shafi kuwasilisha maudhui yake. Utafiti wake ni tofauti na huu kwani ulichunguza utendi nao huu umezingatia riwaya.

Kairu (2005) ametumia nadharia ya kimtindo alipotafiti juu ya uhalisi na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Utafiti wake utatufaa kama marejeleo muhimu ya Nadharia ya Kimtindo. Utafiti wake ni wa uhalisi na mtindo nao huu ni wa mtindo na mielekeo. Kwa hivyo, tafiti hizi ni tofauti. Uhalisi aliotafiti una uwiano na mambo ya uhalisia wa yale anayoshughulikia mwandishi Shafi Adam Shafi katika riwaya zake za *Kuli* na *Haini*. Matukio ya kila siku katika jamii ya kisasa, migomo ya wafanyakazi katika nyanja mbalimbali na kufungwa kwa watu wasio na hatia huku wengine wakiuawa ili kutupilia mbali ushahidi katika kesi zinazowahusu watu mashuhuri.

Gitonga (2011) amechanganua taathira ya dhamira na mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Utafiti wake umekuwa mwanga kwetu kufahamu zaidi kuhusu nadharia ya kimtindo, mihimili yake na uamilifu wake kwa ujumla.

Musembi (2008) ametumia nadharia ya kimtindo alipochunguza "Matumizi ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za G. K. Mkangi *Mafuta* (1984) na *Walenisi (*1995)." Utafiti wake utatufaa tutakaporejelea kuhusu Nadharia ya Kimtindo. Utafiti wake ni tofauti kwani alichunguza taswira na ukinzano ilhali huu utachanganua mtindo na mielekeo. Maoni yake kuwa riwaya inaweza kutumika kama kichocheo yanaingiliana na tuliyonayo kuhusu riwaya za mwandishi Shafi Adam Shafi kwani

masuala anayojadili ni ya kuwahamasisha wanajamii waweze kuiona dhuluma na unyanyasaji wanaopitia chini ya watawala na waajiri wao

1.7 Mbinu za Utafiti

Utafiti wetu ni wa maktabani. Ili kufanikisha utafiti wetu hatukuwa na budi kujihusisha na mbinu mbalimbali ili kutimiza madhumuni yetu. Kwanza, tumesoma riwaya ya *Kuli* (1979) na ya *Haini (*2003) ili kuzielewa kwa undani zaidi kwa lengo la kuzichanganua vilivyo. Tumedurusu vitabu, tasnifu na makala yanayohusiana na utafiti wetu. Pia, tumesoma ili tuweze kuyajibu maswali ya utafiti na kuyafikia malengo yetu ya utafiti huu. Kisha tumechanganua mazingira na mielekeo ya mwandishi ya kijamii, kihistoria, kiuchumi na kimapinduzi. Hatimaye, tumechanganua mtindo wa mwandishi kupitia mbinu za uandishi za ukiushi na uchimuzi.

1.7.1 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni wa kimakusudi kwani vitabu vyote vinne vya Shafi Adam Shafi vingefaa kutafitiwa. Hata hivyo, vipengele tulivyohitaji ili vitusaidie kupata data ya kuchanganua katika utafiti huu vilipatikana katika riwaya mbili teule. Kwa hivyo, riwaya ya *Kuli* na *Haini* ziliteuliwa. Tumeweza kuelezea na kuyafafanua baadhi ya mazingira na mielekeo yake ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi. Tumeuchanganua mtindo wa mwandishi katika riwaya hizi kwa kuzingatia mbinu za ukiushi na uchimuzi.

1.7.2 Ukusanyaji wa Data

Data inayoelezea kuhusu mtindo na mielekeo ya mwandishi imekusanywa kwa kuvisoma vitabu vyake na vitabu vingine vinavyohusiana na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na nadharia ya Kimtindo. Riwaya zilizoteuliwa za *Kuli* na *Haini* tumezisoma ili

kuchanganua mazingira na mielekeo ya mwandishi ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi. Mwishowe, kuuchanganua mtindo wake wa uandishi kupitia mbinu za ukiushi na uchimuzi.

1.7.3 Uchanganuzi wa Data

Data ilipangwa kwa kuzingatia mielekeo na mtindo katika sura ya pili, tatu na ya nne. Kisha, data hii ilichanganuliwa kwa kuzingatia jinsi matumizi ya mbinu za ukiushi na uchimuzi yanavyowiana na riwaya, kuonyesha mielekeo ya mwandishi na mtindo wa uandishi wa riwaya. Haya yote ni kwa kutaka kuliziba pengo la utafiti ambalo ni kuonyesha mielekeo na mtindo katika uandishi wa riwaya teule za Kiswahili. Uchanganuzi pia ulilenga kujibu maswali yaliyohusiana na utafiti huu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na nadharia ya Kimtindo.

1.7.4 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji mifano mwafaka. Maelezo yalitolewa katika sura tano zifuatazo: Pendekezo, mazingira na mielekeo, uchimuzi na ukiushi wa maneno, ukiushi na uchimuzi wa maana na hitimisho.

1.8 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza tumezingatia usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

SURA YA PILI

MAZINGIRA NA MIELEKEO

2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumezingatia usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Katika sura hii tumeshughulikia lengo letu la kwanza na la pili na kulijibu swali la kwanza na la pili. Tumechanganua mazingira na mielekeo ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi katika riwaya za *Kuli* na *Haini***.**

2.1 Mtunzi na Mazingira Yake

Mwandishi wa riwaya za *Kuli* (1979) na *Haini* (2003), Shafi Adam Shafi hakutunga kazi yake katika ombwe tupu, ila alizitunga kutokana na mazingira yaliyomlea. Alichota malighafi yake kutoka katika matini mbalimbali za kitamaduni, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika mazingira hayo, kazi yake inaingiliana na kuathiriana na mazingira alimokulia na kuishi. Athari hii inadhihirika katika riwaya hizi mbili.

2.2 Mazingira Yaliyomwathiri katika Uteuzi Wake wa Mielekeo

Taathira au matokeo ya yale yaliomwathiri mwandishi ni kumwezesha kuziandika riwaya zake zenye matukio ya uhalisia zinazojikita katika jamii yake. Mwandishi hakuweza kujitenga na hali za kihistoria zilizoikumba jamii aizungumziayo. Ufaafu wa nadharia ya uhalisia wa kijamii unajitokeza wazi kwani mhimili wa sita unaafikiana na yale anayoelezea mwandishi kwa kuwatumia wahusika wa kimaendeleo. Wahusika

wanaonuia kubadilisha hali yao ya maisha na wenye nia ya kumiliki njia za kuzalisha mali.

Engels, katika Bisztray (1978:17) anasema uyakinifu humaanisha kuwasawiri wahusika katika hali halisi. Mwandishi Shafi Adam Shafi alizingatia hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizoyafanya mapinduzi ya visiwani Zanzibar mnamo Januari 12, 1964 kuwa jambo lisiloepukika.

Mwandishi anaelezea jinsi Rashidi na wenzake walivyopanga mgomo katika riwaya ya *Kuli* ili kudai haki yao. Wao hawakufua dafu, kwani walipigwa sana na askari. Mwandishi anasema:

“Hapo tena walimchukua kitikiti na kumtia ndani ya gari la polisi” (uk. 165).

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anaelezea kuwa Kiongozi Kigogo aliuawa baada ya kupora mali ya uma mwandishi anasema:

"Kigogo ameuawa” (uk. 13).

2.2.1 Mazingira na Mielekeo ya Kijamii

Mwandishi amelishughulikia suala la dawa za kulevya kwa kutambua kuwa ni tatizo sugu katika jamii. Sio tatizo la mitaani bali limeziathiri jamii katika maeneo ya kazi, shule na taasisi nyingine zozote ndoa ikiwemo. Ni tatizo ambalo linawaathiri watu wa kila umri kuanzia vijana wa shule hadi watu wazima. Katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anaonyesha mielekeo yake kuhusu dawa za kulevya anapoelezea jinsi Rashidi alivyoingilia ulevi anasema:

Ulevi ulikuwa umemchukua Rashidi, anayumba kama kishada.

Salum alikuwa anamzuia asianguke (uk. 120).

Katika riwaya ya *Haini,* mwandishi anaiweka wazi mielekeo yake kuhusu dawa za kulevya anasema:

> *Keshakutana naye uso kwa uso amekumbatiana na kimwana barabarani, amelewa chopi (uk. 1).*

Tunaonelea kuwa matumizi ya dawa za kulevya yamezidi, jambo linalowaathiri vijana kwa wazee.

Mwandishi katika mazingira ya kijamii anadhihirisha mielekeo yake kuhusu afya ya wanajamii. Magonjwa yamekuwa tishio kubwa katika nchi za Afrika Mashariki na hata ulimwengu mzima. Maendeleo na ukuaji wa nchi yoyote hutegemea afya ya wananchi wake na uwezo wao wa kukabiliana na jukumu la ujenzi wa taifa. Kimsingi, kumakinisha mtu na jamii kuhusu afya ni jukumu la Wizara ya Afya, Mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali ambayo yanahusiana moja kwa moja na ustawi wa afya ya mtu binafsi au jamii kwa ujumla.

Hata hivyo, waandishi wa kazi za kifasihi, riwaya zikiwepo wana jukumu la kuihamasisha jamii juu ya masuala yanayowaathiri kama vile ugonjwa wa ukimwi miongoni mwa magonjwa mengine. Ni katika mkabala huu mtunzi ameshughulikia suala la ugonjwa kwa lengo la kuwafahamisha, kuwaelimisha na kuirekebisha mielekeo na mitazamo ya wanajamii kuhusu magonjwa. Anaelezea jinsi babake Rashidi alivyokufa kutokana na ugonjwa wa kiarusi katika riwaya ya *Kuli* anasema:

> *Ugonjwa wa kiarusi ambao ulimlaza kitandani mpaka kufa kwake (uk. 8).*

Aidha, mwandishi anaangazia afya ya mamake Rashidi ambaye alikuwa akiugua sana anaposema:

Ah! Ndio hivyohivyo, hauchi unakucha, mara kichwa, mara miguu,

mara homa almuradi hana uzima kitu (uk. 33).

Mhimili wa tano wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa unawiana na matumizi ya lugha anayotumia mwandishi. Lugha rahisi inayoeleweka anapoendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii. Anapojadili katika mazingira ya kijamii na kuangazia mielekeo kuhusu masuala ya afya inadhihirika wazi kuwa anayatia maanani matatizo yaliyo katika jamii yake.

Maoni yetu kuhusu afya ya jamii ni kuwa serikali haina budi kujitolea mhanga ili iweze kuwasaidia wagonjwa katika jamii. Kuna magonjwa yanayotishia afya ya jamii hasa ukimwi na kansa. Wajaribu juu chini kutafuta suluhisho la kukabiliana na magonjwa haya ili jamii iweze kuendeleza majukumu yao nayo nchi itastawi.

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi katika mazingira ya kijamii anaelezea jinsi Hamza alivyokuwa mgonjwa akiwa jela karibu afe. Mielekeo yake kuhusu jinsi wafungwa wanavyodhulumiwa inadhihirika anaposema:

Leo ndio kwanza siku ya nne, anaumwa, amekongoka hajiwezi.

Si wa mkono si wa mguu (uk. 88).

Vilevile, katika mazingira ya kijamii mwandishi ana mielekeo kuhusu ndoa. Jambo hili hangeepuka kulijadili kwani ndoa ni msingi wa jamii. Katika muktadha wa kijamii, ndoa ni msingi wa utangamano na mshikamano imara katika jamii yoyote ile. Asasi hii imekumbwa na changamoto nyingi.

Ndoa ni muungano kati ya mwanamke na mwanaume kuishi pamoja kama mume na mke. Katika Bibilia Takatifu Mwanzo 2:21-22, Mungu aliumba Adamu na Hawa akawapa shamba la Edeni waweze kuishi huko pamoja. Kwa hivyo, ndoa ina msingi wake kutoka kwa Maulana.

Taiwo (1984) anasema ndoa bila watoto haina nafasi katika jamii za kiafrika hii ni kwa sababu Waafrika wanaamini kuwa watoto ndio watakaoendeleza jamii zao. Kukosekana kwa mtoto huchukuliwa kuwa mwanamke ndiye chanzo cha shida hiyo naye mumewe sharti amuoe mke atakayemzalia watoto atakao.

Baada ya kuoana, kila mmoja kisheria anahitajika kuwa mwaminifu kwa mwenzake. Akikosa kuwa mwaminifu anayekosewa ana haki ya kuiomba mahakama iibatilishe hiyo ndoa. Matatizo ya aina hii katika ndoa ndiyo yaliyomchochea mwandishi katika riwaya ya *Kuli* kulishughulikia suala hili kupitia ndoa ya Majaliwa na Bi Mashavu anaposema:

> *Ijapokuwa Majaliwa na Bi Mashavu walioana walipokuwa vijana kwa muda mrefu walikuwa hawakubahatika kupata mtoto (uk. 1)*

Vilevile, katika riwaya ya *Haini* analishughulikia suala la ndoa anaposema:

> *Alikuwa ndio kwanza ameoa, mchumba aliyekuwa naye kwa muda mrefu aliyemvumilia visa vyake vyote alivyomfanyia wakati wa ujane wake (uk. 1).*

Pia, katika riwaya ya *Kuli* akaangazia ndoa kati ya Rashidi na Amina anaposema:

> *Ilipofika zamu ya Mzee Dau kutoa mkono alimkamata Rashidi mkono na kumbinya huku akimwambia, "Nimekuoza mwanangu mkae kwa salama na masikilizano, awe mkeo, msikilizane mzae ndume*

na njike (uk. 144).

Matumizi ya nadharia ya Uhalisia wa kijamii yanadhihirika wazi katika uandishi wa mwandishi kwani anayaandika mambo halisi yanayokuwemo katika jamii yake anapoiweka wazi mielekeo yake ya kijamii. Sehemu hii ina msingi wake katika mhimili wa tano wenye kutilia mkazo malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii. Jamii kwa jumla inaunga mkono kuwepo kwa ndoa ili kuiendeleza kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Pia, mwandishi katika mazingira ya kijamii anadhihirisha mielekeo yake kuhusu dini ya wanajamii yake inajitokeza katika riwaya ya *Kuli* anapoelezea kuhusu dini ya Kiislamu anasema:

Siku ya pili baada ya sala ya alasiri Bi Mashavu alizikwa (uk.100).

Aidha, katika riwaya ya *Haini* mwandishi anajadili mambo yanayofanywa katika mwezi wa Ramadhani anasema:

"Huu huwa ni mwezi wa toba na kila mtu hushika dini sawasawa.
Vipindi vyote vitano vya swala hutekelezwa kwa ukamilifu vikiongezewa
na rakaa ishirini za Tarawehe na swala ya Witri kwa wale wacha
Mungu zaidi" (uk. 117).

Vilevile, katika mazingira ya kijamii mwandishi anaweka wazi mielekeo yake kuhusu ushirikina katika jamii yake. Katika riwaya ya *Kuli* anaelezea jinsi Majaliwa na Bi. Mashavu walivyosafiri kushiriki maombi katika mzimu ili kuomba mtoto. Mielekeo yake iliathiriwa na mila na desturi ya jamii yake anasema:

Walikata tamaa ya kupata watoto na hakuna mzimu walioubakisha kutokea Unguja hadi Pemba katika jitihada za kuomba mtoto (uk. 1).

Pia, mwandishi anaelezea jinsi mhusika Mzee Tindo alivyomshauri Rashidi anauliza:

Uliwahi kumpeleka kwa yule Mshihiri Malindi kupiga chuku, au hata yule mzee wa Kinyamwezi anayepita akitembeza ugoro? (uk. 33).

Katika riwaya ya *Haini*, mwandishi anayo mielekeo ya ushirikina anapoelezea jinsi Khadija alivyowazuru waganga anasema:

Alinyanyua macho akamtazama Khadija, "Umeleta vile vitu?" alimwuliza. "Nimeleta," Khadija alimjibu, akatia mkono ndani ya mfuko wa karatasi aliokuwa amechukua akatoa kifurushi akamkabidhi mganga (uk. 186).

Kimani (1997) anasema kuwa katika riwaya za visiwani, tunakumbana na makundi yafuatayo; Watamba-na-njia, mafahali, watumishi, wafanyakazi wa mashamba na mjini, mamwinyi na mabepari. Asili yao ikiwa Waafrika waliwekwa pembezoni mwa ardhi yenye rutuba na wale wenye asili ya utumwa. Pia, katika muundo wa kijamii visiwani, rangi ya mtu ilimwelekeza katika tabaka maalum la kijamii. Rangi na tabaka vikaandamana; vikatiana nguvu. Tabaka la mtu lilitegemea rangi yake kwa sababu nafasi za kujiendeleza zilifuata rangi.

Waingereza na Wahindi walikuwepo katika shughuli za viwanda na biashara. Waarabu wakashughulika zaidi na umilikaji wa mashamba, nao Waafrika wakawa ndio wafanyakazi. Baadhi ya waafrika walipalilia na kuchuma karafuu, wengine wakawa wakwezi wa kuangua nazi, wengine makuli na wachukuzi bandarini, na wengine

watumishi viwandani. Aidha, katika mazingira ya kijamii mwandishi ana mielekeo kuhusu muundo wa kijamii. Anaaelezea kuwa muundo huu ulikuwa wa kitabaka.

Mwandishi ameligusia jambo hilo la kitabaka alipoandika jinsi makuli na wachukuzi walivyoteswa na mamwinyi na mabepari katika riwaya ya *Kuli***.** Watu weusi walinyanyaswa na wazungu na wahindi bila kujali maslahi yao kwa kuwalipa mishahara duni mwandishi anasema:

> *Manafi alikuwa mtu ya daily pay kampuni haiwezi ufikiria yeye kitu chochote, George alisema, huku amekaa juu ya kiti chake chenye kuzunguka huku na huku (uk. 82).*

Mwandishi anadhihirisha mielekeo yake kuhusu mamwinyi na mabepari walivyowanyanyasa makuli na wachukuzi. Mwandishi katika riwaya ya *Kuli* anaelezea kuwa waliwalipa mishahara duni na kukataa kuwahudumia walipokumbwa na ajali bandarini wakipakia meli anasema:

> *Aaaa! akaanguka huku akipiga kelele nyingi kwa maumivu. Wafanyakazi wenzake na wengine waliokuwa karibu walimzunguka huku wakijaribu kumsaidia mfanyakazi mwenzao aliyekuwa akipiga mikambe kama mtu anayekata roho. (uk. 6).*

Wafanyakazi bandarini wengine walikufa wakiwa kazini na hawakufidiwa na waajiri anavyosema mwandishi katika *Kuli*:

> *Makuli wengine waliokuwa juu ya tishari waliruka bandarini kutaka kumsaidia Manafi lakini Manafi alitoweka majini. Maji yote katika sehemu ile yalijaa damu na hii ilizidisha taabu ya kuweza kumwona kwa urahisi (uk. 81).*

Katika riwaya ya *Haini,* mwandishi anayo mielekeo inayodhihirisha muundo wa kijamii anapoelezea hali ya umaskini inayowakumba wanajamii yake anasema:

> *Kule kwenye foleni za mikate mambo ni ya bahati nasibu, kila mtu ana bahati yake. Unaweza ukaupata huo mkate au ukaukosa na ndio maana watu husukumana, wakakabana, wakataka kutoana roho (uk. 179).*

Mwandishi anawachora wanajamii yake wakiwa katika tabaka la chini. Wao ni wafanyakazi vibarua bandarini hasa kuyapakia na kuyabeba magunia ya karafuu, ukuli na uchukuzi wa mizigo, magolorana wa kufagia maghala, ubururaji rukwama, kupakua na kupakia meli. Wengine hupanga magunia ndani ya ghala kubwa la kuweka karafuu. Nao wasimamizi wao George na Morarji walikuwa wamiliki wa kazi kwa hivyo wakawa katika tabaka la juu.

Tunaonelea kuwa unyanyasaji wa wafanyakazi ulikuwepo katika jamii ya mwandishi. Jambo hilo ni la kuudhi kwani anayefanya kazi za sulubu hakufaidika kamwe. Mtaji wote ulinyakuliwa na wachache katika tabaka miliki.

2.2.2 Mazingira na Mielekeo ya Kiuchumi

Katika mazingira ya kiuchumi, mwandishi anadhihirisha mielekeo yake kuhusu ukiukaji wa haki za watoto wanapojaribu kujikimu kiuchumi. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa inasisitiza kuwa wahusika wanaotumiwa kama vipasa sauti vya watunzi hutumiwa kama wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao kama anavyofanya Rashidi. Huu ni mhimili unaoonyesha wahusika katika hali halisi. Mwandishi katika *Kuli* anaonyesha mielekeo inayodhihirisha watoto walivyofanya kazi ili kujikimu kiuchumi anasema;

> *Gunia liliinuliwa na mara likatua juu ya bega la Rashidi. Hakupata maisha yake kuinua uzito kama ule. Aliyumba huku na huku uso ameukunja lakini akaweza kwenda kwa shida. Alikwenda kama mtoto mchanga anapojifunza kwenda. Alilirusha gunia kidogo ili* kuli*weka juu ya rikwama (uk. 38).*

Suala hili linaathiri jamii ya kisasa kwani ukiukaji wa haki za watoto unajitokeza wazi. Katika mkataba wa watoto (2003) African Charter on the Rights and the Welfare of the Child (ACRWC). Tanzania imesaini itifaki ya hiari kuhusu usafirishaji wa watoto na ukahaba wa watoto ili kuwalinda dhidi ya kudhulumiwa kwa kuajiriwa au kunyanyaswa kimapenzi. Pia, serikali ya Tanzania ina nafasi kama msimamizi wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda kuhusu watoto. Tanzania inabanwa na matakwa ya kuheshimu msimamo na makubaliano ya kimataifa ambayo imeyaridhia. Tanzania ilisaini mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto, Convention on the Rights of the Child (1991), (CRC).

United Nations International Children‟s Fund (UNICEF) inatoa maelezo juu ya ukatili dhidi ya watoto Tanzania. Inatoa matokeo ya utafiti wa kitaifa wa mwaka wa 2009 kuhusu ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili, miktadha, matukio ya ukatili wa kijinsia, afya na athari ya tabia kwa ukatili uliotokea utotoni. Umuhimu wa kuridhia CRC na ACRWC upo katika ukweli kwamba zimeweka viwango vinavyokubalika kimataifa na kanuni za msingi kwa ajili ya kulinda haki za watoto.

Tanzania Child Rights Forum (TCRF) katika tamko la jukwaa la haki za watoto kuhusu kazi za watoto katika katiba ilichukua jukumu la kuratibu, kuandaa na kuwasilisha maoni

ya wanachama wake. Watoto na vijana waliwezeshwa kushiriki katika michakato kwa kutoa maoni yao.

Katiba ya Kenya (2010) inaelezea jinsi sheria za watoto zinashughulikia haki ambazo mtoto anastahili kupata na wajibu wa serikali na wazazi. Inaelezea wajibu wa mzazi katika kudumisha hali thabiti zinazoshughulikia mashauri ya watoto na kutoa mwongozo kuhusu maslahi ya watoto, msaada wa kisheria, uangalizi na utunzaji watoto na ulezi.

Wajibu wa serikali na familia ni kuhakikisha haki zao zinalindwa kwa manufaa ya mtoto. Kwa hivyo, mtoto ana haki ya kuishi, kulindwa kutokana na ubaguzi wa asili zao, jinsia, imani, dini, mila, kabila, lugha, maoni, mawazo, rangi, tabaka za kiuchumi, makao, ama uhusiano wa kijamii. Haki ya kuishi, kutunzwa na wazazi na kupata elimu kulingana na mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto. Wapate elimu ya dini, walindwe wasinyanyaswe kiuchumi kutokana na kazi zozote zinazowadhuru kiafya, kimwili, kimawazo ama kuathiri maendeleo yao kimaadili na kijamii ama kudhuru masomo yao. Watoto wasisajiliwe kupigana katika vita kamwe.

Watoto walioathiriwa na vita na maafa ya kimaumbile walindwe na kusaidiwa na serikali. Watoto walemavu wanapaswa kuheshimiwa, lazima wapewe matibabu na mafunzo yasiyolipiwa wanayohitaji ama kwa malipo nafuu, kila panapowezekana. Hata hivyo, ni lazima watoto wakingwe kutokana na dhuluma, kupuuzwa na kufanywa watumwa. Haki za watoto hushughulikiwa na azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za mtoto, 1989. Nao vijana wa miaka kumi na minane kwenda mbele hushughulikiwa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu na sheria zinginezo. Kulingana na

ushahidi wa kihistoria, suala la dhuluma dhidi ya watoto limekuwepo tangu mwanzo wa ustaarabu.

Aries (1962) na Radbill, (1968) wanasema kuwa kwa muda mrefu watoto wamekuwa wakidhulumiwa na asasi mbalimbali za kijamii kama vile; dini, utamaduni na waajiri. Pia, kumekuwa na ushahidi kuwa wazazi wamekuwa wakiwadhulumu na hata kuwaua watoto wao.

Kutokana na visa vingi vya dhuluma dhidi ya watoto kulizuka wakereketwa walioandaa makongamano kuhusu dhuluma hizi. Kutokana na juhudi hizo, mashirika mengi yalianza kuundwa yakilenga kushughulikia watoto pamoja na masuala yanayohusu haki zao. Juhudi za serikali nyingi ikiwemo Kenya zilianza harakati za kutunga sheria ili kumlinda mtoto. Nchini Kenya sheria ya watoto ilipitishwa mwaka wa (2001).

Kuna visa mbalimbali vya dhuluma vinavyoripotiwa katika vyombo vya habari. Hili ni suala nyeti ambalo linahitaji kushughulikiwa. Kwa mfano, uchunguzi uliofanywa na Namwamba (2005) mmoja wa watetezi wa haki za kibinadamu ulionyesha kuwa katika jiji la Nairobi, visa zaidi ya mia saba viliripotiwa katika mwaka wa 2004. Pia, kutokana na ongezeko la kusambaa kwa ugonjwa wa ukimwi, watu hufa kila siku. Katika bara la Afrika kuna watoto wengi mayatima wanaoachwa bila walezi na wengine kuachiliwa mikononi mwa jamaa zao. Wengine huweza kuangukia mikononi mwa walezi wanaoishia kuwafanyia maovu ya kila aina.

Mashirika mengi yalianzishwa ili kuwasaidia mayatima, miongoni mwayo lile la “Nyumbani” nchini Kenya na Wakfu wa Francois Xavier Bagnoud (FXB). Mashirika haya husaidia kuendeleza miradi inayowasaidia wanajamii kiuchumi wanapoendeleza

utafiti wa haki za binadamu. Huwasaidia mayatima na maskini kwa kuwaletea amani na usalama. Wanaofaidika ni wanawake, vijana na watoto. Pia, huwapa wagonjwa dawa za kupunguza makali ya ukimwi. Huwasaidia kwa kutoa msaada wa kijumla unaohitajika na watu hutoa msaada wa kijumla unaohitajika na watu wanaoishi na ukimwi. People Living with HIV (PLWHA), familia zao na wanajamii wakihusisha ukimwi na changamoto zinazoikabili afya ya watu ulimwenguni. Suala kuhusu dhuluma dhidi ya watoto ni miongoni mwa masuala ibuka yanayoangaziwa na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile: United Nations Children‟s Fund. (UNICEF), World Health Organization (WHO) na mengineyo.

Kukataa kuyashughulikia mahitaji ya watoto ya kila siku kunachukuliwa kuwa dhuluma dhidi yao. Mahitaji haya ni kama chakula, nguo, afya, hisia na kuwaheshimu. Utunzaji wa mtoto humsaidia kukua vyema. Wajibu wa wazazi kuwafunza maadili mema hujitokeza wakati huo. Mtoto anastahili kustarehe, ahisi pendo na usalama miongoni mwa watu anaoamini. Dhuluma dhidi ya watoto zina athari nyingi katika maisha yao.

Katika mazingira ya kijamii mwandishi ana mielekeo kuhusu ukiukaji wa haki za mtoto. Katika riwaya ya *Haini* anaelezea kuwa wakati Hamza alipotiwa mbaroni Subira mwanawe alikuwa mchanga. Jambo ambalo lilikiuka haki zake za kulelewa na mzazi wake. Mwandishi anasema:

> *“Hamza aliongoza mbele, mikono juu, akahisi sasa kweli shari imemkabili” (uk. 7).*

Mwandishi analishughulikia suala la haki za watoto katika muktadha wa kijamii akidhihirisha mielekeo yake kumhusu mtoto ambaye ni uti wa mgongo wa jamii yoyote

ile. Watoto ni miongoni mwa viumbe muhimu katika jamii na wanahitaji ulinzi. Kwa kawaida, viumbe hawa huwategemea wazazi wao au wanajamii kuwatimizia mahitaji yao ya kila siku. Ingawa nyumbani wanamoishi watoto hawa mnatarajiwa kuwa makazi yenye usalama mwingi, mnaweza kuwa mahali hatari sana na msimo na usalama kwa watoto. Suala kuhusu dhuluma dhidi ya watoto ni miongoni mwa masuala ibuka yanayoangaziwa na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile United Nations Childrens‟s Fund (UNICEF), Word Health Organization (WHO), Non Governmental Organizations (NGOs), Human Rights Council (HRC), United Nations High Commission for Refugees (UNHCR) na Human Rights Organization (HRO).

Maoni yetu ni kuwa watoto wote wapewe haki zao ili wakue vizuri nayo jamii iendelee kuimarika. Ni jambo la kuudhi sana wakati watoto katika jamii yetu wanapodhulumiwa na kukosa haki zao. Wengi hunajisiwa, huuawa, huchomwa, hukosa mahitaji ya kila siku na hata elimu.

Katika mazingira ya kiuchumi mtunzi anazingatia uchumi wa jamii yake. Mielekeo yake kuhusu uchumi inaelekeza kuwa wanajamii yake walikuwa wa tabaka la chini hivyo basi, kuwa katika hali duni kiuchumi. Mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa wa pili unaelezea umuhimu wa kuzingatia maslahi ya wachochole. Hawa ni mafukara wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela. Mhimili huu unazingatia wahusika waliokuwa katika hali duni kiuchumi. Baadaye waliweza kupigania haki zao kupitia mgomo na mapinduzi, ingawa viongozi wao waliuawa na kufungwa jela. Katika *Kuli* mwandishi anasema:

Michirizi ya jasho lililokuwa likiwatoka wafanyakazi iliweza kuonekana waziwazi kwenye miili yao iliyoharibika kwa vumbi la makaa waliyokuwa wakiyabeba. Kila mtu alikuwa mbioni ana haraka ya kutaka kubeba vikapu vingi ili apate malipo zaidi (uk. 15).

Katika *Haini* ana mielekeo kuhusu shida za kiuchumi zilizowakabili wanajamii yake anasema:

"Nilimtuma akanikopee shilingi kumi hapo dukani kwa Mshihiri." "Unakopa mwanangu halafu uje ulipe nini?"aliuliza Bi Farashuu. "Hali yenyewe nd`o kama hii. Usikope mwanangu ukaadhirika bure! Majirani wakaanza kututia mdomoni (uk. 147).

Kisha anaendelea kuelezea kuwa wanajamii hao hawakuwa na riziki mwandishi anasema:

Watu hujihimu kuamka mapema ili kukimbilia kuwahi foleni katika maduka hayo ya ukoo. Kila mtu na kadi yake mkononi. Na kadi hiyo nayo, nayo pia huitwa kadi ya ukoo. Kama huna kadi ya ukoo basi ujue siku ya ukoo hupati ukoo katika duka la ukoo. Utakufa njaa. (uk. 178).

Mwandishi kupitia mielekeo yake ya kiuchumi anadhihirisha shida zilizowakabili wanajamii yake mpaka wakakopa bila kujali wangelipa lini. Pia, iliwalazimu wapewe chakula siku ya ukoo. Vilevile, katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anadhihirisha mielekeo ya kiuchumi anasema:

Hawa wanatutumia kama punda na kila tunapowaambia habari ya nyongeza ya malipo wanatutia huku wakitutoa huku!" aliongezea kuli *mwingine (uk. 62).*

Maoni yetu ni kuwa kila mtu ana haki kama mwananchi bila kujali ukoo wake. Kwa kweli, jambo hili la kupewa chakula ni dhihirisho la shida za kiuchumi miongoni mwa wanajamii ya mwandishi.

Mwandishi katika mazingira ya kiuchumi analishughulikia suala la tamaa ya pesa katika jamii yake. Mwandishi ametoka katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Hili ni eneo ambalo wanajamii wengi wamezama kwenye lindi la umaskini na hawana matumaini ya kujiopoa. Hali hii haiwezi kubadilika ikiwa hazitabuniwa njia nzuri za kuupunguza na hata kuumaliza umaskini. Juhudi za kuupunguza zinaweza kufanikiwa ikiwa zitaongozwa na malengo dhahiri.

Ni kweli, kuwa pesa huwawezesha watu kuziendesha shughuli zao mbalimbali. Pesa zinamweza mtu kuyatimiza mahitaji yake ya kimsingi kama vile, ununuzi wa chakula, nguo, makazi, elimu na hata afya bora. Hata hivyo, umaskini uliokithiri umesababisha wengine kushindwa kuyatimiza mahitaji haya. Kwa mujibu wa takwimu za kimataifa, mtu huhesabiwa kama maskini ikiwa pato lake kwa siku ni dola moja. Kwa sababu hiyo, baadhi ya watu wameingiwa na tamaa ya kutaka kujirundikia pesa pasi kujali maisha ya wengine. Maoni yetu ni kuwa kama suluhisho la ufisadi lingepatikana basi hakungekuwa na watu wachache matajiri na walio wengi kupita kiasi kuwa maskini. Suala hili linafaa kushughulikiwa na viongozi ili kuitatua shida hii.

Mtunzi analiguzia jambo hili katika riwaya zake anapoelezea jinsi waajiriwa walivyonyanyaswa na vile uongozi huko Unguja ulivyowakandamiza wanajamii mpaka wakaamua kuchukua hatua ya kujikomboa. Kwa mujibu wa mhimili wa sita wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa, wahusika wanastahili kubadilisha maisha yao. Hivi ndivyo kina

Rashidi walivyofanya walipoanzisha mapinduzi bandarini kupigania haki yao ya kuongezewa mishahara. Jambo hili linadhihirisha ufaafu wa nadharia hii katika uchambuzi wetu.

Kimani (1997) anelezea kuwa katika mfumo wa uzalishaji mali ambapo walio wengi hawana njia nzuri ya kujiruzuku, inatarajiwa kwamba kutakuwa na tamaa kubwa na uporaji wa mali miongoni mwa wale wenye nguvu kisiasa na kiuchumi. Ufisadi utakuwa na nafasi kubwa katika maisha. Aidha, pupa hiyo itazidisha ubinafsi kwa sababu mtu atayafikiria maslahi yake mwenyewe na sio mno kujali maslahi ya wengine. Kwa vile pupa hii mara nyingi hupatikana miongoni mwa tabaka tawala lenye nguvu, walio wengi hujikuta katika dhuluma. Hali hii husababisha kuweko kundi kubwa la watu wenye hasira na ghadhabu, japo za kibinafsi dhidi ya tabaka tawala. Hili baadaye husahilisha kuweko kwa mlipuko wa kisiasa hasa baada ya watu kupevuka kiurazini. Mwafrika akakengeushwa na ardhi ambayo tangu hapo kale ilikuwa yake, hali hii pamoja na uchaguzi wa 1963 uliowapendelea Waarabu, ni baadhi ya mambo yaliyosababisha mapinduzi 1964.

Mwandishi anawasawiri baadhi ya wahusika wakidhihirisha kuzingatia maslahi yao pekee. Katika riwaya ya *Haini* anaonyesha jinsi Kiongozi Kigogo alivyoongoza Unguja kwa pupa ya mali akawasahau wananchi walioendelea kuteseka maishani hadi akapigwa risasi akafa mwandishi anasema:

> *Sukari hakuna, ukisema unatiwa ndani! Mchele hakuna ukisema unatiwa ndani! Sasa maisha gani haya? "Bora walivyomtoa roho (uk. 89).*

Katika riwaya ya *Kuli* tunakumbana na Mzee Tindo aliyekuwa kiongozi wa kundi la wachukuzi wa karafuu katika ghala la Clove Growers Asociation (CGA) badala ya kuwakilisha maslahi ya wafanyakazi wote aliwakilisha maslahi ya mabepari. Ndiye aliyemfahamisha Morarji kuhusu mipango ya wachukuzi ya kuwasilisha matatizo yao.

Anajipendekeza kwa waajiri wake kusudi apewe tonge. Ni wazi kuwa usaliti kama huo unaorudisha nyuma jitihada za kujikomboa unatokana na ubinafsi wenye misingi yake katika pupa ya kujifaidi wakati wengine wanateseka mwandishi anasema:

> *Mzee Tindo aliaga mara huku akihisi amemfanyia Morarji hisani kubwa. Alitoka nje na kurejea kwake""" (uk. 50).*

Pia mwandishi anasimulia hali ya wafanyakazi katika kampuni ya Smith Mackenzie ambayo ni ya mabepari wa Kiingereza iliyomikili gati ya Unguja chini ya usimamizi wa Bwana George. Hali kadhalika, kampuni ya wakuza karafuu chini ya usimamizi wa Morarji ndiyo iliyowaajiri wachukuzi kama Mzee Tindo mwandishi anasema:

> *Mzee Tindo na wenzake waliingia ndani ya ghala wakaanza kutwishana magunia ya karafuu na kuyapakia juu ya rikwama (uk. 37).*

Kwa hakika, unyanyasaji wa wafanyikazi bandarini ndio chimbuko la mgomo. Kwa hivyo, umilikaji wa ardhi na viwanda ni sehemu muhimu ya uendelezaji wa ubepari wa kilimwengu. Utawala wa Kiingereza ulilinda hali hiyo ili ufaidike kiuchumi.

Riwaya za mtunzi zinatusimulia umwinyi wa kiarabu ukienda sambamba na ukisaidiana na ubepari wa kimagharibi katika uporaji wa mtaji kutoka visiwani Unguja. Wenyeji wakawa watoa jasho ili kutengeneza thamani ya ziada kwa manufaa ya tawala za kigeni.

Kwa hivyo, mwandishi alidhihirsha mielekeo yake kuhusu muundo wa uzalishaji mali katika uandishi wake alipoiandika riwaya yake ya *Kuli* inayoonyesha unyanyasaji wa wafanyakazi bandarini. Kimsingi basi, umilikaji wa nyenzo kuu za uzalishaji mali kabla ya mapinduzi umefungamana na ukoloni visiwani.

Mwandishi anaelezea jinsi wakoloni walivyowanyanyasa wafanyakazi viwandani na kuwakandamiza kwa kuwalipa mishahara midogo. Masoko yaliyokuwa wazi na tayari kupokea vifaa kwa bei nafuu yaliwafaa wakoloni. Ukoloni ulivuruga muundo wa jamii visiwani na kusababisha kuimarisha kwa muundo wa kitabaka. Kundi ndogo lilimiliki nyenzo za uzalishaji mali na kundi kubwa la waafrika likalazimika kulitumikia kundi hilo dogo.

Katika riwaya ya *Kuli* mwandishi amejadili kuwepo na kujiimarisha kwa makundi haya na suala la mapinduzi katika kazi zao anasema:

> *Nyuma ya lile lango kubwa Bwana Ramju alibakia peke yake*
> *amepwelewa na vikaratasi vyake vya rangi ya kibuluu mkononi.*
> *Hakuna aliyekuwa akitaka kazi (uk. 89).*

Mwandishi katika mazingira ya kiuchumi anaiweka wazi mielekeo yake kuhusu elimu na nafasi ya kazi iliyozingatia tabaka la mtu. Nafasi kubwa za elimu ya juu zilitolewa kwa Waarabu, Wahindi na Waingereza. Hii ilimaanisha kwamba waafrika walilazimika kufanya kazi za sulubu za kutumika na kuhudumika. Wengi wao walifanya kazi za kijungu–jiko ambazo hazikuwa na simile bali zilijaa hatari. Kazi zilizokuwa maarufu mjini ni za ukuli na uchukuzi. Jambo hili lilirithiwa na kizazi hadi kingine. Mwandishi aliandika jinsi ukosefu wa elimu ulivyowaathiri waafrika maishani. Alielezea jinsi

mhusika Rashidi katika riwaya ya *Kuli* alivyorithi kazi ya babake ya ukuli kwa sababu hakupata elimu wala ujuzi. Hakuwa na jingine ila kuzitegemea nguvu zake za mikono yake ili kujiruzuku. Mwandishi anasema:

> *Kazi ya kwanza kufikiria ilikuwa ni ya marehemu baba yake, kazi ya u*kuli *(uk. 8).*

Ilimbidi asomewe karatasi za kuwatetea wafanyakazi na wenzake kwani hangeweza kusoma. Baadaye akiwa mtu mzima alihudhuria elimu ya watu wazima baada ya kazi. Mwandishi anasema:

> *Rashidi alianza kudurusu yale aliyojifunza siku ile huku Faki akimsahihisha alipofanya kosa (uk. 78).*

Inadhihirisha wazi kuwa waafrika hawakupata elimu ya juu, ikawa muhali kwao kupata kazi zenye heba na hadhi, badala yake kazi za sulubu. Mwandishi anaelezea katika Riwaya ya *Kuli* kuwa Brek na Ramju ndio waliotoa kazi kwani walitoka katika tabaka la juu bila shaka walipata nafasi nzuri ya kupata elimu. Kwa hivyo, kiwango cha elimu miongoni mwa wanajamii yake kilimwathiri mwandishi katika uandishi alipokuwa akiwateua wahusika wake mwandishi anasema:

> *Taratibu, wakati ulikwenda na ukafika saa moja na nusu king`ora kilimwita kazini George na Wazungu wenzake tu, wakuu wa kampuni ya Smith Mckenzie (uk. 89).*

Maoni yetu ni kuwa ni kweli mtu hupata kazi kulingana na elimu aliyonayo pamoja na tajriba ya kazi yenyewe. Kwa hivyo, elimu itiliwe maanani ili watoto waweze kupewa kazi zenye hadhi na mishahara mikubwa. Uchumi ndio uti wa mgongo katika jamii. Kwa

hivyo, mielekeo yake ya kiuchumi inadhihirisha kuwa alizingatia masuala muhimu katika jamii. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa inawahimiza watu kufanya kazi na kuyainua maisha yao kiuchumi kupitia kumiliki njia za uzalishaji mali. Uchanganuzi huu unaongozwa na mhimili wa nne unaowahimiza watu waweze kushinda unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote ile na hasa katika kazi wanazozifanya.

2.2.3 Mazingira na Mielekeo ya Kihistoria

Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa inazingatia historia ya jamii. Katika mhimili wa kwanza, matukio ya kihistoria husawiriwa kupitia wahusika wanaotekeleza mambo kitabaka na kujitolea kunyakua nguvu za kiuchumi. Mwandishi katika mazingira ya kihistoria anadhihirisha mielekeo yake anapoelezea jinsi kina Rashidi walivyoungana kuupanga mgomo ili kudai nyongeza ya mishahara yao katika riwaya ya *Kuli*. Kwa hivyo, nadharia yetu inafaa katika uchambuzi huu wa kihistoria.

Chinua (1983) anaelezea kuwa uongozi mbaya ndio unaoendeleza shida kama vile ukabila, ukosefu wa uzalendo, ukosefu wa usawa katika jamii, utovu wa nidhamu na hata ufisadi. Alinuia kuzimaliza shida za nchi yake Nigeria kwa kuwahimiza kuzitupilia mbali shida za zamani zilizo vikwazo katika kuendelea kwa nchi. Kupitia ufisadi, migawanyiko ya kikabila, ukosefu wa mpangilio mwema huacha washika dau bila uwezo wa kuiendeleza mipango yao kwa njia ifaayo. Ukosefu wa hali ya kiuchumi na kulinda maliasili imeifanya nchi hii kuendelea kuwa maskini. Licha ya kupatikana kwa mafuta kama rasilimali.

Kimani (1997) anasema ni bayana kuwa taifa la kigeni lililoathiri sana historia ya visiwani Zanzibar baada ya kuimarisha ukoloni wake kwa mapana na marefu ni la

Kiarabu. Ukoloni wa Kiarabu visiwani Zanzibar unapaswa kutazamwa huku ukifungamanishwa na matukio ya bara Ulaya hasa baada ya mapinduzi ya viwanda. Huu ndio wakati watumwa walinunuliwa na kusafirishwa na vilevile malighafi nyingi ikahitajika katika utengenezaji wa vifaa viwandani. Zanzibar palikuwa pahali pazuri pa kufanyia biashara kwa sababu ya bandari zake nzuri zenye maji safi. Aidha, Zanzibar ilipendeza kwa kukaribiana na mwamba wa Afrika Mashariki na usalama iliyotoa dhidi ya makabila makali ya bara. Vilevile, mikarafuu na minazi ilikua vyema sana katika sehemu hiyo. Navyo visiwa vya Zanzibar vilikuwa vya kutamanika.

Pia anaelezea kwamba dalili za udhaifu wa utawala huanza kujibainisha polepole hasa katika matini zilizojificha kama manung‟uniko, uvumi, visa, maandamano, maandishi ya chini kwa chini, migomo na kadhalika zinazolipuka mara kwa mara. Kila panapokuwa na ukandamizaji lazima pawe na ukinzani. Haiwezekani kamwe binadamu akandamizwe bila kukinzana na nguvu zinazomkandamiza. Kwa mfano, mwandishi anaelezea matumizi ya maandishi ya kuwajulisha watu kuhusu mgomo anasema:

> *Kwa muda mfupi tu karatasi zile zilikwisha tawanyika sokoni pale pote na wachukuzi walikusanyana vikundivikundi wakisoma karatasi zile (uk. 179-180).*

Mwandishi katika riwaya ya *Haini* anaelezea jinsi Kiongozi Kigogo wa Unguja alivyouawa baada ya kutawala na kuwakandamiza wananchi. Jambo hilo lilimwathiri mwandishi akaiandika riwaya yake akizingatia tukio hilo la kihistoria, akaelezea jinsi watu walivyoteswa baada ya kushukiwa kuwa wauaji wa kiongozi huyo anasema:

Alilazwa chali, akageuzwa, akalazwa kifudifudi, "Wanani….! Hakuwahi kumaliza kauli yake, alisokomekwa tambara kinywani likamjaa tele, akabakia kunguruma tu, M-m-mmmmm. Maneno yamezuiwa hayatoki tena, ametiwa kizibo, cha mdomo (uk. 65).

Pia, anaonelea kuwa uhasama uibukao kwa sura ya mikinzano una misingi ya kiuchumi. Wale wanaomiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali hung‟ang‟ania thamani ya ziada kubwa iwezekanavyo. Ilhali wale wanaokandamizwa hutaka kujihami kwa kuzuia nguvu na jasho lao visitumiwe sana kwa manufaa ya wachache kwa hivyo, huwa kuna vita vya kila wakati. Kwa mfano, wafanyikazi huunda vyama vyao nao waajiri wakishirikiana na utawala hujitahidi kupunguza nguvu za vyama hivyo kwa kuviingilia na kuwasihi viongozi wake. Almuradi, makundi haya mawili hutazamana na kukabiliana kwa uhasama. Mikinzano yake mara huwa wazi ikabainika lakini mara nyingine hujisetiri na baadaye hujitokeza kwa kishindo.

Maoni yetu ni kuwa hakuna binadamu anayependa idhilali bali daima yuko mbioni kuikabili hali inayomkandamiza ili imfae. Pia, hataweza kuvumilia kuteswa sharti atajikomboa. Jambo linaloshuhudiwa Kiongozi Kigogo alipouawa.

Utawala ni uhusiano baina ya wananchi na viongozi wao, lakini pia ni utaratibu unaowapa wanajamii fursa ya kushiriki kikamilifu kufanya maamuzi katika mambo ya msingi yanayohusu maisha yao ya kila siku. Lazima kuzingatia sifa kuu za utawala bora kama vile, katiba bora, demokrasia, sheria, sera nzuri, uadilifu pia uajibikaji. Lazima maoni ya walio wengi yasikilizwe na kutimizwa.

Kimani (1997) anasema kuwa asasi za kitawala kama dini, polisi na mahakama zinatumiwa ili kuzima juhudi za wanyonge kutetea maslahi yao. Hili si jambo geni hata kidogo kwa sababu tawala nyingi hujinasibisha na tabaka lenye nguvu za kiuchumi. Visiwani Zanzibar, utawala wa kingereza ulishirikiana moja kwa moja na 44

Waarabu pamoja na mabepari wenye viwanda. Askari wa utawala wa Kiingereza wakatumiwa kuzima migomo na maandamano mwandishi katika *Kuli* anasema:

> *Kabla Bakari hajawahi kugeuka na kutazama kule nyuma, kule alikokuwa kaelekea yeye; kiasi cha mita mia mbili na pale walipo aliona gari nne kubwa zilizofuatana zikiwa zimejaa askari polisi waliokuwa na silaha mikononi mwao (uk. 183).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unawapa wahusika wa tabaka la wanyonge nafasi ya kufumbata masombo kujipa nguvu za kiuchumi. Hata ingawa mhusika Bakari aliuawa aliwaongoza wanajamii yake kuweza kupigania haki zao za kiuchumi. Naye mwandishi anajitahidi kuwakuza wahusika wake, anapomsawiri Hamza akikataa kukubali uhaini naye Rashidi kupevuka kiurazini akawaongoza wenzake kupigania haki zao. Nadharia ya Kimtindo inapendekeza mwandishi awakuze wahusika wake katika mhimili wa nne jambo alilolifanya mwandishi.

Mwandishi anaendelea kuiweka wazi mielekeo yake ya utawala usiofaa anaposema:

> *Bakari aligeuka upande wa pili kutaka kumsukuma askari aliyetaka kumvuta mguu, alipigwa risasi ya kifua na askari mwingine aliyekuwa amejibanza kichochoroni kwa mbali kidogo. Aliruka juu na alipoanguka*

alifikia juu ya mikono ya Faraji. Alipapatika na haikuchukua muda alinyoka sawasawa na kukata roho. Damu zilikuwa zikimtoka kama mfereji (uk. 184).

Watetezi wa haki za wanyonge wanafungwa kwa mujibu wa sheria zilizotungwa kulinda maslahi ya mamwinyi na mabepari.

Pia, katika *Kuli* anaonyesha jinsi Rashidi anavyofungwa jela miaka mitatu kazi ngumu kwani mahakama inatekeleza jukumu lake katika ulinzi wa wakoloni mwandishi anasema:

*Alipoteremka kutoka kizimbani Rashidi alifungwa pingu na kuchu*kuli*wa na askari mmoja mkono wake wa* kulia *na wa pili mkono wa kushoto na kutolewa nje (uk. 198).*

Aidha, wafanyakazi wanapokutana baada ya kifo cha Manafi, askari wa wakoloni wanatumwa ili kuwatawanyatawanya. Katika harakati hizo, lengo la inspekta wa mzungu ni kuchukua mkoba wa Bakari ili afichue siri za wafanyakazi ili aweze kuwamaliza nguvu mwandishi anasema:

Walipofika hapo yule afisa wa mwingereza alitaka kuuchukua ule mkoba wa ngozi wa Bakari, lakini kabla hajawahi kufanya hivyo, Rashidi ambaye alikuwa amekaa mstari wa mbele karibu na pale walipokuwa wamekaa kina Faraji, aliruka na kuuchukua ule mkoba na kukimbia nao kwa kasi kabisa (uk. 86).

Katika riwaya ya *Haini* anaonyesha jinsi asasi ya polisi inavyotumiwa na utawala kuwatesa na kuwadhulumu raia wasio na hatia hata ingawa aliyetekeleza mauaji hayo alikuwa ameuawa mwandishi anasema :

> *Kufumba na kufumbua wakajikuta wameshafika kituo cha polisi cha Malindi, "Haya, shuka!" aliamrishwa. Akashuka, akasindikizwa mpaka ndani ambako alikaribishwa kwa kofi kubwa alilopigwa na mkuu wa kituo. Kofi lile likampumbaza asione chochote ila vimurimuri tu vikimetameta, "mwetu, mwetu !" (uk. 8).*

Maoni yetu ni kuwa askari hushirikiana na utawala kuwadhulumu wananchi. Wao huenda kinyume na kazi yao ya kuwalinda wananchi. Ni dhahiri shahiri kwamba viongozi hawana budi kubadili msimamo wao wa uongozi wa kiimla ama wang‟olewe mamlakani kwa mtutu wa bunduki.

Okello (1967) anaelezea kuwa rangi ya mtu ilikuwa kigezo muhimu katika ugawaji wa raslimali za taifa la Zanzibar. Yaani, kabla ya mapinduzi kulikuwa na ubaguzi wa rangi unaoweza kumithilishwa kwa kiasi fulani na ule wa Afrika kusini. Waarabu walikuwa wakwasi kwa kila hali ilhali Waafrika walikuwa wakata kwa sababu Waarabu ndio walioshika nyenzo kuu za uzalishaji mali kama ardhi. Tofauti hii ya kitabaka iliendelezwa na Uingereza ilipochukua ulinzi wa visiwa hivi mnamo 1890. Waarabu wakapewa hadhi kubwa serikalini na nafasi nzuri ya kwenda masomoni ng‟ambo. Mwafrika akakengeushwa na ardhi ambayo tangu hapo kale ilikuwa yake. Okello anatuelezea kuwa hali hii, pamoja na uchaguzi wa 1963 uliowapendelea Waarabu, ni baadhi ya mambo yaliyosababisha mapinduzi ya 1964.

Ngugi (1986) anaelezea kuwa sanaa ya uandishi sio matokeo ya mtu binafsi bali hutokea kwa kuwepo muungano na ushirikiano kati ya jamii. Kwa hivyo, sanaa ni matokeo ya historia ya jamii. Kuna uwiano mkubwa kati ya fasihi na jamii. Riwaya za mwandishi zinaonyesha hali za kiuchumi na kijamii zilizosababisha kuwepo kwa mapinduzi ya visiwani mnamo Januari 1964. Kazi ya fasihi inayozingatia uyakinifu wa kijamii ina kiwango cha ubunifu na kiwango cha uhalisia wa maisha. Endapo kazi hiyo itazungumzia matukio ya jamii basi msanii hatakuwa na budi kuonyesha misingi yake katika historia. Uyakinifu una vipengele vitatu, kusimulia hadithi za ukweli, kuwa na wahusika halisi na kuwasawiri katika hali halisi. Hali halisi hiyo ni ya kihistoria. Kwa hivyo, mwandishi hangeweza kujitenga na hali za kihistoria zilizoikumba jamii aliyoizungumzia ili kazi zake ziwe na uyakinifu. Kwa hakika, fasihi huathiriwa na matukio ya kihistoria na hali kadhalika historia huathiriwa na fasihi (hasa fasihi ikichukuliwa kama chombo cha ukombozi).

Kulingana na uandishi wa mwandishi kuna hali za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizoyafanya mapinduzi ya visiwani Zanzibar kuwa jambo la lazima. Fasihi ni chombo cha jamii kinachotumia lugha kiubunifu ili kusheheni imani na matukio katika jamii yake. Kwa hivyo, patokeapo jambo la kihistoria, fasihi hujaribu kuliteka na kulihifadhi kisanaa. Mwandishi alizingatia fasihi ya kimaendeleo iliyowahamasisha wafanyakazi dhidi ya wanyonyaji katika *Kuli* mwandishi anasema:

> *Hali ya kazi ni mbaya. Kazi nyingi na malipo ni madogo sana. Usalama kazini hapana na wengi katika wenzetu washafikwa na ajali bila ya kampuni kuwafidia wao kitu chochote (uk. 153).*

Fasihi ya kimapinduzi haina budi kupata moyo wa uhasama wa kijamii. Uandishi wake unadhihirisha ubunifu wa kihistoria wakati wa enzi ya ‘uimla’ wa wafanyakazi na pia katika uongozi wa kisiasa inavyodhihirika katika riwaya ya *Haini* mwandishi anasema:

> *Huko wakapelekwa kwa yo -yo-yo yo shangwe na vigelegele vya chini kwa chini wasije wakaambiwa wanasherehekea, wakati watu wamo katika maombolezi ya kifo cha Kigogo (uk. 104).*

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi ameonyesha tukio la kijamii linaloonyesha jinsi kiongozi wa Unguja, Kigogo alivyopigwa risasi baada ya wanajamii kulemewa na matatizo chungu nzima kutokana na uongozi mbaya wa kisiasa mwandishi anasema:

> *Kama huna hiyo kadi ya ukoo, basi ujue siku ya ukoo hupati ukoo katika duka la ukoo. Utakufa njaa (uk. 178).*

Ngugi (1981) anasema, kwa sababu ya hali yake ya kijamii, fasihi inaelekezwa na nguvu na msukumo wa historia ya jamii husika, haiwezi kujiepusha na uchumi, siasa, tabaka, rangi au kile akiitacho Chinua „masuala muhimu zaidi ya wakati huo.“ Nayo hujitokeza katika muktadha maalumu kwa sababu yanahusu kiuchumi, kisiasa, kitabaka na rangi.

Almuradi patokeapo jambo muhimu la kihistoria, fasihi hulihifadhi kwa kulihuisha kisanaa. Kwa hivyo, sanaa na jamii bila shaka zimeungana. Hakuna sanaa isiyoathiriwa na taathira za kijamii na hakuna sanaa ambayo kwa upande wake, imekosa kuiathiri jamii. Waandishi wa visiwani wameyatumia mapinduzi ya 1964 kama kielelezo cha yale yawezayo kutokea kokote kwenye madhila kama alivyofanya mtunzi Shafi Adam Shafi.

Matukio ya kijamii yanaingiliana, Inambidi msanii basi ayatazame kuwasilishiwa hadhira yake. Lakini, huku mengine yakiwa ghafi mengine safi. na kisha akate kauli kuhusu

yale yafaayo aghalabu kabla msanii hajazama katika uhalisi wa kilimwengu, chanzo chake huwa ni jamii fulani finyu. Hali zilizoikumba jamii hiyo hupewa muktadha mpana ili zisigubike jamii pana. Hii ni kwa sababu msanii ni mja wa wakati, jamii yake, utamaduni maalum na tabaka maalum. Aidha, sanaa yote nzuri huibuka katika hali fulani mahsusi lakini ina matokeo ya kilimwengu.

Tunaonelea kuwa sharti mwandishi azingatie masuala yanayowakabili wanajamii anapoandika kwani kuna uhusiano mkubwa kati ya jamiii na fasihi. Matukio ya kihistoria katika jamii humsaidia mwandishi kuelezea jinsi jamii yake inavyoendelea kukabiliana na uhalisi.

Lukacs (1971:73) anaelezea kwamba urazini wa kitabaka ni hisia na ufahamu wa dhima ya kihistoria ya tabaka. Yaani, watu wa tabaka moja huweza kufanya juhudi za pamoja ili waweze kujihami dhidi ya nguvu za tabaka jingine. Hii itawezekana watu wakifahamu mantiki ya tabaka lao na wajinasibishe na matakwa ya tabaka hilo. Pia, wafahamu na wayachukulie mahitaji ya tabaka linguine kama kwamba si halali. Wafahamu na wawe tayari kuchukua hatua ya pamoja ya kisiasa ili kufikia lengo la kisiasa la kijumla na lenye manufaa kwao. Lengo la tabaka lenye urazini ni kujiimarisha na kujihifadhi dhidi ya tabaka linalolikinzana nalo. Kabla ya urazini, watu katika tabaka hilo huvutana wenyewe hasa kwa mashindano au ukosefu wa ufahamu kamili wa adui wao. Wanachukulia kuwa hali yao imesababishwa na baadhi ya watu katika tabaka lao. Kwa hivyo, wanauana na kuibiana. Aidha, wanatafuta suluhu za kibinafsi. Urazini uingiapo ndipo mivutano katika tabaka moja inapoelekezwa dhidi ya tabaka linalokinzana nalo.

Mwandishi katika mazingira ya kihistoria anaidhihirisha mielekeo yake katika riwaya ya *Kuli* anapomtumia mhusika Bakari kama kielelezo cha urazini. Bakari anashirikiana na Faraji katika kuwaelimisha wafanyakazi na kuandaa migomo. Mipango inafanywa ili wafanyakazi wajue kusoma na kuandika. Urazini wao unaamshwa kwa karatasi zinazoelezea hali yao na dhiki zao mwandishi anasema:

> *Lo! Alishangaa yule mtu, mambo makubwa haya. "Alipoinua macho aliona kila mtu sokoni pale amekwisha pata karatasi kama ile aliyokuwa nayo yeye" (uk. 179).*

Vilevile, mwandishi anasema:

> *Chama kilijaribu kila njia kuwasidia lakini pesa ambazo walipata msaada kutoka kwa wafanyakazi wenzao huko Dar es Saalam na zile walizochangishana wenyewe zilikuwa zinakaribia kumalizika (uk. 170).*

Mwandishi anaonekana akisisitiza nafasi ya umoja wakati wa mgomo pale ambapo chama cha wafanyakazi wa Tanganyika kinazisaidia aila zilizolemewa sana. Mhimili wa tatu unawaonyesha binadamu wanaotumiwa kama vipasa sauti vya watunzi ambao hupuliziwa uhai kama binadamu wa kawaida katika ulimwengu tunaoujua. Kwa mfano, Bakari anayepigwa risasi akiwatetea wanajamii yake. Jambo hili hudhihirika katika jamii watu wanapotetea haki zao. Ushirikiano wa wafanyakazi nje ya mipaka ya taifa ni kielelezo cha umoja wa maslahi yao wote ulimwenguni mwandishi anasema:

Kwa sababu hii, Bakari alikuwa heshi safari za Dar es salaam ili kushauriana na kutafuta misaada kutoka kwa ndugu zao, wafanyakazi wa bandarini wa huko (uk. 145).

Mwandishi anazingatia umoja huu ili kuyaleta mabadiliko yenye maana katika mataifa yenye dhuluma. Lakini umoja huu utawezekana kupitia kwa vyama vyenye viongozi kama Bakari waliopevuka kiurazini bali si kutokana na viongozi kama Mzee Tindo wanaozifikiria nafsi zao tu na ambao wako tayari kuisaliti nafasi ipatikanayo. Anamsawiri Mzee Tindo kama wale viongozi wasiopevuka kiurazini na wanaojipendekeza ili wapate makombo kutoka kwa waajiri wao. Ingawa wanajua wananyonywa hawawezi kuchukua hatua madhubuti kujikomboa kwa sababu wanajiona afueni kuliko wenzao mwandishi anasema:

Basi kama wewe nasema pesa haitoshi kwenda tafuta kazi pahala ingine iko pesa mingi!" Morarji alimwambia Rashidi kwa ufidhuli, kisha akamgeukia Mzee Tindo na kumwambia, "Tindo! Hapana chukua yeye kazini tena, haya! Jao!" (uk. 51).

Aidha, katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anaelezea kuwa mfanyakazi mwenye urazini wa kitabaka hujikuta wakati mwengine akikinzana na aila yake kwa sababu wanaona kama wanapuuzwa. Mielekeo ya mwandishi kuhusu jambo hili ni kwamba panapotokea mvutano baina ya masuala ya kibinafsi na ya umma, basi yale ya kibinafsi yafaa yapuuzwe. Anaelezea kuwa ndoa ya Amina na Rashidi inatokea wakati Rashidi anapevuka kiurazini na yuko mbioni kushirikiana na wafanyakazi

wenzake katika kukabiliana na mfumo wa kibepari. Hii inamlazimu ahudhurie mikutano ya usiku mara kwa mara. Amina naye anachukulia kwamba anapuuzwa. Hata hivyo, anapevuka baada ya kuuona ukweli. Jambo hili linadhihirisha matumaini kwamba ijapokuwa Rashidi amefungwa, amemwacha mkewe akiwa na mwamko na matumaini kuwa madhila hayo yataisha mwandishi anasema:

> *Usiku ule walilala bila hata kuzungumza na hata walipoamka asubuhi Amina alikuwa bado amenuna na Rashidi alitoka na kwenda zake kazini bila ya kuzungumza kitu chochote na mkewe (uk. 149).*

Katika riwaya *Haini* Hamduni alipoamua kumpiga Kiongozi Kigogo risasi na kumuua alikuwa amepevuka kiurazini. Akaonelea sharti angemuua ili wanajamii yake wafaidike kwa kumchagua kiongozi mwengine ambaye angeweza kuwasaidia kuyakimu maisha yao mwandishi anasema:

> *Hakuna asiyejua juu ya usuhuba wako mkubwa na Hamduni na hakuna atakayeamini kwamba jinsi mlivyo wewe na Hamduni, Hamduni awe ndiye muuaji na wewe uwe humo (uk. 264).*

Tunaonelea kwamba watu katika jamii wanafaa kuelimishwa kwamba hali yao duni ya maisha haikutokana na majaliwa kama wanavyofikiria. Wanafaa kusaidiwa waweze kua kiurazini ili waweze kujikomboa. Wazingatie elimu ya watoto wao ambao wataweza kutoka katika tabaka la chini wajiimarishe maishani baadaye. Kisha wawapate viongozi ambao watawatumikia vyema badala ya kujilimbikizia mali ya umma huku maisha ya wanajamii yakiendelea kuwa duni. Nao viongozi

wakichaguliwa wasije wakasahau majukumu yao na kufanya kinyume na matarajio ya wananchi.

2.2.4 Mazingira na Mielekeo ya Kimapinduzi

Skocpol (1979) anasema kwamba mapinduzi ya kijamii ni matukio ya ghafla ambayo yanalifanya tabaka moja kuchukua uongozi wa kisiasa na kuleta mabadiliko katika mfumo wa uzalishaji mali.

Jabir (1977) anachunguza muundo wa kiuchumi kuhusiana na mashamba makubwa ya karafuu visiwani Zanzibar ya 1890 na 1964. Aidha, amejadili vile ukulima huo wa mashamba makubwa ulivyosababisha mapinduzi ya 1964. Suala la mashamba makubwa ya karafuu ni muhimu katika uhakiki wetu kwani mwandishi katika riwaya ya *Kuli* anazungumzia jambo hili.

Kimani (1997) anasema kuwa uhasama uibukao kwa sura ya mikinzano, una misingi ya kiuchumi. Wale wanaomiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali hung‟ang‟ania thamani ya ziada kubwa iwezekanavyo; ilhali wale wanaogandamizwa hutaka kujihami kwa kuzuia nguvu na jasho lao visitumiwe sana kwa manufaa ya wachache. Kwa hivyo, huwa kuna vita kila wakati. Kwa mfano, wafanyikazi huunda vyama vyao, nao waajiri hushirikiana na utawala kujitahidi kupunguza nguvu za vyama hivyo kwa kuviingilia na kuwahasi viongozi wake. Almuradi makundi haya mawili hutazamana na kukabiliana kwa uhasama. Mikinzano mingine hujisetiri na baadaye hujitokeza kwa kishindo. Mapinduzi huchochewa na manung‟uniko, uvumi, visa, maandishi ya chini kwa chini, migomo na kadhalika ni mifano ya matini zilizolipuka mara kwa mara. Nadharia ya Uhalisia ya Kijamaa mhimili wa sita unapendekeza

wahusika wa kimaendeleo wanaonuia kubadilisha hali yao ya maisha kama walivyofanya kina Bakari na Rashidi walipowaongoza wafanyakazi kuandaa migomo kazini.

Katika mazingira ya kimapinduzi mwandishi anaiweka wazi mielekeo yake ya mikinzano ya kitabaka. Mhimili wa kwanza katika nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa unaoana na mielekeo ya mwandishi kuhusu usawiri wa wahusika wanaotekeleza matendo ya kitabaka.

Mwandishi katika *Kuli* anaelezea kuhusu mikinzano iliyokuwepo bandarini mnamo 1948. Wafanyazi kama Maajaliwa walivunjwa na kazi na kizazi chao kikaendelea na kazi zao ili kujitarazaki mwandishi anasema :

> *Hii ndio mandhari Rashidi aliyokuta bandarini. Hapo ndipo baba yake aliponyonywa uhai wake akafa bila chochote. Unguja bandarini mwaka 1948 (uk. 9).*

Pia mwandishi anasema:

> *Wakati wa kusukuma rikwama yeye ndiye aliyekuwa mshika usukani, wenzake walikuwa wakipanga magunia ndani ya ghala kubwa la mabati lililokuwa mali ya kampuni ya Kiingereza iliyoitwa CGA au kwa urefu "Clove Growers Association" Humo ndimo zilimowekwa karafuu zote za Unguja na Pemba kungojea mabepari wa kigeni wazipeleke nchi za nje (uk. 27).*

Mwandishi katika *Kuli* anaendelea kuelezea kuwa wafanyakazi waliongozana katika kujiandaa kukabiliana na waajiri wao. Baadhi yao kama Bakari, Faraji na Rashidi

wanaojitolea kwa moyo wa dhati ilihali wengine kama Mzee Tindo wananunuliwa. Usaliti ni jambo la kawaida mikinzano ya kitabaka inapochacha. Wasaliti hurudisha nyuma jitihada za ukombozi mwandishi anasema:

> *Bakari! Bakari inuka!" Faraji aliita kwa kelele zilizochanganyika na kilio. Faraji alimlaza Bakari chini na kuinuka kwa hasira. "Ninyi mbwa ninyi! Ninyi madhalimu! Makatili!" alipiga kelele kama mwendawazimu huku akimwendea askari aliyemkabili. Aliipeleka mikono yake shingoni kwa askari na kutaka kumkaba roho lakini kabla hajawahi kufanya hivyo alipigwa risasi ya kichwa na kufa hapohapo (uk. 184).*

Aidha, usaliti unadhihirishwa na Mzee Tindo anapowasaliti wenzake na kupewa pesa na Morarji mwandishi anasema:

> *Alitoka usiku na hakusimama mpaka kwa Morarji, tajiri wao. Alimweleza yote yaliyotokea na bila ya kumjibu Mzee Tindo kitu chochote, Morarji alitoa shilingi kumi na kumpa Mzee Tindo. Alizipokea kwa heshima (uk. 50).*

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anaelezea jinsi wahusika waliokubali kosa la uhaini walivyodanganywa wakadhani wataachiliwa walivyopelekwa kondem kwani walipewa adhabu ya kifo anaposema:

> *Musadiq alisita kidogo akatoa kitambaa kutoka katika mfuko wake wa koti akajipangusa jasho kwenye paji lake la uso.*
>
> *"Mkadam Bakari," alianza kutaja majina; "Haramia Habib."*

Akafuata Mpakani, Sumbu, Marzuku, Vingosho, Zarikani, Pwacha na Kuchi. Wote hawapo pale, tayari washapelekwa kondem" (uk. 264).

Mwandishi anaendelea kudhihirisha mielekeo yake ya kimapinduzi katika *Kuli* anapoelezea jinsi wafanyikazi walivyopanga mgomo wao mwandishi anasema:

Jambo muhimu tunalotaka kukwambieni hivi sasa ni kuhusu mgomo wetu" (uk. 148).

Mwandishi pia anaelezea kuwa Smith Mackenzie hakutaka kuyatimiza waliyodai wafanyakazi nao wakaamua kuweka mikakati ya kudhihirisha madai yao. Kisha wakampa masharti atimize mambo hayo mwandishi anasema:

"Huko kwenye ofisi ya chama cha wafanyakazi wa bandarini, Bakari pamoja na wenzake waliofanya kazi ofisini hapo walikuwa na kazi kubwa ya kutayarisha madai hayo na walipomaliza kufanya hivyo walipiga chapa karatasi chungu nzima zilizoelezea kilio cha wafanyakazi wa bandarini" (uk. 153).

Mhimili wa pili katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa huzingatia maslahi ya wachochole ambao ni mafukara wa ulimwengu wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela. Mhimili huu unalingana na jinsi Bakari na wenzake walivyowatetea maskini katika jamii yao.

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anaiweka wazi mielekeo yake ya kimapinduzi kisha kudhihirisha kuwa wanajamii walikuwa wamechoshwa na uongozi wake mwandishi anasema:

> *"Watangazaji wamelala nini?" aliuliza Hamza kwa mzaha.*
> *Kabla hata hakujibiwa ulisikika mlio uliokuwa na kishindo tu-tu-tu" (uk. 1).*

Mwandishi anaelezea jinsi Hamza alivyowaza na kuwazua kumhusu Hamduni rafiki yake aliyemfanya atiwe mbaroni baada ya kumuua Kiongozi Kigogo mwandishi anasema:

> *Hivi Luteni Hamduni amefanya nini?" Ni rafiki yake wa siku nyingi na amekuwa luteni kwa muda mrefu. Hivi karibuni tu kumekuwa na fununu kwamba angelipandishwa cheo na kuwa Kapten. Sasa inakuwaje tena, leo anasakwa kwa bunduki na mizinga? (uk. 8).*

Mwandishi katika mazingira ya kimapinduzi alidhihirisha mielekeo yake anapoelezea kuhusu nyumba zilizohamwa anaposema:

> *Ni jumba kongwe kama majumba yote ya mji ule. Wakazi wake siyo wale waliokuwa wakiishi humo wakati mji huo ulipokuwa maskani ya wale waliojivisha heshima ya ubwana na utukufu kwa mujibu wa kabila na nasaba zao. Wakati huo majumba hayo yalikuwa mchana yaking`ara usiku*

yakimeremeta. Sasa, hao wameyahama majumba yao na kuhajiri nchi kukimbia zahama za mapinduzi (uk. 189).

Mwandishi anaitumia mielekeo ya kimapinduzi kudhihirisha kuwa binadamu sharti atumie njia zozote zile ili kujinasua kutokana na dhiki inayomkabili. Hata ingawa walioongoza mapinduzi waliuawa haukupita muda mwingi watu wa Unguja wakajipatia uhuru wao. Pia, kupitia mauaji ya Kiongozi Kigogo ni dhihirisho kuwa watu wanaweza kumwondoa kiongozi yeyote yule kama hawatimizii mahitaji yao.

Maoni yetu ni kuwa binadamu aweze kuzitetea haki zake popote alipo. Asipofanya hivyo atajikuta amekandamizwa vilivyo. Maslahi yake hayatatiliwa maanani na ataendelea kunyanyaswa na kuishi katika lindi la umaskini milele. Nao wafanyakazi walipwe mishahara ya kuwatosha na pia masilahi yao mengine yazingatiwe ili waweze kufanya kazi vizuri. Waepuke migomo inayotokea kila wakati. Vilevile, viongozi wa nchi mbalimbali wajue kuwa wanaweza kutolewa mamlakani wakati wowote ule kwa mtutu wa bunduki au kupinduliwa. Kwa hivyo, wawe viongozi wanaozingatia haki na amani. Aidha, binadamu sharti aweze kuzitetea haki zake popote alipo. Asipofanya hivyo atajikuta amekandamizwa vilivyo.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua mazingira na mielekeo ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi. Katika sura ya tatu tutachanganua mtindo aliotumia mtunzi kupitia mbinu za uchimuzi na ukiushi wa maneno kupitia mazugumzo, mlazo, nyimbo msamiati, uradidi wa maneno, misemo na nahau, methali.

SURA YA TATU

UCHIMUZI NA UKIUSHI WA MANENO

3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumechanganua mazingira na kubainisha mielekeo iliyomwathiri mwandishi Shafi Adam Shafi wakati alipoziandika riwaya za *Kuli* na *Haini***.** Mazingira na mielekeo iliyochanganuliwa ni ile ya kihistoria, kiuchumi, kijamii na kimapinduzi. Katika sura hii tumelijibu swali la tatu na tumelichanganua lengo letu la tatu kwa kubainisha mtindo wa mwandishi kupitia mbinu za ukiushi na uchimuzi wa maneno katika riwaya hizi mbili.

Mwandishi Shafi Adam Shafi ametumia kipengele cha mtindo kuwasilisha kazi yake ya kisanaa kwa ustadi ili kisa chake kipendeze wasomaji na kiweze kuwanasa kiasi cha kuwafanya wakifurahie na kukifuata tokea mwanzo hadi mwisho. Mhimili wa nane wa nadharia ya Kimtindo unaelezea kuwa uteuzi wa msamiati uliotumiwa na mwandishi uweze kuleta mvuto kwa msomaji kwa kumtia ari ya kusoma. Kwa kweli riwaya za mtunzi zinamsisimua msomaji kwa hali ya juu. Tumetalii kwa dhati ustadi aliotumia mwandishi kuwasilisha maudhui ya riwaya hizi. Ili kufanya hivyo, tumejadili mtindo wa mwandishi kupitia mbinu za ukiushi na uchimuzi wa maneno.

Nazo sura za riwaya hizi mbili ni nyingi. Riwaya ya *Kuli* ina sura kumi na mbili, zingine ni ndefu na zingine ni fupi. Nayo riwaya ya *Haini* ina sura ishirini na saba na zile nyingi ni fupi, chache ndizo ndefu. Sura hizi huwa zimepangwa kwa nia fulani.

Mhimili wa sita unaafikiana na kazi hizi kwani riwaya hizi zina sura fupi na ndefu kulingana na nadharia ya Kimtindo.

3.1 Mtindo katika Riwaya za *Kuli na Haini*

Riwaya ya ***Kuli*** ina sura kumi na mbili. Hata hivyo, kinyume na matarajio ya masimulizi ya hadithi, masimulizi katika riwaya hii hayajawasilishwa kufuatana na matukio. Katika sehemu kadhaa ule mfuatano wa masimulizi umekiukwa, hivyo basi hadithi imepoteza mtiririko wake. Huu ni ukiushi wa nje uliofanywa kimakusudi na mwandishi na wenye dhima maalum ya uchimuzi unaomwathiri msomaji. Hapo mwanzo wa riwaya hii kwa mfano, mwandishi anaelezea kuhusu Majaliwa. Anasema alianza kazi ya ukuli wakati yungali kijana wa miaka ishirini na mmoja. Anaelezea jinsi Majaliwa alivyokuwa mfanyakazi mashuhuri bandarini, jinsi dongo lake lilivyokuwa zuri kwani alionekana kijana akiwa na umri wa miaka hamsini na mitano. Alikuwa mwingi wa heshima, busara na huruma kwani aliwapa nasaha wenzake kuhusu matatizo ya kinyumbani.

Usimulizi ni uelezeaji wa matukio katika hadithi nayo mazungumzo ni maongezi yanayopatikana kati ya wahusika wa kifasihi. Mazungumzo huhusisha mambo muhimu tu katika uendelezaji wa msuko. Sifa za mazungumzo zinatuwezesha kuwatambua wahusika wanaoshiriki katika maongezi hayo kutokana na uteuzi wao wa maneno, lugha zao na matamshi yao. Dhima ya mazungumzo katika hali ya fasihi uhalisia ni mwelemeo mkubwa wa kuakisi maongezi kama yalivyo katika ulimwengu halisi. Mwandishi huyatumia maandishi kuwasilisha maneno ya wasemaji kwa mkato

bila kuwepo kwa vishikizi kama “ alisema,” “ alifafanua,” na “alifikiri.” Mwandishi huingiza hisia zake kumhusu mhusika fulani au usemi wake.

Mwandishi Shafi Adam Shafi ameyatumia mazungumzo kama mbinu ya ubunifu ili kuwapa uhai wahusika wanapoongea kati yao. Mbinu hii inamsaidia msomaji kuifahamu hulka ya mhusika anapotathmini lugha anayotumia. Mazungumzo pia huipamba lugha na kumfanya msomaji atafakari wanachosema wahusika.

Mtiririko wa usimulizi huu unapotea wakati mazungumzo yanapoingizwa na mwandishi kati ya Majaliwa na mkewe Bi. Mashavu. Ukiushi wa kimakusudi unamletea msomaji ari ya kutaka kujua wahusika hao wanajadiliana kuhusu nini. Kwa hivyo, uchimuzi hutokea. Uchimuzi unaomvutia msomaji zaidi aweze kuendelea kusoma hadithi kwani itampendeza zaidi. Kwa mfano anaposema:

Si kama sitaki kwenda kazini,nataka sana, lakini leo najihisi

Hali yangu naumwaumwa, nahisi kama homa na kizunguzungu (uk. 2).

Mazungumzo haya yanamdokezea msomaji kuwa wanaoongea wanakijua wanachojadiliana. Lakini Bi. Mashavu anaonekana hajui kinachomfanya mumewe awe kitandani wakati wa kazi. Tabia ya Bi. Mashavu ya kumdadisi mumewe haitarajiwi. Mazungumzo haya yanafikia kiwango cha kuchukiza wakati Majaliwa anapomwambia mkewe asimkere. Naye Bi. Mashavu anadhihirisha ujasiri anapoendelea kumuuliza mumewe maswali anapomwambia:

“Sasa si bora nikakutekelea maji ya moto ujimwagie

labda utapata nafuu” (uk. 2).

Kulingana na sauti ya mazungumzo hayo maswali kadhaa yanamjia msomaji ubongoni. Kwa mfano, atajiuliza kwa nini Bi. Mashavu anaongea na mumewe kwa ufidhuli. Lakini badala ya mwandishi kuiridhisha hamu ya msomaji kwa kumweleza tukio la mazungumzo hayo anaendelea kumsimulia kuhusu vile Majaliwa alivyoipenda kazi yake iliyomsaidia kuikimu familia yake. Jambo hili humtia ilhamu msomaji. Kwa hivyo, uumbaji wa hali ambayo msomaji hufanywa kutamani habari zaidi, mwandishi hafaulu tu kuhifadhi mwendo wa msomaji bali pia kuzidisha udadisi wa kutaka kujua kinachotokea. Hii ni kumaanisha kuwa kile msomaji alistahili kusoma mwanzo atakisoma baadaye, kudhihirisha kinyume katika masimulizi. Yafuatayo ni mazungumzo mengine katika riwaya ya *Kuli* kati ya Majaliwa na mkewe mwandishi anasema:

> *"Rashidi kawa mtundu siku hizi," Bi Mashavu alianza mazungumzo,*
> *"Leo nilimwacha hapo katikati kidogo tu mara namsikia yupo nje,*
> *tokea amejua huko kutambaa imekuwa shida." "Nd"o mwanamume,*
> *lazima awe mtundu," Majaliwa alisema. (uk. 5).*

Mwandishi anatumia dayalojia kati ya wahusika wake jambo linaloafikiana na mhimili wa pili wa nadharia ya Kimtindo. Aidha, matumizi ya nafsi ya kwanza na ya pili yanadhihirika. Nafsi ya kwanza hutumika katika usimulizi unaofanywa na mhusika aliye mshiriki wa matukio au matendo ya hadithi au asiwe mshiriki. Aghalabu usimulizi huu hujenga uhusiano wa karibu kati ya hadithi na msomaji. Nafsi ya pili huwa ni usimulizi unaopatikana katika hadithi inayosimulia katika nafsi ya pili. Nayo nafsi ya pili ni usimulizi unaotambulishwa na matumizi ya -li- wakati msimulizi huelezea matukio au mambo yanayomhusu mtu mwingine. Usimulizi huu

umezoeleka sana katika uandishi wa kifasihi. Katika riwaya za mwandishi Shafi tumebainisha usimulizi wa nafsi zote tatu kwa hivyo, mhimili wa tatu wa nadharia ya Kimtindo unawiana na kazi hii kudhihirisha ufaafu wa nadharia hii. Mwandishi anayatumia mazungumzo kati ya mtu aliyeulizwa kazi na Rashidi anaposema:

> *"Nenda kanyonye huko, kazi utafanya mtoto kama wewe? Ondoka usije ukapigwa kumbo ukatumbukia baharini" (uk. 11).*

Mazungumzo yanaonyesha Rashidi akitafuta kazi akiwa angali mtoto mchanga. Naye mtu aliyemwuliza kazi ana hulka ya kutumia kejeli badala ya kuchunguza kiini cha mtoto Rashidi kutafuta kazi anampuuzilia mbali.

Vilevile, mwandishi anayatumia mazungumzo kati ya Rashidi na mama yake, Bi Mashavu anaposema:

> *"Nani?" aliuliza Bi. Mashavu kwa sauti ya mtu aliyekasirika kwa kukatiwa ile raha ya usingizi wa alfajiri. "Miye Rashidi" "unataka nini tena alfajiri hii mtoto weye! Huwachi kunikera roho yangu? Kutwa unanipigisha kelele basi huniwachi alau saa hizi nikapumzika?" (uk. 24).*

Mazungumzo hayo kati ya Rashidi na mama yake yanatoa sifa ya uvivu wa Bi Mashavu ambaye badala ya kuamka mapema na kujishughulisha na kazi tofauti tofauti yeye analala hataki kuamka. Rashidi naye kwa ukakamavu wake anaamka mapema kwenda kuitafuta kazi ili apate riziki yake na ya mamake.

Mwandishi anayatumia mazungumzo kati ya Faraji, George na mfanyakazi aliyekuwa ameuegemea mti huku akisinzia alipokamatwa shati akainuliwa na kupigwa kofi

kubwa sana na George. Naye alipojizoazoa alishtukia amekwisha mvaa George maungoni wanabumburushana. Mwandishi anaposema;

> *"Bloody fool", George alitukana huku akienda zake anapangusa na kuzinyosha nguo zake."Ningelimvunja kichwa chake sasa hivi,"alisema yule* kuli *huku midomo inamtetemeka kwa hamaki. "Powa moto bradha," Faraji alimwambia yule* kuli, *huku akimpigapiga begani, "yule ana mwisho wake yule, tuendeleeni na kazi (uk. 67- 68).*

Mazungumzo haya yanadhihirisha ya kuwa George alikuwa mtu katili asiyekuwa na huruma. Udhalimu wake unajitokeza anapomchapa kuli na kumtukana kazini. Naye Faraji ni mtu mwenye amani ambaye hakutaka vita viendelee lakini alimtuliza yule kuli na wenzake, kazi ikaendelea. Kuli huyo naye ana sifa ya kukasirika mara moja na kumkabili adui kwa vita bila kujali yatakayompata, pia ni mtu mvivu anayelala kazini wakati wenzake wanapoendelea kufanya kazi. Yeye ni kielelezo cha watu wazembe wanaolala wakiwa kazini.

Mwandishi pia anatoa mazungumzo kati ya Rashidi na Salum kuelezea jinsi Rashidi alivyohimizwa na Salum anywe pombe naye akakataa anasema:

> *"Rashidi ee! Pita!"*
>
> *"Wapi?" Rashidi alijibu kwa kustaajabu.*
>
> *"Pita ndani."*
>
> *"Ndani kuja kufanya nini?"*
>
> *"Wewe pita tu!" Salum alisema kwa sauti ya kumlazimisha Rashidi (uk. 117).*

Mazungumzo haya yanaelezea jinsi Salum alivyoipenda pombe na akajaribu kumhimiza Rashidi ashiriki katika ulevi. Rashidi naye hakuwa ameionja pombe na alishangazwa na jinsi watu walivyoingia ndani ya kijumba wakiwa wazima na akili zao na walivyotoka wakiwa wameishiwa na adabu huku wakitukana ovyo.

Mwandishi pia katika riwaya ya *Haini* anaelezea jinsi Hamza na wenzake walivyokuwa wamekaa ukumbini wakisubiri taarifa ya habari kutoka sauti ya Unguja. Mazungumzo yao yamestawi. Walikuwa wakivuta sigareti huku moshi ukielea ndani ya ukumbi mzima. Ukumbi uliopambwa ukapambika. Kassim, Fadhil na Pango, wote wametulia hapana anayesema, wanasubiri taarifa ya habari ya saa kumi na mbili lakini hakuna habari yoyote inayotangazwa kutoka redioni. Mazungumzo yafuatayo yanakatiza hamu ya kusikiliza taarifa ya habari:

> *"Enh! si sherehe za diwali lazima Mabaniani walize fataki na kurusha fashfashi,"Fadhil akaongeza Hizo si fataki wala si fashfashi. Hizo ni risasi, tena risasi zenyewe ni za mishingan", alieleza Pango. Mwanajeshi wa siku nyingi aliyeanzia ukuruta mpaka sasa kafikia cheo cha u-sajini (uk. 1- 2).*

Mwandishi ametumia mbinu ya ukiushi kuashiria jinsi kina Hamza walivyosubiri habari lakini walichosikia ni mlio wa bunduki. Mwandishi amedhihirisha uchimuzi anapomfanya msomaji asikie sauti ya risasi ilhali alikuwa akingojea habari itangazwe. Kwa hivyo, msomaji hutamani kujua kilichosababisha kupigwa kwa risasi na pia yatakayowapata kina Hamza baada ya wao kutoka chumbani.

Mbinu za ukiushi na uchimuzi zinamsaidia msomaji kupata habari halisi kumhusu mhusika Hamza kabla ya mambo mengine kumhusu kutolewa kinaganaga. Kwa mfano, alipofahamishwa kwa msomaji mara ya kwanza mwanzo wa riwaya, alikuwa katika ujana wake na katika kilele cha maisha yake. Amesawiriwa kama mwanamume asiyeona uzito katika maisha, asiyemjali mchumbaye. Hii ndiyo taswira ya hulka yake Hamza anayoiona msomaji mwanzo wa riwaya.

Hata baada ya msomaji kupata maoni yake kumhusu Hamza kuhusu tabia yake ya uasherati ambayo imesisitizwa hapo mwanzoni, mwandishi anapoteza mtiririko wa hadithi anaposisitiza jinsi Hamza alivyomuoa Khadija naye akahamia kwa wazazi wake kabla ya kujifungua kulingana na desturi yao.

Ukiushi pia unaonyesha usanaa kwa kuwa habari haielezwi kwa msomaji moja kwa moja kama katika ngano. Ukiushi huu umetumiwa na mwandishi kama uchimuzi wenye nia ya kimakusudi ya kumpa msomaji fursa ya kugundua sehemu muhimu katika ujumbe. Ile hali na hulka ya Hamza. Matokeo ya hayo ni kuwa msomaji atakapoendelea kuisoma riwaya hii atakuwa na maoni hasi kumhusu Hamza na hatadanganyika atakapobadilika na kuwa mtu mzuri ili kuuficha uovu wa hapo awali.

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi ametumia mbinu hii ya mazungumzo sana. Kwa mfano:

> *“Leo utalala hapa.” “Tena nende wapi na unasikia watu hawaruhusiwi kutoka nje? Lakini nikipata nafasi ya kutoka ntatoka nizipeleke hizi habari” “Utoke wende wapi? Usitoke ukajitafutia balaa” (uk. 6).*

Mwandishi ameyatumia mazungumzo haya baina ya Hamza na mkewe kuonyesha jinsi Khadija alivyompenda mumewe na hangetaka apatwe na balaa mtaani ndipo akamuonya asithubutu kutoka nje.

Askari mmoja waliongea na Hamza alipokuwa akimhoji kabla hawajamchukua kutoka Kisimamajongoo kwa kina Khadija. Mwandishi anasema:

"Wewe nd"o Hamza?"

"Ndiyo!" alijibu kwa haraka, tena sasa kwa sauti ya hofu na wasiwasi.

"Wewe mwandishi wa habari?"

"Ndiyo!""

"Jana ulisikiliza BBC?"

"Sikusikiliza!"

"Hamduni unamjua?"

"Namjua!"

"Yuko wapi?"

"Sikumwona tokea tulipoachana jana mchana.

Aliniambia anakwenda Mwanyanya kuna mavuna!" (uk. 7).

Askari alitaka kujua kama Hamza alimjua Hamduni ambaye alimuua Kiongozi Kigogo. Hamza naye akamjulisha kuwa hakuwa amemuona kutoka siku iliyopita. Mwandishi anayaendeleza mazungumzo yaliyo hapo juu anaposema:

"Twende huku!"

"Wapi?" Hamza aliuliza.

"Wewe twende tu. Mbwa mkubwa unaulizauliza nini?" (uk. 7).

Hamza alitaka kujua alikuwa akipelekwa wapi, lakini askari yule alianza kuonyesha ukatili akamtukana. Hofu ikamjaa Hamza asijue Hamduni amezua balaa gani. Mwandishi anaelezea jinsi mlango wa chumba cha kina Hamza ulivyofunguliwa mara tu baada ya kunywa uji, askari kawasimamia mlangoni kama mwenye kutaka kutoa roho zao, anasema:

"Hamza nd"o nani humu?" aliuliza.

"Mimi!" alijibu kwa haraka, ameingiwa na kiwewe.

"Vaa nguo zako," aliamrisha yule askari. (uk. 36).

Mazungumzo hayo yanaonyesha jinsi yule askari alivyokuwa mkatili na mwenye kutisha, akafananishwa na mtu anayeweza kuwatoa roho zao. Hamza naye alikuwa mtu mtiifu kwani alipoambiwa avae nguo zake alitoka nje ya chumba, lango likakomewa, wakaongozana Hamza mbele askari nyuma, mpaka mlango wa mbele, pale wanapopokelewa wanaokuja kama anavyoelezea mwandishi.

Baada ya kukaa katika chumba cha kiza kwa siku kumi na mbili wakaja kumtoa akiwa amevurugika, hajiwezi. Akarudishwa kwa Ba Mkwe lakini hakumkuta Doto chumbani jambo lililomzidishia Hamza ukiwa na unyonge. Hamza akawa anaweweseka ovyo. Kelele zake zilimshtua Mtani ambaye alikuwa ameshika zamu siku ile akatimua mbio kuona kama mahaini wanatoana roho mle vyumbani. Alipowasha kurunzi yake akaona ni Hamza akifurukuta na kupiga mikambi kama mfa maji mwandishi anasema;

"Wanakuja! Wanakuja!"

"Nani?" Mtani alimwuliza.

“Wanakuja! Hao! Hao! Wanakuja!” (uk. 94).

Hamza alikuwa na homa iliyokuwa imempanda kichwani. Naye Mtani hakujali aliufunga mlango na kumwacha apone au afe bora amalize zamu yake aondoke. Mtani ni mhusika asiye na huruma na utu.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi ameitumia mbinu hii ya ubunifu ya mazungumzo ili kumsaidia msomaji kuwatambua wahusika wanaoshiriki katika maongezi kutokana na uteuzi wao wa maneno, matamshi na hata lugha wanayotumia. Wazungumzaji wawili huwakilisha mitazamo, mawazo na sifa tofauti. Pia, kudhihirisha tabaka, elimu, umri na mielekeo ya mhusika. Mwandishi ameyatumia mazungumzo ili kuleta hali ya uhalisia na uhai wa wahusika wanapotoa mawazo yao. Mazungumzo humsaidia mwandishi kusukuma matukio upande anaokusudia.

3.2 Mlazo kama Mbinu ya Ukiushi

Ahmed, (2015), anasema ukiushi ni mbinu ya kisanaa katika kazi na fasihi ambapo tendo au suala linafanyika kinyume cha matarajio au sifa za kimatumizi ya lugha zilizo katika jamii fulani. Kuna aina nyingi za ukiushi kama vile kimsamiati, kisarufi, kimaandishi, kifonolojia, kisemantiki, kisajili, kilahaja na hata wa kihistoria.

Katika riwaya zote mbili *Kuli* na *Haini* mwandishi anatumia herufi lakini anapotaka kusisitiza sifa fulani katika ujumbe wake anatumia herufi za mlazo. Kwa hivyo, hubadilisha kile kinachotarajiwa katika akili ya msomaji kama taswira. Matokeo hayo hujitokeza pale sehemu iliyoandikwa kwa mlazo inapojitokeza zaidi kuliko iliyoandikwa kwa herufi za kawaida.

Vifungu hivyo vya mlazo huashiria mhusika binafsi. Wahusika huwa na mazungumzo binafsi, wanapojibizana kuhusu maswala fulani. Kupitia mbinu hii mwandishi huweza kujiondoa kutoka kwa masimulizi na kumwezesha msomaji kuwafahamu wahusika vizuri moja kwa moja akaweza kuzifahamu hata shida zinazowapata kisaikolojia. Vifungu hivyo kwa kweli huwa vinahusu hisia za hali ya juu ya wahusika.

Wimbo ni bahari mojawapo ya Ushairi. Wimbo huwa na mizani kumi na miwili kila ubeti, una mishororo au mistari mitatu kila ubeti. Sifa za wimbo ni kufanana na shairi la tathlitha lakini shairi hili huwa na mizani mingi kuliko kumi na miwili.

Tumeviangalia vifungu kutoka riwaya zote mbili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kuli* mwandishi ametumia wimbo alioimba Rashidi alipokuwa mlevi anayumba kama kishada. Matumizi ya wimbo katika uandishi unadhihirisha ubunifu wa mwandishi katika uandishi anapoelezea dhamira ya kimapenzi. Wimbo huu unadhihirisha mawazo yake kumhusu mpenzi wake Amina. Kwa hivyo, unaonyesha mazungumzo yake ya binafsi, pia hisia zake za mapenzi kwa Amina anapoimba:

“Mapenzi yamenisibu,
ghafula usingizini,
nimependa kitu ghali
hakiuzwi madukani
ningelipoteza mali
hakitia mkononi” (uk. 121).

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi Shafi Adam Shafi ametumia herufi za mlazo kuuandika wimbo wa Hamza alioupenda sana, akauimba akiwa miguu ameipachika

juu, akipiga miluzi kwa sauti ndogo. Mwandishi ametumia herufi za mlazo ili kubadilisha mtiririko wake wa kuandika, kusisitiza anachoelezea na kudhihirisha hisia za mhusika. Wimbo huu unadhihirisha hali ya furaha na matumaini. Alijenga upya matumaini pale ambapo kila mtu alikuwa amekata tamaa anapoimba:

"Msegeju ana ng"ombe
nami nna ngombe zangu
namwambia tuchanganye hataki
kwaheri nakwenda zangu" (uk. 58).

Naye Khadija anapowaza juu ya mumewe, anatamani kama mtoto wake angekuwa akimlilia baba yake kisha akambembeleza anapomwimbia lakini anaendelea kulia. Ufuatao ni wimbo unaodhihirisha hisia na mawazo yake Khadija;

"Nilipochukua mimba
Taabu na mashaka yangu.
Usiku kucha silali.
Nawania roho yangu.
Nambiwa mwana si wangu.
Mwana ni wa mume wangu" (uk. 144).

Wimbo huu utamfahamisha msomaji shida alizonazo Khadija. Kilio cha mwanawe kinamkumbusha Hamza mumewe na shida zinazomkabili. Mawazo tele juu ya mwanawe na jinsi atakavyokua bila baba yake yanamtatiza sana asijue la kufanya ndipo akauimba wimbo huu. Katika mhimili wa tano wa nadharia ya Kimtindo hisia za mwandishi zinaonekana, zinaweza kudhihirisha dhihaka, mapenzi, ukali au kejeli.

Mhusika Khadija anadhihirisha hisia za mapenzi. Katika *Kuli* wimbo wa Rashidi kwa Amina unaonyesha mapenzi yake kwake. Katika *Haini* Hamza naye anaimba anapomkumbuka Khadija. Mtoto anapolia anamfanya Khadija aimbe wimbo kudhihirisha jinsi maisha yake yalivyokuwa na dhihaka, ukali na kejeli. Kwa hivyo, nadharia hii inafaa kuchambua kazi hii. Maoni yetu ni kuwa matumizi ya mlazo humsaidia mwandishi kudhihirisha hisia za mhusika wake.

Kifungu kifuatacho kinaonyesha mazungumzo binafsi ya Hamza.

> *"Na hata hao waliobaki nao pia watatoka tu," alisema Hamza. Yupo peke yake. Aligeuka nyuma na kuangalia lile lango la gereza. Alilitazama kwa chuki na hasira, uchungu ukamjaa moyoni akawaza jinsi lango lile lilivyoficha nyuma yake mateso na madhila" (uk. 267).*

Wakati alipoyasema maneno haya ubongo wake ulikumbuka, ukakumbuka maisha yake huko gerezani na shida alizopitia. Hasa ule uhusiano wake na Abdul, aliyekuwa mwenza gerezani akayakumbuka na maneno yake, "Tutatoka tu! Kweli ametoka. Akaondoka taratibu pale alipokuwa amesimama kuelekea nyumbani kwa Khadija mpenzi wake na Subira mtoto wake, safari hii peke yake, hawakuhitajika tena askari wa kumsindikiza huku wamemwelekezea mitutu ya bunduki. Hayo yamekwisha.

Katika hali ya kukumbuka maisha ya jela, Hamza anakumbuka yale masumbuko makali na maumivu makubwa aliyopitia huko gerezani. Sharti ikumbukwe kuwa Hamza alipoyanena maneno hayo hakuwa na kazi wala usaidizi wowote, maisha

kwake yalikuwa hayana maana ila madhila. Mkewe na mtoto wake walikuwa wamesumbuka kwa shida. Kwa hivyo, maisha yalikuwa ni mateso tu.

Kifungu kifuatacho pia ni mfano wa ukiushi wa nje, unaoleta tofauti kubwa kati ya dunia ya matajiri na wachochole katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anasema:

> *Asante! Asante Bwana, Rashidi alisema huku akijipinda mbele ikiwa ni kama ishara ya kuonyesha heshima. Ijapokuwa Rashidi alifurahi kwa kupata shilingi bila ya hata kuitumainia, pale pale ilimjia fikira na kuhisi kwamba jambo alilolifanya lilikuwa si zuri; palepale aliwaza yale anayokatazwa na mama yake ya kutoomba pesa na akakumbuka jinsi, safari moja alipokuwa mdogo alivyopigwa kwa kumwomba mtu senti tano tu (uk. 29).*

Kifungu hiki kinaangazia mfano wa maisha ya huzuni na kusikitisha ya watu wa tabaka la chini katika jamii ya mwandishi. Katika *Kuli* Rashidi ni mfano wa watu wasiobahatika na pia fukara ambao watu wa jamii wameamua hawatayazingatia masuala yao. Ujumbe huu unadhihrisha mambo mawili yenye kejeli. Kwanza, Rashidi hata ingawa anaonekana katika hali ya umaskini na anatarajiwa kuwa hohehahe amesawiriwa kinyume. Anaonekana akiwa na furaha akiyakubali yaliyompata kwa furaha. Pili, hata hivyo ingawa kuna watu wengi walio fukara kuna wachache walio matajiri, wanaosawiriwa kuwa wakarimu na wakristo. Mwandishi anatumia dhihaka na kejeli kudhihirisha jinsi matajiri wanavyowadharau maskini katika jamii yake.

Mhimili wa tano wa nadharia ya Kimtindo unaweka wazi matumizi ya dhihaka na kejeli ili kudhihirisha hisia za mwandishi jambo linalotokea katika kazi ya mtunzi.

Tunaonelea kuwa kicheko cha furaha cha Rashidi ni kejeli, sababu maalumu ikiwa ni kudhihaki maovu katika jamii yake. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanajamii wanaoonekana wakarimu au wakristo sio ukweli na lengo lao ni kupata sifa nzuri na hata kuyajali maslahi yao wenyewe. Hili ni dhihirisho kuwa wanyonge katika jamii hawatiliwi maanani na matajiri. Haya ni maovu ya ukabaila anayojaribu kufichua mwandishi katika riwaya ya *Kuli.*

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anaelezea jinsi Kondo akiwa amelala chali, ametundika mguu juu hana habari ya wanaopiga ramli wala ya wale wanaojitayarisha kwa safari ya mahakamani mwandishi anasema:

> *Hali yake ya uchangamfu imerudi vile vile. Yuko mbali anaimba wimbo wa Mbaraka Mwinshehe. Alizihifadhi vizuri nyimbo hizo, maneno, milio ya matarumbeta, milio ya magitaa na mivumo ya masaksafoni. Vyote hivyo huviigiza kwa milunzi mpaka ukadhani labda kikosi kizima cha "Super vokano" kinatumbuiza ndani ya chumba hicho. Wale walioshtushwa na habari za kupelekwa mahakamani walimwona Kondo kama anayewafanyia tashtiti kwa kuusahau ule mtihani uliowakabili (uk. 108-109).*

Mwandishi amemtumia mhusika Kondo kudhihirisha ukiushi kwani furaha haiwezi kuwepo pamoja na hofu. Uchangamfu unaomjia Kondo akaanza kuimba wakati wengine wanahofia yatakayowapata mle mahakamani utajitokeza kama uchimuzi kwa

msomaji kwani ataliona jambo hilo kama kejeli. Kondo mwenyewe ni mhusika wa tatizo hilo. Labda anajaribu kuyasahau kupitia kuimba.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi alitaka kuonyesha jinsi matatizo katika jamii yake yanavyotupiliwa mbali na wale wanaostahili kuwatatulia. Watu wa tabaka la chini hawana wa kuwatetea kwani hata wale wanaochaguliwa kama wawakilishi wao hujinyakulia mali wakawasahau waliowachagua. Kwa hivyo, tofauti kati ya maskini na matajiri itaendelea kuwa kubwa. Hili ni kwa sababu walio na mali wanaendelea kutajirika nao wenzao wanaendelea kuteseka. Tunapendekeza kuwa maslahi ya wananchi yatiliwe maanani ili tofauti ya kitabaka itupiliwe mbali.

3.3 Ukiushi na Uchimuzi wa Maneno

Wamitila (2003) anaelezea kwamba ukiushi ni sifa za kimtindo ambazo si za kawaida zinazoenda kinyume na sifa za kimatumizi ya lugha zinazopatikana katika jamii. Nao uchimuzi ni mbinu ya kuyadokeza mambo fulani au sifa fulani katika kazi ya kifasihi kwa namna ya waziwazi na kuyafanya yajitokeze waziwazi yakilinganishwa na mengine. Hii ni mbinu inayotumiwa kusisitizia mambo fulani yanayoonekana kuwa muhimu au yenye uzito katika kazi fulani ya kifasihi.

Msamiati aliotumia mwandishi ni baadhi ya maneno yanayotumika katika mazingira yake alimozaliwa kule Unguja. Yeye mwenyewe ni Mswahili anayeifahamu lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, maneno aliyotumia katika uandishi wake yanafahamika na wakazi wa maeneo hayo. Maneno ya Kiarabu yanaweza kuwepo kutokana na Waarabu kuishi huko Unguja. Kuna uwezekano wakazi wa Unguja huyatumia

maneno hayo. Vilevile, tutazingatia maneno ya Kingereza, maneno ya Kihindi, misemo na methali alizotumia mtunzi katika riwaya za *Kuli* na *Haini*.

Mwandishi ametumia maneno ya lugha ya kigeni ili kudhihirisha umahiri wake wa kuimudu lugha hii na hivyo kuitumia kama ukiushi wa kimsamiati. Pia, maneno haya yameandikwa kwa herufi za mlazo ili kubadilisha mtiririko wake na kusisitiza anachoelezea. Maneno haya yanaweza kuwekwa katika vikundi vitatu. Kwanza, yale yasiyo na maneno yanayofanana ya Kiswahili. Kwa mfano, katika *Kuli* kuna maneno kama vile:

Bloody fool (uk. 6, 150).

Crème (uk. 23).

Katika *Haini* kuna maneno kama vile:

The big nine (uk. 155).

Full- suit (uk. 22, 157).

Pili, kuna maneno yaliyo na visawe katika Kiswahili lakini mwandishi akaamua kuyatumia kwa lugha ya Kigeni na lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika *Kuli* kuna maneno kama vile:

kofia- hat (uk. 41).

Katika *Haini* kuna maneno yafuatayo;

akaomba radhi - excuse me! (uk. 241).

Tatu, yale maneno ya Kingereza yaliyo na maneno ya Kiswahili yanayolingana, lakini mwandishi aliamua kuyatumia maneno ya Kingereza. Tumeyaangalia maneno yafuatayo katika riwaya ya *Kuli:*

Jail badala ya jela, gereza (uk. 92).

"Listen you fools!" badala ya "sikilizeni nyinyi wajinga!" (uk. 92).

Katika riwaya ya *Haini* ametumia maneno kama vile:

Repeater badala ya anayerudia darasa (uk. 220).

Physics badala ya fizikia (uk. 200).

Chemistry badala ya kemia (uk. 200).

Mwandishi Shafi Adam Shafi ameyatumia maneno haya ya Kingereza badala ya maneno ya Kiswahili kama ukiushi na kwa kusudi la kutaka msomaji aone athari ya maneno hayo kama uchimuzi katika riwaya ili aweze kudadisi na kutaka kujua anachokusudia mwandishi. Tunaonelea kuwa mbinu ya mlazo hupitisha hisia za mhusika kwa msomaji naye hushiriki katika hali ya furaha au huzuni.

3.4 Dhana ya Lafudhi

Lafudhi ni matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo au lugha zinazomzunguka. Pia, ni udhihirishaji wa sauti za lugha unaomtabulisha mtu mmoja na jamii ya watu kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu, (2004).

Hapa tumechanganua maneno katika riwaya ya *Kuli* yaliyotamkwa kwa lafudhi ya Kihindi huko bandarini wasimamizi walipokuwa wakiongea na wafanyakazi. Kwa mfano,

“Chukua hii toto peleka kwenye gengi yako!” (uk.56).

Mwandishi katika riwaya ya *Haini* ametumia lafudhi ya Kimakonde. Mwandishi amemtumia mhusika Fimbo katika matumizi ya lafudhi ya Kimakonde kwa mfano, Shadidi anapokuwa akiwaandalia “pudding” *w*afungwa wenzake alimtazama Fimbo kisha kwa dharau aliguna” Ah! Wewe Mmakonde unajuaje kula pudding?” Ndipo Fimbo akasema;

“Chacha pudi chichi unanjalau?" “Chichi kwetu Nchumbiji tunakula pudi na jaidi ya Pudi,” alijigamba” (uk. 26).

“Ndiyo njinga! Tena ukileta kelele jako nitakunyonga apa apa!” (uk. 27).

Katika riwaya ya *Kuli* mwandishi ametumia lahaja ya Kishihiri anapomtumia Mzee wa Kishihiri kama mhusika anayefanya kazi ya kuuza makaa. Anatumia lafudhi ya Kishihiri anapoongea Kiswahili mwandishi anasema;

“Ya shekh, nini nataka haba, habana bahala ya mshezo” (uk. 13).

“Weye nataka kazi? Naweza kubeba kigabu ya makaa weye?” (uk. 14).

“ Wee Kalb wee! Weye nashkua kibati mara mbili kwa kikabu moya,” (uk. 15).

Hii ni sanaa ya kunakili kwa ulinganifu lafudhi ya mtu mwingine ili kuridhisha zaidi nyoyo za wasomaji wa jambo ambalo hawakushuhudia. Maoni yetu ni kuwa mbinu hii ya lafudhi ameitumia mwandishi ili kumnata msomaji aweze kuendelea kusoma. Jambo linalodhihirishwa na mhimili wa nane katika nadharia ya Kimtindo.

3.5 Dhana ya Misemo na Nahau

Doris, Ken na Norah, (2016), wanaelezea kuwa misemo ni fungu ya maneno yenye maana fiche pia huitwa nahau. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu, (2004), nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ambayo huonekana waziwazi. Huwa na kitenzi na jina.

3.5.1 Misemo na Nahau katika Riwaya ya Kuli

Mtunzi ametumia nahau ifuatayo katika riwaya ya Kuli “walikata tamaa” (uk. 1). Nahau hii imetumiwa kuonyesha wahusika Majaliwa na Bi Mashavu wamepoteza matumaini ya kumpata mtoto na hakuna mzimu waliobakisha tokea Unguja hadi Pemba. Mtunzi ametumia nahau nyingine “yangeenda mrama” (uk. 2). Nahau imetumiwa kuelezea mhusika Majaliwa sharti angeenda kazini. Maudhui yanayojitokeza ni ya umaskini.

Mhusika Rashidi aliuliza swali huku “kapigwa na mshangao” (uk. 12). Nahua imetumiwa kuelezea alivyoshtuka. Maudhui yanayodhihirika ni ya umaskini. Nahau nyingine ni “alishika njia” (uk. 19). Nahau hii inamaanisha kuwa Mzee Shauri alienda zake.

Kulingana na mhusika Rashidi watu hawakupoteza muda mle ndani “walitoka chordo” (uk. 119). Rashidi anautumia nahau hii kumaanisha walitoka wakiwa wamelewa chopi huku wakigombana wenyewe au na muuzaji. Maudhui yanayodhihirika ni ya umaskini.

Mhusika Farjalla ametumia msemo huu “atamtilia mtu kitumbua chake mchanga” (uk. 45). Anaashiria “kitumbua kimeingia mchanga”. Msemo huu ulitumiwa na

Farjalla alipokuwa akimwelezea Rashidi jinsi wanavyoweza kufutwa kazi. Maudhui yanayodhihirika ni ya unyanyasaji na dhuluma kwa wafanyikazi. Kuna nahau nyingine “wanapika jungu” katika (uk. 76). Unaashiria kuwa Rashidi hakufahamu ni jambo lipi lililokuwa likiendelea pale gatini. Maudhui ya kimapinduzi na ukombozi yanayojitokeza.

Mtunzi ametumia nahau “alishika hamsini” (uk. 77). Anaelezea jinsi Rashidi alivyomwacha Faki pale Miti Ulaya, walipokuwa wamesimama naye akaenda zake, akaendelea na shughuli zake. Kauli “tuchukue hatua” imetumiwa na mhusika Bakari katika (uk. 85). Inaashiria kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kipigania haki zao kutoka kwa mabepari. Maudhui ya dhuluma na ukatili kazini yanadhihirika.

Nahau inayokuza maudhui ya kimapinduzi ni “akipiga upatu” (uk. 88). Alfajiri na mapema mfanyakazi mmoja alijitolea kupitia mitaani akiwaeleza watu wasiende gatini kwani mgomo ulikuwa umeanza. Maana yake ni kuwa alichukua chombo cha madini ya chuma na kukipiga.

Nahau inayoelezea jinsi Rashidi alivyofanya kazi ni “alichapa kazi” (uk. 113). Ina maana ya kuwa Rashidi alifanya kazi mpaka saa kumi na mbili jioni. Nahau ina maudhui ya kazi pia waajiri waliokuwa wamemwajiri hawakumthamini yeye na wenzake kwani walifanya kazi saa nyingi na mshahara ukawa duni.

Msemo mwingine ambao umetumika ni “potelea mbali na liwe litakalokuwa” (uk. 175). Pia ametumia msemo “kuvunja jungu” (uk. 142). Vilevile, mtunzi ametumia nahau “amepigwa na bumbuazi” (uk. 159).

3.5.2 Misemo na Nahau katika Riwaya ya Haini

Mtunzi ametumia nahau hii “akifumba macho” (uk. 1). Anaonyesha jinsi Khadija alistahimili yote aliyopitia mwishowe akaolewa na mchumba wake Hamza. Nahau inakuza maudhui ya matumaini na uvumilivu.

Mwandishi ametumia nahau hii “likapigwa moto” (uk. 8). Inaelezea gari liliguruma likang‟oa nanga. Maudhui ya ukatili yanakuzwa kwani hawakuwa na uhakika yeye ndiye aliyekuwa muuaji.

Msemo huu ameutumia mtunzi “miaka nenda miaka rudi” (uk. 34). Mtunzi anaelezea jinsi kuta lile liliwatenganisha walio ndani mahabusu na walio nje, raia huru. Kuta lilikuwa hapo kwa miaka mingi. Pia, msemo unaashiria jinsi watu wengi walivyodhulumiwa na kuteswa kwa muda mrefu kwa makosa yasiyo yao.

Mtunzi ametumia nahau hii “kuukabili mtutu” (uk. 36). Nahau inaashiria kuwa Hamza alikuwa mbele ya askari Jeshi kama aliyehukumiwa kifo na aliyestahili kupigwa risasi. Maudhui ya ukatili yanadhihirishwa kwani askari lazima angojee kesi iamuliwe na hakimu iwapo mshukiwa atauawa kulingana na kosa alilotenda.

Aidha, mtunzi ametumia nahau hii “asalim amri” (uk. 66). Anaelezea jinsi Hamza alivyoteswa hadi akakubali kushirikiana na Hamduni kumuua kiongozi Kigogo. Maudhui ya ukatili yanaonekana kwani binadamu hawezi kutumbukizwa kisimani akiwa hai, huo ni unyama wa hali ya juu.

Mtunzi ametumia nahau “kukata tamaa” (uk. 130). Anaelezea jinsi wafungwa walivyokuwa na hofu na wasiwasi wamepoteza matumaini wasijue litakalowapata

huko kwa Ba Mkwe kwani zahma za kupiga na kupopoa, kutesa na kuua zilikuwa zimeisha.

Mwandishi ametumia kauli hii “kula mwata” (uk. 134). Anaashiria jinsi mke wa Khalfani alivyotaabika akapata taabu sana, naye hakuweza kustahimili akaidai talaka kwa Shekhe, akaolewa tena.

Mhusika Mfaume ametumia nahau hii “naweka nadhiri” (uk. 220). Nahau hii inakuza maudhui ya matumaini kuwa mhusika na wenzake sharti wangeachiliwa huru. Mwandishi ametumia msemo mwingine “hajijui wala hajitambui” (uk. 41). Maana ya msemo huu ni kuwa katika hali muhututi. Umetumiwa na mtunzi kuonyesha jinsi Hamza alivyokuwa kama mtu anayetaka kukata roho. Maudhui yanayojitokeza ni ya ukatili, udhalimu na uhayawani kwani vitendo hivyo havina utu wowote.

Mtunzi ametumia nahau “vimetumbukia nyongo” (uk. 202). Anaelezea jinsi watu wote tisa walivyokwama, kama samaki walioingia demani hawaioni njia ya kutokea. Maudhui ya tamaa yanadhihirika wazi, kwani ni vipi mtu akubali jambo ambalo hajalifanya ili ale vinono?

Mhusika Bi Farashuu anamuonya binti Khadija asikope akaadhirike bure! Anatumia nahau “Kututia mdomoni” (uk. 147). Anaashiria hofu aliyokuwa nayo na katu hakutaka majirani wagundue dhiki iliyowakabili. Maudhui yanayojitokeza ni yale ya umaskini.

Mhusika Haramia alitumia kauli “tusimame kidete” (uk. 16). Anawahimiza wenzake wasikubali chochote wasichokijua kwani askari hawakuwa na ushahidi wowote. Maudhui yanayodhihirika ni ya kutumia ukweli badala ya uongo.

Nahau ingine ni “wamemkondolea macho” (uk. 166). Nahau imetumiwa na mhusika Dude anapomwita Haramia aliyetakikana na Kanali Bunju ampeleke Mashakani Hotel. Wahusika Vingosho, Zarikani walioshtuka Dude alipomwita Haramia.

Mhusika Kanali Bunju alipoongea kule ofisini Haramia moyo “ukamwenda mbio” (uk. 175). Nahau inamaanisha alishtuka moyo ukapiga kwa kasi. Maudhui yanayotokea ni ya ukatili. Haramia aliogopa alipokumbuka alivyong‟ang‟ana na chatu huko Mashakani Hotel.

Mke wa Kapteni Baraka aliitumia kauli “kukaa enda” (uk. 184). Mhusika alimkanya mumewe kushirikiana na Khadija alipotaka kujua habari za mumewe Hamza. Nahau ingine ambayo imetumika ni “kupiga simile” (uk. 210). Vilevile, nahau hii “kufanyia ndaro” (uk. 225). Pia nahau, “aliyetia fora” (uk. 251).

Maoni yetu ni kuwa mwandishi ameitumia misemo kama mbinu ya uhamishaji wa maana maadamu inamsaidia kuitumia lugha kwa undani zaidi. Imemsaidia kuyaelezea maudhui na dhamira yake kwa msomaji anayefikiria zaidi juu ya kile anachoelezea mwandishi hivyo kutafakari juu ya matukio anayosoma. Nadharia ya kimtindo katika mhimili wa nane inapendekeza matumizi ya msamiati wa kuleta mvuto na kumtia ari msomaji kama alivyofanya mwandishi alipotumia misemo. Kwa hivyo, nadharia hii inafaa katika uchanganuzi huu.

3.6 Dhana ya Methali

Kutokana na maoni ya Maitaria (2012), methali zimeibuliwa ili kutumika kuwashilisha maadili katika jamii. Pia, zimesheheni busara na elimu kuhusu maisha na falsafa ya jamii pamoja na kuufumba ujumbe ambao huwasilishwa kupitia kwa tamadhali za semi. Hutumika kuelimisha na kuburudisha jamii, kuiadilisha na kuielekeza, kuikanya na kuikemea, kuishauri na kuinasihi, kuikosoa na kuihimiza. Kwa jumla, methali ni semi fupi zinazotumia lugha ya mafumbo ili kuonya, kukosoa, kusisitiza na kuelekeza. Ukweli wake hutegemea jamii na mazingira maalum. Methali hutumiwa kupamba lugha kwa kuipa kazi ya fasihi usanii.

3.6.1 Methali katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi Shafi Adam Shafi amezitumia methali ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika riwaya ili kuendeleza maudhui na kujengea taswira. Zifuatazo ni baadhi ya methali katika riwaya ya *Kuli***.**

Mhusika Rashidi ametumia methali “hauchi unakucha” (uk. 33). Ameitumia kujiliwaza na kwa hivyo akawa na matumaini ya kuishi. Kauli ambayo imetumiwa na Mzee Tindo ni “kikulacho ki nguoni mwako” (uk. 49). Yeye anaelezea kuwa anayekutendea mabaya ni yule mja mnayejuana. Alinuia kuwa Rashidi aliyemtafutia kazi ameungana na wafanyakazi wenzake kudai nyongeza ya mshahara. Maudhui ya unyanyasaji na matabaka yanadhihirisha kwani makuli hawakuwa na haki ya kutetea haki zao.

Mtunzi vilevile ametumia methali “ibilisi wa mtu ni mtu” (uk. 123). Methali hii imetumiwa na Rashidi akiwa chumbani mwake akikumbuka namna Salum

alivyomzaini mpaka akakubali kulewa. Methali inatahadharisha kuwa tusikubali kuyafanya yanayoyaharibu maisha yetu hata tukishawishiwa na marafiki.

Mhusika Faraji metumia methali “maji tushayavulia nguo na sasa hatuna budi kuyakoga” (uk. 169). Methali yenyewe ni “ukiyavulia nguo utayaoga” kumaanisha kuwa mtu anapojitolea kutenda jambo lolote hana budi awe tayari kulikamilisha. Maudhui yanayodhihirika ni ya kazi.

Vilevile, kidokezo cha methali “yana mwisho haya” (uk. 198). Imetumiwa na mhusika Rashidi. Kwa kawaida methali hii huwa “hakuna refu lisilo na ncha” Mhusika anaendeleza maudhui ya mapambano na ukombozi. Kwa hivyo, Rashidi anaitumia kuwaandaa wenzake kuwa tayari kupigania haki na wakishafaulu basi shida zao zitafika mwisho.

3.6.2 Methali katika Riwaya ya Haini

Zifuatazo ni baadhi ya methali alizotumia mtunzi katika riwaya ya *Haini*. “Paka akiondoka panya hutawala” methali hii imetumiwa na mhusika Mzee Machale anaposema “paka wameshaondoka sasa zamu yake yeye panya kutawala” (uk. 69). Anaitumia akiufurahia ufalme wake wa kutawala mahabusu akihisi yeye ni mkubwa. Methali hii inakuza maudhui ya kazi kwani inawahimiza wafanyikazi wawe na bidii bila ya kuwategemea wasimazi wao.

Vilevile, methali iliyotumiwa na mhusika Hamza ni “nguo ya kuazima haisetiri matako” (uk. 85). Anaitumia huko Kumbakumba alipoamrishwa avue nguo alizokuwa amevaa. Ilikuwa lazima kulazimishwa kuvua nguo na kudhalilishwa ule utu pia

kuzushwa hadhi ya ubinadamu kila ulipofikishwa kule. Maudhui ya udhalimu na unyama yanajitokeza kupita methali hii.

Aidha, mhusika Sururu anaitumia methali “bandu bandu huisha gogo” (uk. 113). Inaendeleza maudhui ya matumaini licha ya matatizo waliopitia. Sururu anaitumia anapowaza jinsi angelitoboa shimo kubwa chini ya ukuta ili waweze kutoroka jela. Methali hii inadhihirisha umuhimu wa ushirikiano katika jamii.

Aidha, mhusika Haramia anadokeza methali “kwa shujaa huenda kilio, kwa woga huenda kicheko” (uk. 173). Hamza aliufikiri usemi huu alipomwona chatu ashajiwa na unyama wake, akajua akijiregeza atamla mzima mzima na hakuwa na budi kujihami kwa namna yoyote ili kuyanusuru maisha yake. Woga ukamtoka ukamjia moyo wa kishujaa akapambana na chatu yule. Haramia alipobanwa kwenye mbavu na chatu yule akashindwa kupumua akakidhibiti kichwa cha chatu akaikeketa shingo kwa meno, akanyofoa minofu na kuitema. Akamwachilia chatu alipohakikisha amekikata kichwa chake na kutoka katika kiwiliwili chake, amekufa. Maudhui yanayojitokeza ni ya ukatili kwani ni unyama binadamu kurushiwa chatu amle.

Mhusika Azizi ametumia methali “mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo” (uk. 183). Alimaanisha kuwa Khadija angekubali wakutane chini ya mti wa Mabaniani. Maudhui yanayojitokeza ni ya uchu wa kimapenzi.

Kauli aliyotumia mhusika Khadija ni “subira yavuta kheri” (uk. 186). Methali hii inakuza maudhui ya matumaini kwa kumpa mhusika faraja akasubiri kwani hakuna kisichokuwa na mwisho. Pia, methali yenyewe ni “ subira huvuta heri huleta kilicho mbali. ”

Maudhui ya ukosefu wa haki yamewasilishwa kupitia methali “mwenye nguvu mpishe” (uk. 150). Inakuza maudhui ya umaskini kwani Khadija na wananchi wenzake walikuwa wakisukumana katika foleni ili wakapate mikate ya boflo. Pia, inadhihirisha tofauti kuu kati ya maskini na matajiri. Vilevile, matabaka yanayojitokeza ni mawili.

Mtunzi ametumia methali hii “leo ndio leo, asemaye kesho ni mwongo” (uk. 119). Methali hii inatumiwa na Sururu alipokuwa akijitayarisha kuuparamia ukuta ili autimize mpango wake wa “Kata Mbunga” uliokuwa umeshaiva. Mshipa wa ukaidi umesimama haambiliki, hashauriki, hashawishiki. Methali hii inaendeleza maudhui ya ujasiri wa kupigania haki kutoka kwa wadhalimu.

Maudhui ya kukata tamaa yamedhihirishwa kupitia kwa methali “mbio za sakafuni huishia ukingoni” (uk. 126). Methali hii inatumiwa na Sururu anapozinduka na kujikuta amezungukwa na askari kila mmoja akiwa na bunduki mkononi. Wakamburura na kumwambia kuwa atakiona kilichomtoa kanga manyoya.

Kauli hii “mnashukuru kweli au shukrani yenyewe ni ile ya punda?” (uk. 166). Kidokezo hiki ni cha methali “asante ya punda ni mateke.” Maudhui ya ukatili na dhuluma kwa wafungwa yanajitokeza. Kanali Bunju anamwambia Haramia alipopanga vile atampeleka Mashakani Hotel akabiliane na Chatu.

Methali nyingine ambazo zimetumika ni kama vile, “mtego wa panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo” (uk. 158). Vilevile, “dua la kuku halimpati mwewe” (uk. 14).

Mwandishi katika riwaya zote mbili amezitumia methali ambazo zimemsaidia kuelezea maudhui na dhamira yake. Mbinu hii ya uhamishaji wa maana imemsaidia msomaji kutafakari zaidi alilokusudia mwandishi. Pia, zinawaonya, kuelimisha, kutahadharisha na kuwaelimisha wasomaji wakawa na hekima na busara ya kuweza kuishi na wenzao ipasavyo kwa kushirikiana vilivyo katika kila jambo.

Tunaonelea kuwa mwandishi aliyateua maneno aliyotumia kwa njia ya kipekee hasa anapozichagua methali zilizofaa katika uandishi wake. Jambo linalopendekezwa na mhimili wa nane wa nadharia ya kimtindo unaoelezea kuhusu uteuzi wa msamiati unaoleta mvuto kwa msomaji kwa kumtia ari ya kusoma. Hivyo basi, kudhihirisha ufaafu wake katika kuzichanganua kazi za mwandishi.

3.7 Uradidi wa Maneno

Matinde, (2012), anasema ni utaratibu unaotumika kuunda maneno ambayo sehemu ya neno lote hurudiwa na kuunda neno au msisitizo fulani. Takriri ni urudiaji wa maneno, silabi, au sauti zinazolingana katika fasihi kwa njia tatu. Kuna takriri ya fonimu zenye mlio unaoweza kuendelezwa ambazo aghalabu ni irabu na takriri ya maneno.

Uradidi ni hali ya mwandishi kurudia vipengele fulani katika matini ili yalete uchimuzi. Baadhi ya vipengele hivi vinajitokeza kama uradidi wa maneno. Vinaweza pia kuwa maneno ya visawe.

3.7.1 Uradidi katika Riwaya ya Kuli

Tutaanza kwa kuchanganua uradidi wa maneno katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anasema:

> *Kazi? Kazi gani? Hizi kazi zilizopo hapa zinakushinda! Leo maji hujateka mitungi yote mikavu na unajua vizuri kwamba siku hizi serikali inafunga maji kutwa (uk. 21).*

Katika aya hii neno linalorudiwa ni "*Kazi."* Neno hili limerudiwa mara tatu. Kwa hivyo, linajitokeza kama uchimuzi kwani msomaji atalizingatia zaidi akitaka kujua mwandishi alinuia nini alipolitumia. Sentensi ya kwanza ni swali la balagha ambalo halihitaji jibu, "*Kazi? Kazi gani?"* Hili swali lina dhima la uchimuzi na pia sentensi hiyo ina hisia kali. Yafaa kusisitiza kuwa kwa kweli *Kuli* ni riwaya yenye hisia, kwa kawaida hadithi hii inaleta hisia zenye nguvu za kumwathiri msomaji. Mwandishi katika juhudi za kuzitoa hizi hisia amewasiliana kwa kutumia lugha kwa njia ambayo hisia hazitaihepa makini ya msomaji. Hisia na misemo ya kukata tamaa, ufidhuli, masikitiko, kukosa matumaini na umaskini, haya yote yameonekana kupitia usambamba, uradidi na msisitizo wa sifa fulani.

Pia, mwandishi ametumia uradidi wa visawe katika riwaya ya *Kuli* kwa mfano;

> *Ijapokuwa alikuwa mhindi, tabia ya Ramju ilikuwa kama ya mfanyakazi yeyote yule wa bandarini. Kwa masihara, matusi na kusutana na ma*kuli *wengine kwa mzaha (uk. 56).*

Mwandishi anaelezea kuwa Ramju alitangamana na wafanyakazi huko bandarini akawa mmoja wao hasa kwa jinsi alivyotumia lugha walivyofanya makuli. Mwandishi ametumia takriri kwa ustadi anapoteua maneno yanayotoa maana inayofanana kuelezea lugha aliyotumia Ramju.

Mwandishi huamua kwa makusudi kurudiarudia maneno au vipengele kwa lengo maalum la kusisitiza jambo ama kulitia mkazo jambo linaloelezwa. Mtindo huu wa msisitizo una lengo la kufanya jambo limwingie msomaji vyema. Aidha, takriri inatumiwa kupambanua dhamira zilizoko katika hadithi. Wakati huo huo pia takriri inapamba hadithi kisanaa na kusaidia kuweka kumbukumbu ya baadhi ya mambo muhimu. Takriri pia hutumika kwa nia ya kutaka kukazia jambo fulani, ikiwa jambo hilo litatajwa mara nyingi na kurudiwarudiwa kirefu, ama kutajwa peke yake. Takriri katika fasihi hukusudiwa kujenga msisitizo wa mlio na kuleta maana fulani. Mwandishi amezitumia takriri zifuatazo katika riwaya ya *Kuli*:

Mtunzi ametumia uradidi huu "alimbonyezabonyeza" (uk. 6). Anaelezea jinsi Mwingereza alivyombinya mfanyakazi aliyeumia na kumzidishia maumivu.

Maudhui yanayojitokeza ni ya ukatili. Aidha, ametumia uradidi "ndogondogo" (uk. 8). Anatoa mifano ya kazi ambazo Rashidi angeweza kufanya kulingana na umri wake mdogo. Maudhui ya dhuluma kwa watoto yanajidhihirisha.

Mtunzi ametumia uradidi "akishughulikashughulika" (uk. 12). Anasisitiza jinsi yule mzee wa Kishihiri alivyokuwa katika harakati ya kutekeleza kazi yake. Maudhui yanayojitokeza ni ya bidii maishani. Vilevile, mtunzi ametumia uradidi "pilikapilika" (uk. 15). Anatilia mkazo vile Rashidi alivyokuwa na shughuli nyingi zilizomzidishia njaa.

Uradidi mwingine ni "alibabaishababaisha" (uk. 30). Mtunzi anaashiria Rashidi alivyofanya kazi tofauti akawasidia magolona kufagia maghala naye akapewa shilingi mbili. Maudhui yanayojitokeza ni ya dhuluma kwa watoto. Mhusika Bi. Mashavu

ametumia uradidi “parkachaparkacha” (uk. 42). Mtunzi anaelezea jinsi Bi. Mashavu alivyokasirishwa na mwanawe Rashidi alipomwamsha usingizini. Maudhui yanayojitokeza ni ya uvivu.

Mhusika Rashidi alijiambia mwenyewe “Bepari ni bepari tu” (uk. 68). Alionelea kuwa mfanyabiashara yeyote sharti awanyanyase na kuwadhulumu wafanyakazi wake. Maudhui ya unyanyasaji na dhuluma unajitokeza. Pia, mhusika Rashidi ametumia uradidi anaposema “Mimi…mimi…..mimi….n‟‟ntaka kupendana na wewe.” (uk. 111). Takriri ya neno “mimi” inatilia mkazo kuwa Rashidi alitaka kuelezea alivyompenda Amina. Maudhui ya mapenzi yanadhidirika.

Vilevile, mhusika Rashidi ametumia uradidi anaposema “Nisamehe Amina, nisamehe mpenzi wangu, mpenzi wa roho yangu.” (uk. 131). Uradidi wa neno nisamehe unaelezea jinsi Rashidi alivyoomba msamaha kutoka kwa Amina. Mhusika Rashidi akiwa kortini aliona mambo “yanazungushwazungushwa” (uk. 195). Uradidi huu unaelezea kuwa William alimjibu Rashidi bila kuzingztia aliloulizwa. Maudhui yanayojitokeza ni ya dhuluma dhidi ya wafanyakazi.

Aidha, Rashidi anapoelezea kuhusu maisha yake anasema; “Mimi nasema kweli tupu, nimezaliwa katika taabu. Na kwa taabu tu, mimi taabu siogopi, nimelelewa katika taabu, taabu ndiyo iliyonilea” (uk. 189). Takriri ya neno taabu inasisitiza jinsi Rashidi alivyopata taabu tangu alipozaliwa akawa amezizoea. Maudhui yanayodhihirika ni ya umaskini miongono mwa wanajamii. Naye mhusika Amina ametumia uradidi anaposema “Maskini mume wangu! N‟‟na nani mimi tena! Ameniacha katika hali hii ya ujauzito! Maskini mume wangu! Maskini mume wangu!” (uk. 166). Uradidi

umetumiwa na mtunzi kusisitiza jinsi Amina alivyolia mumewe alipotiwa mbaroni. Mhusika Bakari ametumia uradidi anaposema “Jiteteeni! Jiteteeni! (uk. 183). Takriri ya neno hili linadhihirisha jinsi Bakari alivyowahimiza wafanyakazi bila kujali yatakayotokea mpaka maslahi yao yatiliwe maanani. Maudhui yanayodhihirika ni ya kupigania haki ya wafanyakazi.

3.7.2 Uradidi katika Riwaya ya Haini

Katika riwaya ya *Haini* tumechanganua aya ifuatayo:

> *“Aaaaa! Usivute masigara humu, huoni kama kuna mtoto mchanga na masigareti yako hayo ya kila wakati, he! Na huziachi hizo sigareti (uk. 4).*

Neno linalorudiwa ni sigareti. Neno hili limerudiwa mara tano hivyo basi msomaji ataliona kama uchimuzi. Msomaji atajiuliza kwani sigareti zina nini. Mwandishi anasisitiza hadhari za sigareti kwa mtoto mchanga kwani zitamdhuru afya. Kwa hivyo, sio vizuri kuvuta sigara mahali penye watoto wachanga. Jambo hili limetiliwa mkazo na mwandishi ili kutoa tahadhari kwa wanaovuta sigara katika jamii yake wajue kuwa zinadhuru afya zao na pia jamii nzima na hasa watoto. Sigareti husababisha ugonjwa wa kansa au saratani ya mapafu ambayo mwishowe husababisha kifo. Takriri ya neno hilo linamletea msomaji hisia za uoga anapokumbushwa kuhusu madhara ya uvutaji wa sigara na hata dawa zingine za kulevya ambazo zinatumiwa na wanajamii aliyonuia kuelimisha.

Kuna uradidi na pia mazungumzo yanayodhihirika katika matumizi ya visawe. Kwa mfano katika riwaya ya *Haini* kuna aya zifuatazo:

Wewe hujui sheria ya chui ndani ya zizi la mbuzi?" aliuliza Ambar naye. "Sheria ya chui ndani ya zizi la mbuzi ni rarua rarua, chana chana, kabakaba, ua wote. Hiyo nd`o sheria ya chui ndani ya zizi la mbuzi." Alisisitiza Ambar (uk. 137).

Kwa Haramia Kanali Bunju ni katili, jahili aliyekosa hata chembe ya huruma ndani ya moyo wake" Mnafiki! Mzandiki! Mungu amlaani!" Haramia alimlaani kimoyomoyo (uk. 167).

Visawe hivi vimetumiwa kumaanisha kuwaua mbuzi. Hali ya chui kuwa zizini ni mbaya kwani atawaua mbuzi wote. Mwandishi anamchorea msomaji taswira ya mbuzi waliouawa na chui. Uchimuzi huu utamwogofya msomaji naye ataendelea kusoma ajue yatakayotokea. Kwa hivyo, humpa ari ya kujua zaidi. Maneno *rarua, chana, kaba na ua* ni visawe. Aidha, maneno *katili, jahili, mnafiki na mzandiki* ni visawe. Maneno haya yanaonyesha usanii wa mwadishi na ujuzi wake wa kutumia lugha. Tumechukua baadhi ya matumizi ya uradidi na kuelezea kulingana na muktadha alioutumia mwandishi kuelezea maudhui na dhamira yake kwa msomaji.

Mwandishi anapotaka kuonyesha watu wakirudia kitendo fulani, anatumia mbinu ya takriri. Mtunzi ametumia uradidi huu "zimevuruganavurugana" (uk. 2). Anaelezea jinsi mbingu zilivyopambika kwa rangi ya kibuluu. Mtunzi ametumia uradidi wa neno "akapondwapondwa," (uk. 40). Anaelezea jinsi Hamza alivyocharazwa. Uradidi huu unauweka wazi zaidi ukatili na unyama kwa wafungwa. Maudhui yanayojitokeza ni ya ukatili.

Mtunzi ametumia uradidi ufuatao “Madhalim!” Madhalim!” (uk. 43). Anaashiria udhalimu waliotendwa wafungwa huko kwa Ba. Mkwe. Haiwezekani katika hali halisi kumwacha mtu aliye hai na maiti katika chumba kimoja. Maudhui ya unyama yanadhihirishwa. Aidha, mwandishi ametumia uradidi wa neno “Yametutumkatutumka” (uk. 46). Anaelezea jinsi mwili wa Hamza ulivyokuwa na uchungu kwa kupigwa na mateso, si wa kukaa si wa kulala. Maudhui ya uhayawani yanajitokeza wazi.

Pia, mtunzi ametumia uradidi “yamezonganazongana” (uk. 73). Anasisitiza jinsi wafungwa walivyokuwa na madevu na manywele matimtim. Mhusika Kanali Bunju ametumia uradidi huu “tumekufinyenifinyeni.” (uk. 167). Anaelezea jinsi wafungwa walivyopigwa na askari. Maudhui ya ukatili yanajidhihirisha.

Mhusika Khadija ametumia uradidi ufuatao “Sina nafasi leo!“‟ (uk. 183). Ametilia mkazo kuwa hangekubali kukutana na mhusika Azizi. Maudhui yanayodhihirika ni ya uasherati Azizi anapotilia mkazo kuwa sharti wangekutana na Khadija.

Mhusika Maburuki ametumia uradidi wa neno “Omba” (uk. 252). Anaomba usaidizi kutoka kwa Umoja wa Mataifa, kwa Pop na kwa Mashekhe waweze kutumia uwezo wao kuwatoa katika mikono ya madhalimu. Mhusika Maburuki na wenzake wanatumia uradidi “Tumeyakataa! Tumeyakataa!” (uk. 260). Wanasisitiza kuwa washtakiwa wote wameyakataa maelezo yaliyotolewa na Chopra mahakamani. Maudhui yanayodhihirishwa ni ya dhuluma. Mtunzi ametumia uradidi „„„yamemlengalenga” katika (uk. 265). Anaelezea jinsi Hamza alivyowakumbatia

Khadija na Subira kwa furaha iliyomjaa moyoni baada ya kuachiliwa gerezani, machozi yakamtoka machoni mwake.

Tumeonelea kuwa mwandishi ametumia uradidi kama mbinu ya ubunifu inayomsaidia kumuongeza ari msomaji na kutilia mkazo jambo analokusudia kusema. Pia, mbinu hii hutia mvuto zaidi katika lugha ya mwandishi na huleta athari kwa msomaji. Jambo hili linadhihirishwa na nadharia ya Kimtindo mhimili wa nane unaaoelezea kuwa sharti lugha ya mwandishi iwe na mvuto kwa msomaji.

3.8 Ukiushi na Uchimuzi wa Kisintaksia

Habwe, (2007), anasema sintaksia ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile kategoria za maneno, vikundi na vishazi.

3.8.1 Urefu wa Sentensi

Kuna aina tatu za sentensi kama vile, sentensi sahili ambayo ina kishazi kimoja kinachojisimamia, mara nyingi ni kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifu kinacholeta maana kamili iliyokusudiwa. Sentensi ambatano huundwa kwa kutumia viunganishi ili kuunganisha vishazi. Sentensi changamano huwa na kishazi kikuu kimoja kinachojisimamia pamoja na kingine au vingine visaidizi. Hii ni sentensi iliyochanganyika na ina tungo sahili na tungo tegemezi kama kipashio chake kimojawapo.

Ukiushi na uchimuzi unaoletwa na sentensi hutegemea ni mara ngapi aina hizo za sentensi zimetumiwa katika matini fulani. Kwa mfano, pale sentensi ndefu

zimetumika sana, sentensi fupi hutokeza kama ukiushi na uchimuzi. Vilevile, pale sentensi fupi zimetumika sentensi ndefu hutokea kama ukiushi na uchimuzi.

Katika aya ifuatayo kwa mfano, mwandishi ametumia sentensi ndefu na sentensi fupi. Matokeo ni kuwa sentensi fupi sio nyingi kwa hivyo huleta uchimuzi dhidi ya zile ndefu. Kwa njia hii hupata kutumika kusisitiza ujumbe.

Katika riwaya ya *Kuli* tumetumia aya ifuatayo kuchunguza matumizi ya sentensi ndefu na fupi.

> *(1)Kelele za nini saa hizi mama? (2) Unataka kuwaamsha watu bure.(3)Mimi nilikuwa kazini.(4) "Nimeshapata kazi nyingine," Rashidi alisema kwa sauti ya mtu aliyekwishakukua na utoto umekwisha kumtoka kabisa (uk. 58).*

Aya hii ilikuwa ya kumwomba na kumsihi mama yake aache kelele alizozoea. Kuacha kelele ndilo jambo muhimu alilotaka Rashidi kumfahamisha mama yake Bi. Mashavu. Kwa hivyo, baada ya kumsihi kwa kutumia swali la balagha Rashidi anamwelezea mama yake anayotaka kumwelezea katika sentensi ya (4) na anasisitiza ujumbe wake katika sentensi ya (4) anapomwambia amepata kazi nyingine kwa hivyo hana haja ya kumpigia kelele. Swali la balagha katika mwanzo wa aya litamwacha Bi. Mashavu akifikiria zaidi kinachomfanya ampigie Rashidi kelele wakati ule wa usiku watu wote wakiwa wamelala.

Katika riwaya ya *Haini* tumetumia aya ifuatayo kuonyesha ukiushi na uchimuzi.

(1)Maombolezo ya Nassor yakamchoma Hamza ndani ya moyo wake.(2) Mawazo ya mke na mtoto. (3) Yeye mwenyewe ndoa yake na Khadija bado changa na ndio kwanza amepata mtoto wake wa kwanza. (4) Amemwona wiki moja tu mara akakamatwa.(5) Hata jina hajawahi kumpa.(6)"Ntamwita masumbuko", aliwazo moyoni. (7) Akamtazama Nassor, sasa kilio kimemkolea (uk. 30).

Aya hii inaelezea taabu walizokuwa nazo wafungwa hadi kulia kwi kwi kwi. Sentensi ya (2) inaonyesha jinsi Hamza alivyoudhiwa na kilio cha Nassor akimlilia mkewe na wanawe akifikiria yeye pekee ndiye aliye na mke na mtoto humo chumbani. Akaanza kuwaza kumhusu mkewe na mwanawe. Sentensi ya (5) Hamza anamtafutia mwanawe jina, akawaza jina "Masumbuko" lakini baadaye akakumbuka kuwa nyimbo mbaya habembelezewi mtoto!

Kifungu hiki kinadhihirisha hisia zilizompata Nassor alipoanza kulia hadi Hamza naye akaingiwa na hofu akawaza na kuwazua jinsi alivyoshikwa kwa jambo lisilomhusu kamwe kabla hajampa mwanawe jina. Sentensi ya (3) inaleta ukiushi kwani ni ndefu nazo hizo zingine ni fupi. Tunaonelea kuwa mwandishi Shafi Adam Shafi ni stadi katika uteuzi wake wa sentensi kwani anaweza kuzitumia ndefu na fupi kwa makini.

3.8.2 Usambamba na Uradidi katika Sentensi

Mwania (2006), alilenga kuonyesha jinsi usambamba unavyochangia katika kuwasilisha ujumbe wa jamii lengwa. Alibainisha kuwa usambamba unadhihirika kupitia nyenzo za uchimuzi na ukiushi.

Riwaya za Shafi Adam Shafi zinamfanya msomaji kupitia kwenye hisia kali. Hisia hizi huelezwa kwa kutumia mbinu za usambamba na uradidi wa sentensi zinazomfanya msomaji kuingia kwenye hisia kali za mhusika katika riwaya. Kwa hivyo, hisia za kukata tamaa na kupoteza matumaini humpata msomaji. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anasema:

> *Hebu tazama safari ile waliposema tutayatengeneza mpaka leo wametengeza kitu gani? Ke mimi naona kila siku mambo yanazidi kuharihika tu, kila siku wenzetu wanafukuzwa kazini bure! (uk. 147).*

Rashidi anaelezea jinsi walivyondanganywa kuhusu mishahara yao kuongezwa lakini hawakutimiziwa. Kwa hivyo, Rashidi anaonekana amekata tamaa na kukosa matumaini kuwa wataongezewa mishahara.

Katika riwaya ya *Haini* kuna mfano ufuatao:

> *Yeye anasema ati tunayajua, tumeyapanga sisi tunajua nini? Sisi tumepanga nini Kuchi? Sisi hatuna tunalolijua wala hakuna tulichokipanga sisi tumedokezwa tu na huko kudokezwa ndiko* kuli*kotuponza," aliendelea kusema Haramia (uk. 158).*

Mwandishi anautumia usambamba na uradidi anapoyarudia maneno tunayajua, tumeyapanga na tumedokezwa ili kusisitiza ukosefu wa matumaini uliomjaa Haramia.

Wakati wahusika wengine wanakata tamaa kuna wao wenye ujasiri ambao hawawezi kuvumilia shida hizo na huamua kutoroka ingawa hawana uhakika watafaulu lakini huwa na matumaini mema.

Pia, katika riwaya ya *Haini* Sururu anapanga mpango wa "Kata Mbuga" na anatoroka ingawa anashikwa na kurudishwa jela baada ya kupigwa vibaya. Mwandishi anatumia usambamba anasema:

> *Aliukamata waya wa senyenge akajaribu kuuparamia na kila alipousukuma huku na kutaka kuukiuka afike upande wa pili wa ule waya, ncha zake zilimchocha na kumtoboatoboa mikono na miguu. Alinyanyua mguu kutaka kuukiuka, ncha moja ikamchana paja; ncha nyingine ikamchana mkono alipojaribu kuuparamia (uk. 121-122).*

Katika riwaya ya *Kuli* mhusika Chum anajitokeza kuwa na ujasiri anapoenda kwa kamishna kumuuliza kuhusu Bakari na Faraji walipokuwa wamefungiwa chumbani mwandishi anasema:

> *Chum alikuwa mwepesi wa kufikiri na kabla hapajazungumzwa chochote katika mkutano ule alisema, "Nafikiri hatuna haja ya kuzungumza mengi, wenzetu bado wapo ndani wanateseka bure na wala hatujui. Mimi naona bora sasa hivi tena bila ya*

kupoteza wakati, tufunge safari nini litawatokea twende tukaonane na kamishna wa polisi (uk. 91).

Kuna wakati mwandishi anaamua kutumia uradidi wa vitenzi kimakusudi akarudia neno mara mbili au zaidi. Kisha maneno hayo hujitokeza wazi. Kwa mfano katika riwaya ya *Kuli* anaposema:

*Baada ya kumaliza maneno yake Faraji alitoka nje kwa ghadhabu. Wafanyakazi wengine wote walikuwa wanasubiri nje; wamejiinamia kwa majonzi ya mwenzao wanasubiri matokeo. Walikuwa na hamu ya kujua hatua gani itachu*kuli*wa kuhusu marehemu Manafi (uk. 83).*

Aya hii inaelezea kuwa madai waliotoa kina Faraji hayakuzaa mazao yoyote kwani hayakutiliwa maanani na George aliyedai Manafi ni mtu wa *daily pay*. Pia, inaelezea uchungu waliokuwa nao wafanyakazi hao walipogundua kuwa matakwa yao hayangetimizwa. Uchimuzi unajitokeza Faraji anapokata tamaa na kutoka nje kwa kuukubali ukweli kuwa wataendelea kunyanyaswa. Kukubali kunyanyaswa pia kunaonekana kupitia wahusika kama vile Mzee Tindo anayehongwa ili awazuie wenzake kudai haki yao. Lakini kuna wao wenye ujasiri wa kukataa kuyakubali maovu wanayotendewa na waajiri na kuamini kuwa kuna kiwango cha uovu ambao mtu hawezi kuvumilia. Hawa ndio wanaotumainia kuwa na mabadiliko, ingawa hawaoni dalili zozote wanatarajia sharti wapate mapinduzi. Mwandishi anazingatia maoni yao. Kwa hivyo, lazima aweze kuzikabili hisia zinazomfanya mtu asijali, awe na ukosefu wa matumaini na aweze kumwelezea msomaji kwa mkazo zaidi kwa

kutumia sifa nyingine ya usambamba. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anasema:

> *Kutokana na mazungumzo na wenzake Rashidi alibaini kuwa mgogoro mkubwa uliokuwa unaendelea kati ya wafanyakazi wa bandarini na wakuu wao wa kizungu haukuwa mzuri, na wakuu hao walikuwa wakiwasemesha wafanyakazi kwa chuki na jeuri na mengine ndiyo kama yale aliyofanyiwa yule mfanyikazi aliyekuwa akisinzia wakati wa kusuka kamba (uk. 72).*

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anasema:

> *Walitaka kusikia Mzee Machale atasema nini. Labda anajua lolote kuhusu hatima yao. Labda litamtoka neno la heri litakalowapa matumaini, neno litakalowaondolea majonzi yaliyojaa ndani ya nyoyo zao, neno litakalojenga matumaini ndani ya nyumba ile iliyojaa hofu na vitisho vilivyowagubika gubi gubi katika maisha yao ya ndani mle Mchana na usiku. Mpaka wakakata tamaa ya yale matumaini madogo waliyokuwa nayo yakafifia kabisa, wasione chochote mbele yao ila mauti na nakama tu (uk. 55-56).*

Wakati mwandishi anapotumia usambamba, msomaji atajua kuwa anataka agundue kuwa watu waliokuwa katika jamii yake walikuwa wanasiasa. Jambo hili ni muhimu kwani baadaye kutakuwa na mapinduzi katika jamii hiyo. Mwandishi pia ametumia

usambamba kuelezea jinsi mhusika anavyoweza kukiri hatia yake na kuweza kujilaumu akaona alikuwa akikosea kimaadili.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Kuli* Rashidi anamwelezea Amina kuwa alikuwa amemkosea alipoenda kwao akiwa mlevi anaposema:

> *Nisamehe Amina, nisamehe mpenzi wangu, mpenzi wa roho yangu. Nilikuwa nimelewa na wala sikujua nililokuwa nikifanya. Mimi Amina silewi lakini siku ile rafiki yangu Salum, yule tuliyefuatana ngomani tulipokutana mara ya kwanza, alinitia ushetani akanilewesha. Basi Amina nakuomba unisamehe, nakushika miguu na nakuahidi sitorejea tena kitendo kama kile (uk. 131).*

Wakati haya maneno yaliposemwa katika hadithi, Rashidi alikuwa akiomba msamaha kwa kwenda nyumbani kwa akina Amina akiwa mlevi jambo ambalo lilimdunisha yeye mwenyewe na pia ni laana katika jamii kwenda kwa wakwe ukiwa mlevi na mtovu wa nidhamu. Maneno Nisamehe Amina, Nisamehe mpenzi wangu ni ishara kuwa Rashidi alikuwa amejitambua, amejikosoa mwenyewe na akayaona makosa yake yanayoonekana kupitia sifa za usambamba katika maneno nakuomba, unisamehe, nakushika miguu. Kwa kweli, Rashidi alijua wazi kuwa hangeuvunja urafiki wake na Salum. Kwa hivyo, athari za uchimuzi huu ni kukiri makosa yake, kujihurumia na kujilaumu.

Mwandishi anadhihirisha hisia za mapenzi. Mhimili wa tano wa nadharia ya Kimtindo unapendekeza mwandishi adhihirishe hisia zake anapoandika kazi yake kwa hivyo kuonyesha uwiano na kazi hii.

Katika riwaya ya *Haini,* mwandishi anaelezea jinsi Haramia baada ya kumuua chatu kule Mashakani Hotel alivyoonelea heri ayakubali yote atakayoambiwa na Kanali Bunju badala ya kurudishwa Mashakani Hotel anasema:

> *Mimi ni mateka wenu. Nimekwishasalimu amri kwenu, chochote mnachokitaka mimi nitalifanya, lolote mnalolitaka mimi nitalisema. Kama mtanisikiliza mimi nisikilizeni, kama kuna wengine mnaowasikiliza hiyo ni hiyari yenu (uk. 177).*

Usambamba unajitokeza Haramia anapotumia neno *mimi* mara nne kuelezea kuwa anakubali aambiwalo anaposema:

> *Mimi ni mateka wenu…Mimi nitakifanya,…*
>
> *Mimi nitalisema,...Mimi nisikilizeni.*

Mbinu hii inasisitiza jambo muhimu analoelezea mwandishi na kumfanya msomaji kulifikiria analoelezea mwandishi kwa undani zaidi. Katika nadharia ya Kimtindo mhimili wa tano unasisitiza kujiweka wazi kwa hisia za mwandishi. Jambo linalodhihirika kwani mhusika Haramia ana hisia za dhihaka anapokubali kuwa hatakataa atakaloambiwa. Tunaonelea kuwa ni vizuri mwandishi huzitoa hisia zake anapoandika kwani ni mmojawapo wa jamii yake na anawasilisha hisia zao kwa jumla.

3.9 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua ukiushi na uchimuzi wa maneno. Tumezingatia matumizi ya mlazo, lafudhi, misemo, methali, uradidi wa maneno, na matumizi ya kisintaksia kuonyesha urefu, usambamba na uradidi katika sentensi. Katika sura ya nne tutachanganua ukiushi na uchimuzi wa maana.

SURA YA NNE

UKIUSHI NA UCHIMUZI WA MAANA

4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumechanganua uchimuzi na ukiushi wa maneno kama mbinu za mtindo. Katika sura hii tumebainisha ukiushi na uchimuzi wa maana. Kisarufi maneno hayo kwa kawaida huhusu uvunjaji wa kanuni na uteuzi wa maneno. Katika sura hii tumechanganua mbinu za lugha kama vile sitiari, tashibihi, tabaini, tanakali, tashihisi, jazanda na ishara. Tamathali hizi zimechanganuliwa kulingana na vile mtunzi alivyozitumia kudhihirisha ukiushi na uchimuzi katika kazi zake.

Wamitila (2008), anasema kuwa mtindo hujumulisha zile mbinu ambazo mwandishi atazitumia katika kufaulisha na kuwasilisha ujumbe wake, anaendelea kusema kuwa ni jumla ya vipengele ambavyo mwandishi atavifungamanisha katika kuwasilisha ujumbe. Katika kufanya hivyo, mtindo huo huweza kujukuliwa kama tabia ya mwandishi huyo.

4.1 Dhana ya Sitiari

Kwa mujibu wa King'ei na Kemoli (2001), sitiari ni matumizi ya lugha yenye kufumba maana ilimradi kutilia mkazo jambo linaloeleza kama pambo. Vitu viwili hulinganishwa kwa kutumia neno "ni". Kwa hivyo, sitiari haina maana moja bali inaweza kufasiriwa kwa njia kadha.

4.1.1 Sitiari katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi ametumia sitiari kadhaa kama vile; “ni bingwa” (uk. 19). Inaelezea jinsi wafanyikazi bandari walivyokuwa hodari kwa kutumia matusi. Wafanyikazi bandirini wanalinganishwa na bingwa wa kutukana. Mhusika Rashidi anatumia sitiari “ni jungu” (uk. 64). Anayalinganisha mambo yaliyokuwa yakiendelea kazini na jungu likipikwa. Sitiari “maisha ya moto” (uk. 55). Imetumiwa na mhusika Rashidi anayalinganisha maisha na moto. Rashidi anasema wafanyikazi wa bandarini “ni madume” (uk. 65). Anawalinganisha na Mzee Tindo na Farjalla waliokataa kuwatetea wafanyikazi akawaona jasiri kwani waliweza kudai nyongeza ya mishahara yao. Mhusika Amina ametumia sitiari “yule shetani” (uk. 159). Anamlinganisha Faraji na shetani kwani kila alipoenda kwao ilikuwa ni lazima Rashidi angeandamana naye.

4.1.2 Sitiari katika Riwaya ya Haini

Mtunzi ametumia sitiari “lilikuwa jitu” (uk. 102). Mhusika Mheshimiwa Masaburi anafananishwa na jitu la dhiraa mbili, mwingi wa mwili, kifua kipana, mkono umejaaa kama kozi la mnazi. Mhusika Kanali Bunju alijinasibu kuwa yeye “ndiye jabari” (uk. 165). Mhusika anajilinganisha na jabari kwani hata kama hakukirithi kiti cha Kigogo alikuwa na madaraka yasiyokuwa na kikomo. Sitiari nyingine ni “ni bingwa” (uk. 53). Inamlinganisha mhusika Doto na mjuzi wa kuongea kwa ishara za vidoto. Mhusika Doto alitumia sitiari “ni binadamu” (uk. 67). Aliwaza jinsi binadamu anavyoweza kukosa huruma, akajifanya yeye ni bora kuliko wengine. Mhusika Chopra ametumia sitiari “wewe ni haini tu!” (uk. 251). Chopra anamlinganisha mhusika Heri na haini kwa kudai alishiriki katika mauaji ya Kiongozi Kigogo. Mhusika Haramia ametumia sitiari “ni katili, jabili” (uk. 167). Anaitumia

anapomlinganisha Kanali Bunju na hayawani asiye kuwa na hata chembe ya huruma ndani ya moyo wake. Sitiari nyingine iliyotumiwa na mtunzi ni “ni kitendawili” (uk. 228). Wahusika wote waliona siku hiyo kama kitendawili na kila mmoja wao akijaribu kukitegua. Wafungwa wote walisubiri kwa hamu. Hii ni siku waliopelekwa mahakamani kesi yao isikilizwe. Mhusika Abdul anawalinganisha wafungwa wote na muhanga anaposema “sisi ni mhanga” (uk. 89). Anaelezea jinsi wengine wataweza kupata nusura baada ya kuuawa kwa Kiongozi Kigogo kwani wananchi wangeweza kupata bidhaa muhimu kama sukari na mchele. Vilevile, mhusika Sururu ametumia sitiari “ni kachero” (uk. 116). Anaitumiwa alipotolewa Zonga aliyedhani atakuwa mwenziwe katika utoro. Sururu alishangazwa na jinsi alivyomwamini karibu amweleze nia yake ya kutoroka. Anamlinganisha na mpelelezi aliyepelekwa gerezani ili aweze kupeleleza mambo. Mhusika Faraji amemtusi Ambar kuwa “ni mjinga” (uk. 138). Sitiari hii inamfananisha Ambar na mtu mpumbavu. Matusi ya Faraji yanamfanya acharazwe vibaya na Ambar anapomchupia kwa ghafla kama simba anavyomrukia paa amwindaye. Mhusika Faraji anamuuliza Swedi kinachomchekesha kwa sababu yeye “ni mtu mkimya” (uk. 137). Faraji anamlinganisha na mtu asiyeongea kila wakati. Mtunzi pia ametumia sitiari “ndio viduhushi” (uk. 134). Wapishi wanaopeleka uji wa alfajiri na chakula cha mchana wanalinganishwa na wapelelezi wanaopeleleza yanayotokea mle Kumbakumba. Aidha, mtunzi anaitumia sitiari “yu majinuni” (uk. 172). Anamlinganisha mhusika Haramia na mtu aliyerukwa na akili. Haramia alishtuka sana alipomwona Chatu alivyojinyumbua akijitayarisha kumshambulia.

Mwandishi amezitumia sitiari kama mbinu ya uhamishaji wa maana kuipamba lugha na kumtia ari msomaji. Mbinu hii imemsaidia mwandishi kulinganisha vitu viwili bila ya kutumia viungio kama “mithili ya” au “kama.” Maoni yetu ni kuwa matumizi ya sitiari hudhihirisha ulinganishi wa moja kwa moja. Ufaafu wa nadharia ya Kimtindo unajiweka wazi kwani mwandishi ametumia tamathali hii ya usemi kuifanya kazi yake iwe na mvuto kwa msomaji. Mhimili wa saba unahimiza matumizi ya lugha yenye kumvutia msomaji.

4.2 Dhana ya Tashibihi

Karuga (2005) anaelezea kuwa mbinu ya tashibihi hulinganisha kitu kimoja na kitu kingine katika hali ya utendaji, sura, rangi, tabia au jinsi ya kujimudu. Maneno kama vile mithili ya, sawa na, mfano wa, hutumika kuleta ufananishaji. Hutumiwa kujenga maudhui na taswira.

4.2.1 Tashibihi katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi amezitumia tashibihi, tumezitolea maelezo baadhi ya tashibihi hizi kulingana na muktadha aliotumia mwandishi kuwasilisha maudhui na dhamira yake.

Mwandishi anaelezea kuhusu chumba cha Bi Mashavu kupitia kwa tashibihi hii “ilivuja kama mwembe” (uk. 16). Nyumba hiyo ilivuja maji kwa wingi wakati wa mvua ya masika. Bi Mashavi na mumewe Majaliwa walikuwa na mtoto mmoja tu “kama chongo” (uk. 20). Tashibihi hii inaelezea hawakuwa na mtoto mwengine.

Mtunzi anaelezea jinsi Rashidi alivyolemewa na gunia lenye uzito mkubwa akaenda “kama mtoto mchanga” (uk. 38). Tashibihi hii inatumiwa kuonyesha jinsi Rashidi alivyokuwa mdogo bila nguvu za kulibeba gunia. Maudhui ya ukiukaji wa haki za

watoto yanadhihirika. Kulingana na kuli mmoja walifanya kazi ya kitumwa, akaonelea wanatumiwa “kama punda” (uk. 62). Tashibihi hii inaashiria jinsi wafanyakazi bandarini walivyotumiwa vibaya na waajiri wao waliowalipa mishahara duni. Maudhui ya ubinafsi na unyanyasaji yanadhihirika.

Kauli nyingine iliyotumiwa na Rashidi ni “kama mbwa” (uk. 54). Inaashiria vile Rashidi alivyofukuzwa na Morarji badala ya kumpa kazi. Maudhui ya ubaguzi wa watoto yanajitokeza katika jamii. Mtunzi anapoelezea jinsi Rashidi alivyomnyemelea Ramju na kumgusa anaitumia tashibihi “kama paka” (uk. 56). Anaelezea vile Rashidi alivyoenda alipokuwa Ramju polepole.

Wahusika Chum, Ubwa na Mbaraka walipoenda kumwona kamishna wa polisi waliingia ndani ya ofisi yake. Mtunzi anaelezea kuwa macho yake yalikuwa yanang‟ara “kama ya paka” (uk. 91). Tashibihi hii inatumiwa kuelezea jinsi alivyokuwa na macho ya kuogofya. Pia, ameitumia tashibihi hii “kama kiboko” (uk. 90). Anaelezea ukubwa wa ofisa wa Kiingereza waliomkuta Bakari na Faraji akawatazama kwa hasira na kuwauliza walichotaka.

Mtunzi ametumia tashibihi hii “kama chatu” (uk. 100). Anaelezea kuhusu njia iliyotumiwa na Rashidi. Vilevile, ameitumia tashibihi hii “kama sumaku” (uk. 105). Anaelezea jinsi Rashidi alivyovutiwa na msichana aliyecheza taarab akamuuliza Salum kama anamjua. Aidha, mwandishi ametumia tashibihi “kama kishada” (uk. 120). Anaelezea vile Rashidi alivyotembea. Maudhui yanayojitokeza ni ya dawa za kulevya.

Pia, mtunzi ametumia tashibihi “kama ugonjwa wa safura” (uk. 155). Maelezo haya yanaelezea jinsi Amina alivyokuwa amekasirishwa na Rashidi akanuna. Maudhui ya urazini yanatumiwa kuonyesha Amina alikuwa hajaelewa umuhimu wa Rashidi na wenzake kupigania haki zao. Aidha, mwandishi anaendelea kutumia tashbihi hii “kama upepo” (uk. 161). Tashibihi inaashiria jinsi usiku huo ulipoisha haraka na mara asubuhi ya Jumamosi ikaingia.

Mtunzi anapoelezea jinsi Rashidi na ofisa wa kingereza walivyotupiana macho anaitumia tashibihi “kama majogoo” (uk. 163). Tashibihi hii inadhihirisha jinsi mapambano ya makuli yalivyopamba moto wakidai kuongezewa mishahara yao.

4.2.2 Tashibihi katika Riwaya ya Haini

Mtunzi ametumia tashibihi ananuka “kama fungo” (uk. 13). Kauli hii ni maelezo ya jinsi alivyokuwa mchafu kabla ya kuoga, kupiga mswaki na kuchana nywele.

Tashibihi nyingine ni “kama pilipili” (uk. 22). Anaitumia kuelezea macho ya askari aliyemsimamia Hamza akifanya kazi yalivyokuwa mekundu ya kutisha. Vilevile, tashibihi inayoelezea hali ya Hamza akiwa katika chumba cha kiza ni “kama mtoto” (uk. 92). Inatumiwa kuonyesha jinsi mhusika Hamza alivyokuwa mnyonge akashindwa kutembea akajishikilia asianguke.

Maudhui ya ukatili nayo yanadhihirisha uovu waliokuwa nao askari wakamtia katika chumba cha kiza kwa siku kumi na mbili. Kulingana na mtunzi maisha ya jela yalikuwa magumu kwa Hamza, anatumia tashibihi “amekonda kama uzi” (uk. 140). Mwandishi anaendeleza maudhui ya unyanyasaji na mateso gerezani. Anaelezea kuwa Hamza alikuwa amedhoofika sana.

Aidha, ametumia tashibihi “kama askari” (uk. 2). Hali hii inarejelea mhusika Pango alipoamrisha kina Kassim, Fadhil na Hamza watoke waliposikia mlio na kishindo tu-tu-tu.

Mhusika Hamza anaitumia tashibihi “Kama majambazi” (uk. 6). Anaelezea jinsi usiku ulivyokuwa mrefu aliupata usingizi akalala fofofo, mpaka aliposhituliwa kwa vishindo vya watu waliogonga mlango. Mwandishi pia ametumia tashibihi “kama kaburi” (uk. 43). Anaelezea jinsi Hamza alivyokiona chumba alichoachwa peke yake na maiti huko kwa Ba Mkwe. Alikuwa chumbani na maiti makusudi ili iwe onyo kwake akawa na hofu kubwa.

Mwandishi vilevile ametumia “mithili ya” katika tashibihi ili kulinganisha vitu viwili anaposema; “mithili ya mtu aliyewahi kuugua ndui au tetekuanga” (uk. 24). Tashibihi hii inaulinganisha uso wa Masanja na mtu aliyeugua ugonjwa wa ndui au tetekuanga kwa jinsi ulivyojaa vikovu. Vilevile, “mithili ya beberu lililopea” (uk.24). Kumaanisha ndevu zile zilikuwa kama za beberu aliyekua vizuri au msese, ndege mwenye mdomo mrefu. Tashibihi “mithili ya dafu lililochongwa vizuri” (uk. 25). Mwandishi anaelezea jinsi uso wa Kondo ulivyokuwa duara kama dafu lililochongwa vizuri. Aidha, “mithili ya mgonjwa aliyegubikwa na homa kali” (uk. 47). Tashibihi hii inalinganisha hali ya woga aliokuwa nao Hamza uliomtetemesha kama mgonjwa aliye na homa kali. Huu ni uoga mwingi kushinda wa kunguru akimbizaye mbawa zake. Tashibihi “mithili ya mtu anayeelea (uk. 67). Kumaanisha Hamza hakumwoa vizuri kwa sababu mwili wake wote ulikuwa umedhoofika baada ya kurushwa ndani ya kisima. Hizi ni baadhi ya tashibihi alizotumia mwandishi katika riwaya ya *Haini*, kwa

kweli ameitumia mbinu hii sana katika riwaya hii. Tumeshuhudia ya kwamba mwandishi anadhihirisha umahiri wake wa kuitumia mbinu hii. Nadharia ya kimtindo katika mhimili wa tano unaoyesha umuhimu wa matumizi ya tamathali za usemi ikiwemo tashibihi.

4.3 Dhana ya Tabaini

Kuligana na Kamusi Sanifu, (2004), tabaini ni tamathali ya usemi yenye dhana ya kukinzana lakini maana ya msingi haibadiliki.

4.3.1 Tabaini katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi Shafi Adam Shafi ameitumia mbinu ya ubunifu ya tabaini katika riwaya ya *Kuli* ili kuirembesha lugha iwe na mvuto anapotumia maneno yanayokinzana kwa mfano, mtunzi ametumia tabaini "wakiingia na kutoka" (uk. 28). Inaelezea jinsi Rashidi alivyobakia mbele ya banda la mabati akiangalia yaliyotendeka. Tabaini nyingine ni "yalikuja na kuondoka" (uk. 26). Imetumika kuashiria magari yaliyotoka shamba na bidhaa ya karafuu. Maana yake ni kuwa magari yalipakuliwa kisha yakarudi shambani.

Aidha, Mwandishi ametumia tabaini "akaking‟ng‟ania na kung‟ang‟anua" (uk. 25). Anaashiria kuwa Mhusika Rashidi aliposukumwa alikazana kushikilia chuma na hakuna angeweza kumuondoa. Vilevile, tabaini ambayo imetumiwa na mtunzi ni "alipanga na kupangua" (uk. 23). Mhusika Rashidi anawaza jinsi binadamu ataishi maisha yenye shida akawaza na kuwazua.

Mhusika Rashidi ametumia tabaini "wanatutia huku wakitutoa" (uk. 62). Rashidi alilalamika walivyotumiwa kama punda bila nyongeza ya malipo. Maudhui

yanayojitokeza ni ya unyanyashaji. Pia, mwandishi ametumia tabaini “kujenga na kubomoa” (uk. 126). Inaashiria jinsi Rashidi alivyofikiria kuhusu ndoa yake na Amina akawaza na kuwazua.

Mhusika Amina ameitumia tabaini “heri wala shari” (uk. 112). Anaashiria jinsi mtoto Zainabu alivyondanganywa na mchumba wake aliyemkimbia baada ya kujifungua hakumjali kamwe. Amina alimtaka Rashidi amhakikishie angempeda wakati wa raha na shida. Naye mhusika Farhani anatumia tabaini “wazima au wagonjwa” (uk. 137). Anaelezea jinsi Rashidi alivyokaa kwa muda mrefu bila kuwajulia hali.

Mtunzi ametumia tabaini “waliingia na kutoka” (uk. 117). Inaelezea jinsi Rashidi alivyowaona watu wakiingia ndani ya kijumba kisha wakatoka wakiwa wanatukana ovyo na wakipepesuka wakiimba nyimbo zisizo mwanzo wala mwisho.

Pia, ametumia tabaini “furaha na huzuni” (uk. 197). Anaashiria kuwa Rashidi anaposoma barua ya mkewe Amina alipigwa na butwaa akaisoma tena na tena. Aidha, mtunzi anatumia tabaini “akisinzia na kuzinduka” (uk. 195). Anaelezea jinsi hakimu alivyoinamisha kichwa chake chini akafikiri na baada ya kushtuliwa aliinua kichwa chake akasema angetoa hukumu siku ya Ijumaa.

4.3.2 Tabaini katika Riwaya ya Haini

Pia, katika riwaya ya *Haini* mwandishi ameitumia mbinu hii ya tabaini kuelezea maudhui yake kwa mfano, ametumia tabaini “si maiti yu hai” (uk. 26). Anaelezea jinsi Sugu alivyokuwa fremu ya maiti, uhai wenyewe wa mafupa matupu ila yeye hakufa. Naye mhusika Khadija aliomba Mungu awasalim salama kwa kutumia tabaini

hii ”Kheri wala shari” (uk. 5). Anaashiria hali ilivyokuwa watu walipoelezwa wasitoke vyumbani.

Mtunzi ametumia tabaini “ilipofunguliwa na kufungwa” (uk. 12). Anaelezea vile Hamza alivyokuwa na wasiwasi kwani wafungwa wenzake walitolewa vyumbani mwao. Alfajiri mlango wa chumba chake ukafunguliwa akaona askari amemsimamia kama Ziraili aliyekuja kumtoa roho. Mhusika Sururu anatumia tabaini hii “si wa mkono wala si wa mguu.” (uk. 127). Anaelezea kuwa kama angekuwa kule kumbakumba, angetiwa katika chumba cha kiza alale majeruhi ndani ya dimbwi la maji.

Vilievile, mtunzi anatumia tabaini “si kusi si kaskazi” (uk. 187). Anaashiria upepo mzuri wa forodhani ambao hauna majira. Anaendelea kuelezea jinsi Khadija alivyofurahishwa na hewa hiyo pale barazani alipokaa akiwaza juu ya salamu alizokuwa nazo Azizi.

Mtunzi ameelezea jinsi kwa Ba Mkwe kulivyo kimya jii, anaitumia tabaini “si mchana si usiku” (uk. 43). Inaashiria kuwa wafungwa hawakuona kitu ila kiza totoro kimetanda mbele yao. Vilevile, mtunzi ametumia tabaini hii “si wa kukaa si wa kulala” (uk. 46). Anaelezea jinsi mhusika Hamza alivyokuwa chumbani akiwa peke yake mwili wote umejaa maumivu ya kilio na mateso.

Wahusika wanaongea vile Mzee Machale alivyokaa gerezani sana. Mwandishi ametumia “uongo na ukweli” (uk. 58). Anamaanisha waliongea juu ya mambo yaliyokuwa ya kutoka nje, yakakuja, yakaingia gerezani hivyo yakawa bila uhakika na ukweli.

Mtunzi ametumia tabaini hii “likapanda na kushuka” (uk. 64). Anaelezea jinsi Hamza alivyolisikiliza lile gari lilivyoguruma kwenye vilima na mabonde. Pia, ametumia tabaini hii “ukitaka usitake” (uk. 65). Anaelezea jinsi Hamza alivyozongwa kamba mwili nzima.

Vilevile, mwandishi ametumia tabaini nyingine “kufa kupona” (uk. 66). Anaashiria jinsi Hamza alivyotumbukizwa kisimani ili akiri kuwa ndiye aliyemuua Kiongozi Kigogo, ilimbidi awandanganye askari wale kuwa anasema ukweli ili kuyanusuru maisha yake.

Kuna tabaini “si wa dunia hii si wa ahera” (uk. 67). Inaelezea jinsi mhusika Doto alivyomsaidia Hamza baada ya kuteswa na askari. Doto pia alistaaajabu jinsi binadamu anavyoweza kukosa huruma kwa mwenzake kiasi cha kumtesa nusura afe.

Mwandishi ametumia tabaini kama mbinu ya kulisisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayoonyesha msisitizo wazi, tabaini pia hupamba lugha na kuifanya iwe ya kupendeza na kumfanya msomaji aweze kufikiria zaidi juu ya maana anayokusudia mwandishi.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi ametumia tabaini katika riwaya zake mbili ili kusisitiza analosema. Mhimili wa nane wa nadharia ya Kimtindo unamhimiza mwandishi kuitumia lugha inayomtia ari msomaji. Kwa hivyo, mwandishi anatumia lugha yenye mvuto naye msomaji akaweza kuendelea kusoma. Nao ufaafu wa nadharia hii unajitokeza kulingana na mhimili wa nane wa nadharia ya Kimtindo.

4.4 Dhana ya Tanakali

King‟ei na Ndungo (2005), wanaelezea tanakali kama neno linalotokana na neno “nakili” ambalo humaanisha “iga” au “fuatisha”. Hutumia maneno yanayoiga sauti au yanayojaribu kudhihirisha sauti au milio mbalimbali inayoambatana na vitendo tofauti.

4.4.1 Tanakali katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi anatumia tanakali ili kujenga picha katika akili ya msomaji. Tanakali alizotumia katika riwaya ya *Kuli* ni kama zifuatazo, tumezitolea maelezo kulingana na mazingira aliyozitumia mwandishi. Kwa mfano, tanakali hii mtunzi anapoelezea jinsi Majaliwa alivyolala ametumia tanakali “amejifunika gubigubi” (uk. 2). Inaashiria jinsi alivyojifunika shuka hadi saa moja na nusu kwa sababu alikuwa akiumwa. Aidha, tanakali iliyotumiwa ni “zilitulia tulii” (uk. 89). Imetumiwa na mwandishi kuelezea vile bandari ilivyokuwa shwari na zile ghasia na vishindo vya kawaida havikuonekana kabisa.

Tanakali mbili zinazoonekana ni “jii” na “chopi” (uk. 125). Mtunzi anaelezea jinsi Salum alivyokaa chumbani akiwa amelewa kupindukia. Vilevile, ameitumia tanakali “walichukua kitikiti” (uk. 165). Hali hii inarejelea mhusika Rashidi alivyochukuliwa na askari na kumtia ndani ya gari la polisi. Mwandishi ametumia tanakali nyingine “ubelaubela” (uk. 174). Anaelezea jinsi mhusika Faraji wakiwa na Bakari walivyolibeba kapu kubwa waliloletewa na dereva aliyelowa jasho mwili mzima. Aidha, mwandishi ametumia tanakali ifuatayo “kuenea vururu” (uk. 180). Inatumiwa na mtunzi kuelezea jinsi karatasi zilizotawanywa sokoni zilivyoenea mjini.

4.4.2 Tanakali katika Riwaya ya Haini

Kauli nyingine ni “jii” (uk. 5). Tanakali hii imetumiwa na mtunzi anapoelezea jinsi kulivyokuwa na kimya kingi wakati Khadija alipokuwa akimyonyesha mwanawe. Aidha, mwandishi ametumia tanakali “lala fo fo fo” (uk. 6). Anaelezea kuwa Hamza alikuwa ameukosa usingizi mpaka jogoo la kwanza lilipowika ndio alipoupata nao ukamgubika. Mtunzi ameendelea kutumia tanakali kama vile “vikimetameta, “mwetu, mwetu!” (uk. 8). Anaelezea jinsi Hamza alivyopigwa kofi kubwa na mkuu wa kituo cha polisi cha Malindi nalo likampumbaza asio ne chochote.

Tanakali nyingine aliyotumia mwandishi ni “ananuka hffu!” (uk. 21). Inaashiria jinsi mhusika Sururu alivyokuwa amepigwa baada ya kurejeshwa alipotaka kutoroka. Mwili wake ulikuwa umeoza akawa hajijui hajitambui.

Tanakali ifuatayo imetumiwa na mtunzi “kimekwisha, fyuu” (uk. 22). Anaelezea jinsi chakula walichopewa wafungwa kilivyokuwa kidogo na kamwe hakikuwatosha. Pia, anaendelea kutumia tanakali hii “Damu, mwaaa,” (uk. 40). Anaelezea vile Hamza alivyotiririkwa na damu baada ya kutwangwa kichwa na askari usalama akitumia gongo la mpera.

Vilevile, ametumia tanakali “akitandikwa mipera, pu-pu-pu,” (uk. 46). Anaelezea jinsi wafungwa walivyotandikwa wakasikika wakilia na kuomba msamaha. Tanakali nyingine ni “linang‟ara, jeupeee.” (uk. 77). Mtunzi anaashiria jumba kubwa la kizamani la ghorofa moja ambalo lilionekana kama gofu lililohamwa lakini likapakwa chokaa likang‟ara.

Tanakali hii ameitumia mtunzi “wamekwama, ngwa!” (uk. 83). Kauli hii ni maelezo ya jinsi mhusika Hamza alivyowaza aliyoambia na Kanali Maisara, awavutie wafungwa wenzake wakubali uhaini mwishowe wauawe wote. Pia, mtunzi ametumia tanakali “Jasho chururu.” (uk. 86). Inadhihirisha vile mhusika alivyoingizwa chumba cha kiza vuke la chumbani likamfukiza akawa kama aliyetiwa ndani ya tanuri. Mtunzi pia ametumia tanakali nyingine “zzuuuum!” (uk. 122). Kauli hii imetumiwa na mhusika Koplo Ngwali alipotaka kumpiga risasi mhusika Sururu alipouparamia ukuta akitoroka jela.

Mhusika Haramia ametumia tanakali hii “Tena tukatae katakata” (uk. 156). Anawaambia wakifika mahakamani waelezee jinsi walivyopigwa ili wakubali kesi hiyo. Mtunzi ametumia tanakali hii “marshi marshi” (uk. 205). Anaashiria jinsi wafungwa walivyotolewa chumbani na askari.

Tanakali nyingine iliyotumiwa na mtunzi ni “kiza tii” (uk. 197). Inaelezea jinsi mhusika Hamza alivyokuwa ndani ya chumba kilichojaa giza. Aidha, ametumia tanakali hii “ukawapita “vuup”, (uk. 210-211). Inaashiria jinsi msafara ulivyoingia mjini kama umeme ukawafadhaisha watu wote.

Tumeonelea kwamba mwandishi ameitumia mbinu hii ya ubunifu kuipamba lugha kwa kuonyesha jinsi sauti inavyoigiza kitu kiangukavyo, kilivyo au kiliavyo. Tanakali kama mojawapo ya tamathali ya usemi imetumiwa na mwandishi. Jambo hili linadhihirisha ufaafu wa nadharia ya Kimtindo kupitia mhimili wa saba unaopendekeza matumizi ya tamathali za usemi kama tanakali.

4.5 Dhana ya Tashihisi

Mohammed (1995:127), anaelezea kuwa tashihisi ni mbinu ya uhusiano na ulinganisho wa vitu visivyo na uhai na vitu vyenye uhai hasa binadamu mwenyewe. Ni tamathali ambapo kitu hupewa sifa na hisia kama mtu.

4.5.1 Tashihisi katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi ameitumia mbinu ya uhuishaji katika masimulizi yake ili kuleta mvuto, kurutubisha fasihi na kuijenga picha halisi katika akili ya msomaji. Katika riwaya yake ya *Kuli* mhusika Majaliwa ametumia tashihisi "Nilipigwa na homa ya ghafla" (uk. 3). Katika muktadha huu mhusika anaelezea jinsi alivyokuwa mgonjwa. Pia, mtunzi ametumia tashihisi hii "ikamvunja" (uk. 8). Inaelezea jinsi mhusika Majaliwa alivyofanya kazi miaka mingi akapatwa na ugonjwa wa kiarusi uliomuua.

Mwandishi pia ametumia tashihisi "kilimlilia" (uk. 31). Katika muktadha huu mwandishi anahuisha king‟ora kwa kukipa uhai wa kuweza kulia kama binadamu. Aidha, mtunzi ametumia tashihisi "usingizi mwembamba" (uk. 32). Huo ni wakati mhusika Mzee Tindo alipouliza swali alipozinduka usingizini uliomchukua akisikiliza redio.

Mtunzi ametumia tashihisi hii "haikumsimamia" (uk. 53). Uhuishaji huu unaashiria kuwa Rashidi hakuwa na bahati ya kupata kazi nazo shida zikawalemea na mama yake. Pia, mtunzi ametumia tashihisi hii "aligombana." (uk. 70). Mbinu hii ya uhuishaji inatumiwa mhusika Rashidi alipovamiwa na mbu na kunguni wakimkera usingizini.

Mwandishi ametumia tashihisi hii “ikisubiri” (uk. 94). Huu ni wakati milima ya magunia ya karafuu yalikuwa bado kupakiwa ndani ya meli. Vilevile, ametumia tashihisi “nyimbo zimemchukua” (uk. 105). Mhusika Rashidi alimshtua Salum kwa kumshika bega kama kumvuta nyuma ili ampishe naye apate kuona vizuri. Mtunzi ametumia tashihisi hii “umejiinamia” (uk. 177). Mbinu hii imetumiwa kuonyesha kwamba mji wote ulikuwa kimya .

4.5.2 Tashihisi katika Riwaya ya Haini

Mwandishi ametumia tashihisi hii “daftari kubwa limelala” (uk. 9). Huu ni wakati wafungwa walipotolewa nje wakaamrishwa wajipange mstari mmoja. Askari aliyekuwa kwenye meza ya mapokezi akauliza angeandika kosa lao ni lipi.

Pia, mtunzi ametumia tashihisi hii “wafu wakafufuliwa” (uk. 17). Katika muktadha huu gereza lile lilikuwa ni dunia ya pekee ambayo siku ya mwisho imefika na parapanda imelia kwa hivyo wafu sharti wangefufuliwa.

Mtunzi ameendelea kutumia mbinu hii anaposema “lilichoka kuwa tupu” (uk. 15). Huu ni wakati msamaha ulitangazwa na Kigogo miezi michache tu kabla ya kuuawa. Mwandishi ametumia tashihisi nyingine “chupa zinatoka jasho” (uk. 79). Anaashiria jinsi soda zilizoletwa na askari wa kike zilivyokuwa baridi kama barafu. Aidha, anaendelea kutumia tashihisi “vyumba vitupu vinawazomea” (uk. 104). Mbinu hii inatumiwa na mwandishi kuelezea kuwa wafungwa mia sita na hamsini na tano waliojaza kumbakumba walihamishwa wakabaki kina Hamza.

Mtunzi ametumia tashihisi “Limemeza na kutema” (uk. 63). Huu ni uhuishaji unaelezea jinsi Gereza la Kinoamiguu lilivyoingia watu wengi na wengine wakitoka.

Mtunzi ametumia tashihisi hii “usingizi mfupi” (uk. 86). Huu ni wakati mhusika Hamza alipozinduliwa kutoka usingizi aliopata kwa taabu.

Tashihisi nyingine iliyotumiwa ni “udongo ulioshiba chokaa” (uk. 113). Mbinu hii imetumiwa na mtunzi kuonyesha kwamba kuta lile lilikuwa limejengwa imara likasimama madhubuti. Aidha, tashihisi iliyotumiwa na mtunzi ni “unamkimbia” (uk. 124). Anaelezea jinsi Sururu alivyokuwa na matumaini alipouona mwanga hafifu lakini akashindwa kuufikia kwani ulikuwa mbali na alipokuwa.

Mtunzi ametumia tashihisi hii “unawatazama” (uk. 150). Inaashiria ule mnara wa saa wa kanisa la Waingereza ulivyosimama mbele ya watu waliokuwa wamepanga mstari wapewe mikate. Mtunzi akimrejelea Kanali Bunju ametumia tashihisi “kinamzomea” (uk. 161). Anaelezea jinsi Kanali Bunju alivyokerwa kwa kutochukua kiti cha Kigogo baada ya kifo chake. Yeye alikuwa na usuhuba naye akadhani angemrithi lakini akapewa mtu mwingine.

Mwandishi ametumia tashihisi nyingine “imemezwa” (uk. 208). Walikuwa wamechimbiwa makaburi tisa ambayo wangezikwa baada ya kupigwa risasi. Nusura hawakuiona tena ukamezwa na wingu la nakama. Vilevile, mtunzi ametumia tashihisi “wanavyomsaili maiti” (uk. 239). Huu ni uhuishaji wa maiti ambaye kamwe hawezi kuhuishwa. Anaelezea jinsi Chopra alivyomsaili Mkadam kama wafanyavyo Munkar na Nakir wakimsaili maiti mwanandani.

Maoni yetu ni kwamba mwandishi ameitumia mbinu hii ya uhamishaji wa maana kusisitiza ujumbe aliokusudia msomaji kupata. Pia, kumfanya msomaji aelewe kwa undani zaidi maudhui na dhamira yake. Aidha, kama mbinu ya ulinganishi unaovutia

anapohuisha vitu visivyo na uhai na sifa ya binadamu. Tashihisi zimemsaidia kuweza kuziguza hisi za msomaji na kupamba lugha ipendeze zaidi. Ufaafu wa nadharia ya Kimtindo unadhihirika kwani mwandishi ameitumia tamathali hii ya usemi, kama mhimili wa saba unavyopendekeza ili kutia mvuto katika lugha.

4.6 Dhana ya Jazanda

King'ei, Muusya na Mwangi (2012), wanasema kuwa jazanda ni tamathali ilinganishayo vitu au hali mbili bila kutumia maneno ya kulinganisha. Jazanda huweza kudokeza kuhusu mandhari katika hadithi.

4.6.1 Jazanda katika Riwaya ya Kuli

Mwandishi Shafi Adam Shafi ametumia jazanda katika riwaya za *Kuli* na *Haini* ili kumchorea msomaji picha kamili ya anachomwelezea aweze kuelewa zaidi. Taswira hizi huleta uchimuzi kwa msomaji na kumpa ilhamu ya kuendelea kusoma hadithi. Amezitumia taswira kudhihirisha ubunifu wake katika uandishi wa riwaya ya *Kuli*. Taswira alizotumia zinamhamazisha msomaji anapoziona picha katika maelezo ya mwandishi. Kwa mfano, mwandishi anapoelezea jinsi Majaliwa alivyotoka kwake kwenda Hajitumbo kununua chakula cha siku ambayo hakwenda kazini, anasema:

> *Ilipofika saa nne, Majaliwa ilimbidi kutoka na hakusimama mpaka kwa Hajitumbo. Haikuwa masafa marefu kutoka Mferejimaringo mpaka hapo na baada ya kufika tu alinunua fungu la muhogo na papa mkavu na hiyo ilitosha kwa chakula cha siku ile" (uk. 3).*

Mwandishi anamchorea msomaji picha ya Majaliwa alipokuwa akienda Hajitumbo na alipofika akanunua muhogo na papa. Msomaji ataiona taswira ya mwendo wa

Majaliwa na alichonunua akilini mwake. Jambo hili litamfanya kutambua jinsi wafanyakazi wa bandirini walivyoishi maisha ya shida. Mwandishi ametumia taswira ya uoni anapomchorea msomaji picha ya chumba cha Bi Mashavu, anaposema:

> *Ijapokuwa chumba hicho kilikuwa kidogo, Bi Mashavu alikiweka katika hali ya usafi kabisa. Kitanda cha samadari kilichokuwemo humo kilitandikwa vizuri kwa shuka nyeupe iliyofumwa maua mekundu katikati. Mlikuwa na viti viwili vya „murscheya" vilivyokuwa na mito ya usumba ambayo ilivishwa foronya safi nyeupe. Kila magharibi Bi Mashavu alikuwa na kawaida ya kunyunyiza asumini juu ya kitanda na baadaye kufukiza udi ambao ulileta harufu nzuri ndani ya chumba hicho. Kila siku kanga safi zilining"inizwa juu ya besera ya kitanda na Majaliwa, baada ya kwisha kukoga tu, alivuta moja ya kanga hizo na kujjifunga kiunoni" (uk. 5).*

Mwandishi anamchorea msomaji picha ya chumba kizuri cha Bi Mashavu kwa hivyo, anakiona vizuri. Pia, anaviona viti, mito na foronya. Taswira ya harufu inazijia hisia za mnuso zinazomfanya msomaji kunusa harufu nzuri ya asumini aliyotumia Bi Mashavu kunyunyizia juu ya kitanda na harufu ya udi aliofukiza chumbani. Msomaji pia anamwona Majaliwa baada ya kujifunga kanga safi kiunoni baada ya kukoga. Taswira hizi zitavuta nadhari ya msomaji awe na hamu ya kuendelea kuisoma riwaya.

Mwandishi anapoelezea jinsi Bi Mashavu alivyokuwa akimtunza mumewe vizuri anasema:

> *Bi Mashavu naye alikuwa amekwisha koga, amejifunga kanga moja kifuani na moja amejitanda. Amejitia tarabizuna ananukia vizuri. Sinia ya chakula iliwekwa katikati ya chumba na hapo tena Majaliwa na Bi Mashavu walikaa juu ya mkeka na kuanza kula (uk. 5).*

Mwandishi amemchorea msomaji picha ya Bi Mashavu akaweza kuona alivyokuwa mrembo baada ya kukoga na kujifunga kanga kifuani na kujitanda nyingine. Kisha taswira ya harufu msomaji anapopatwa na hisia za mnuso na kunusa tarabizuna iliyomfanya Bi Mashavu kunukia vizuri. Taswira nyingine ya mwonjo inampata msomaji anayetamani kukionja chakula kilichowekwa juu ya mkeka kikiwa ndani ya sinia.

4.6.2 Jazanda katika Riwaya ya Haini

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anatuchorea taswira ya hisi ya uoga anapoelezea kuhusu mhusika Hamza alivyokuwa na hofu baada ya kusikia mlio wa risasi anaposema:

> *Hamza alisimama akachungulia dirishani. Ukumbi wa nyumba yake ulikuwa ghorofa ya kwanza ya kijumba kidogo cha ghorofa mbili. Nyumba yenyewe ilikuwa katikati ya majumba mengine yaliyosongamana na kuufanya mtaa mzima uwe na vichochoro vyembamba, sifa ya mji wa Unguja (uk. 2).*

Taswira ya jinsi alivyochungulia inaonyesha jinsi alivyokuwa na wasiwasi mwingi na alitaka kubainisha kilichokuwa kikitendeka huko mjini Unguja. Taswira hii inamhamasisha msomaji juu ya mauaji baada ya risasi kufyatuliwa naye kuwa na mvuto wa kutaka kujua kama kuna mtu yeyote aliyeuawa.

Isitoshe, mwandishi pia katika riwaya ya *Haini* ametumia taswira ya hisi, ya kuona chumba cha Hamza na Khadija, anapotumia maelezo yafuatayo:

> *Kilikuwa chumba kidogo tu ambacho kila kitu ndani yake kimepangwa kwa uangalifu ili kuitumia vizuri kila nafasi iliyopatikana (uk. 4).*

Maelezo haya yanatilia mkazo jinsi hali ilivyokuwa katika chumba chao. Ndipo mwandishi anapoelezea msomaji zaidi juu ya chumba hicho anapomchorea taswira anaposema kuwa:

> *Mlikuwemo na kitanda cha futi tatu na nusu kilichokuwepo chini ya dirisha, Viti viwili, kimoja katika kila pembe ya kitanda. Zulia dogo la usumba lilitandikwa mbele ya kitanda. Meza ndogo ya msaji ilikaa vizuri katika pembe ya chumba karibu na mlango. Juu yake palikuwa na nepi zilizokunjwa vizuri. Sabuni ya mtoto, podari ya mtoto na mafuta ya mtoto. Chini ya ile meza palikuwepo dishi la kumkogeshea mtoto, chini ya kitanda palikuwa na chungu kilichojaa jimbo. Na vyote hivyo vilikifukiza kile chumba kikawa kimejaa harufu ya uzazi na kukipa sura ya matumaini ya maisha mapya, kwa mtoto na wazazi wake. (uk. 4).*

Msomaji ataiona taswira ya chumba hicho vizuri kwani mwandishi amemwelezea vitu vyote vilivyo chumbani humo. Kwa hivyo, mpangilio wa vitu vilivyo Ndani utajitokeza na kuganda akilini mwa msomaji na kuelewa zaidi juu ya maisha ya Hamza.

Aidha, mwandishi ametumia taswira ya hisi kuwahamasisha wasomaji dhidi ya maonevu katika jamii hasa matumizi mabaya ya asasi ya polisi na mahakama. Anaelezea jinsi watuhumiwa walivyopigwa vibaya kisha kufungiwa katika vyumba vilivyokuwa na kiza kizito vilivyofungwa kwa makufuli na minyororo ili wasiweze kutoroka anaposema:

> *Alimtazama tena Barakati vile alivyochuchumaa na kichupi kichafu alichokivaa, pingu zimemkaza mikononi. Barakati alikuwa mfupi mnene, na vile alivyochuchumaa na misuli ilivyomjaa kifuani na mikononi, alionekana kama mwanariadha mnyanyuaji vyuma vizito. Uso ulimvimba macho yakaonekana madogo. Domo nalo lilimvimba likajaa tele juu ya uso wake mpana (uk. 9).*

Taswira hii inaashiria mateso aliyotendewa Barakati. Katika uhasilia wa maisha, ni dhuluma kumpiga mtu mpaka akavimba macho. Taswira hii inamwonyesha msomaji kuhusu mikakati inayotumiwa na watawala kuwadhulumu watawaliwa. Vilevile, mitafaruku kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa inaangaziwa. Maelezo ya mwandishi kuhusu hali ya Barakati inaibua taswira ya kiumbe ambaye hali yake ilikuwa mbaya mno. Jambo ambalo linamdhalilisha mhusika huyu, naye msomaji

atakasirika anapoiona taswira hiyo isiyo ya kawaida na kugundua kuwa mfumo wa kisiasa hautambui haki za kibinadamu. Taswira nyingine ya hisi aliyotumia mwandishi inaonyesha chumba alimofungiwa Hamza peke yake anapoelezea:

> *Hamza alitiwa chumba cha peke yake. Kilikuwa chumba kikubwa cha kiasi cha mita tano za mraba. Kitupu, hamna chochote ndani zaidi ya ndoo moja tupu, mbovu. Kilikuwa na dirisha moja tu nalo lilikuwa juu ambako huwezi kufika kwa kuchungulia. (uk. 11).*

Taswira hii inaashiria uoga mwingi aliokuwa nao Hamza alipofungiwa chumbani peke yake ili asiweze kuwasiliana na wenzake. Msomaji anaiona taswira hii kama njia ya kumtenga ili aweze kudhulumiwa zaidi kwani mahakama kama hizi hazikujengwa kumtetea mtawaliwa. Naye msomaji atafikiria zaidi juu ya mfumo wa kisiasa nchini. Mhimili wa nane katika ndharia ya Kimtindo unamhimiza mwandishi kutumia lugha ya kumtia msomaji mvuto na ari ya kusoma. Jambo linalojitokeza katika kazi za mwandishi hivyo basi, kudhihirisha ufaafu wa nadharia hii. Tumeonelea kuwa mbinu hii inayoleta picha ubongoni inamfanya msomaji aione taswira ya kinachoelezwa na mwandishi hivyo kumtia ari ya kuendeleaa kusoma.

4.7 Dhana ya Ishara

Utafiti wa Nyanchama (2004), ulihusu matumizi ya taswira na ishara katika “Sauti ya Dhiki” ulilenga kuchunguza na kubainsha sababu zilizochangia matumizi ya taswira. Ishara bia huweza kutambulika na watu wengine popote pale walipo. Kwa mfano, mto hutumiwa kama ishara ya kuonyesha mpito wa maisha, milima huashiria

matatizo, mvua huashiria neema, pete kuashiria ndoa na kadhalika. Ishara zisizo bia hueleweka katika muktadha wa kazi inayohusika. Ishara ya ndege anayeruka kwa shida ni ishara ya kuvunjika kwa ndoto na hatima ya kujiendeleza kibinafsi na kufikia furaha.

Ishara ni mbinu inayosimamia, kuwakilisha au kumaanisha kitu kingine. Jambo alilotaka kusema kwa kutumia maneno yanayokinzana. Matokeo ya uchimuzi wake hutokana na kuwa jazanda inaweza kuuficha ujumbe fulani na kumfanya msomaji ashangazwe na kile alichokusudia kusema mwandishi.

4.7.1 Ishara katika Riwaya ya Kuli

Katika riwaya ya *Kuli* mwandishi ametumia ishara ya paka anaposema:

> *Rashidi hakupenda kurejea nyumbani wakati ule na alistahabu kupitisha siku ile hivi hivi akizubaa majiani. Alikuwa na hakika kwamba akirudi huko nyumbani, atamkuta paka amelala jikoni (uk. 16).*

Katika aya hii mwandishi ametumia ishara ya paka kuelezea maisha ya Rashidi yalivyo. Anaposema Rashidi kuwa paka atalala jikoni inamaanisha kuwa hakikupikwa chakula kwani hakikupatikana. Mwandishi anamwelezea msomaji kuwa Rashidi hakuwa na uhakika katika maisha yake bali alimtegemea mama yake ambaye alikuwa hohehahe. Rashidi anamwona paka akiwa na starehe kumshinda kwani hajishughulishi kutafuta riziki na sharti atalishwa kumaanisha Rashidi alikuwa amekata tamaa na kukosa matumaini katika maisha yake.

4.7.2 Ishara katika Riwaya ya Haini

Katika riwaya ya *Haini* mwandishi anaitumia ishara ya picha anaposema:

> *Ukutani inaning''inia picha kubwa ya Hamza na Khadija Wamekumbatiana (uk. 1).*

Hiyo picha ukutani ni ishara inayoonyesha kile kitakachompata Hamza baadaye. Ni maelezo yasiyo dhahiri ya kitakachotokea kwake Hamza. Picha hiyo inayoonyesha uzuri na ujana wao wawili wanapokumbatiana. Picha hiyo inajitokeza kama mbinu ya uchimuzi inapoonyesha jinsi walivyopendana na hakuna kati yao angeweza kufikiria kuwa wangetengana kupitia kutiwa mbaroni kwa Hamza.

Maoni yetu ni kuwa mbinu hii inamfanya msomaji kutafakari kwa undani zaidi ili aweze kung`amua anachokusudia mwandishi. Matumizi haya yanawiana na mhimili wa nane wa nadharia ya Kimtindo unaomwelekeza mwandishi kutumia lugha itakayomvutia msomaji aweze kufikiria kuhusu analolisema.

4.8 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumechanganua mtindo wa mwandishi Shafi Adam Shafi kwa kuzingatia mbinu alizotumia za ukuishi na uchimuzi wa maana. Mbinu hizi zinadhihirisha umahiri wa mwandishi wa kumnata msomaji ili apatwe na taharuki wakati wa kuzisoma riwaya za *Kuli na Haini.* Katika sura ya tano tutatoa muhtasari wa utafiti, matokeo, changamoto, mchango na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Muhtasari na Matokeo ya Utafiti

5.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti mzima kuanzia sura ya kuanza hadi ya mwisho. Aidha, sura hii imetoa matokeo ya utafiti kupitia ugunduzi mbalimbali ambao umetokana na uchunguzi kuhusu kila lengo la utafiti kwa kuzingatia misingi ya nadharia za utafiti.

Vilevile, sura hii imetoa changamoto katika utafiti huu na mapendekezo ya masuala muhimu ambayo yanaweza kuwa kichocheo cha uchunguzi mwingine zaidi kuhusu fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umechanganua mielekeo na mtindo katika uandishi wa riwaya teule za Kiswahili, *Kuli na Haini*. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ya kubainisha jinsi mazingira na mielekeo ya mwandishi yanavyowiana na uandishi wa riwaya teule. Hatimaye, kubainisha namna mbinu za ukiushi na uchimuzi zinavyowiana na zile za riwaya teule.

Malengo haya yalichanganuliwa na kufafanuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa na nadharia ya kimtindo. Malengo haya ya utafiti yametekelezwa kupitia sura tano za tasnifu hii.

Sura ya kwanza imefafanua msingi wa utafiti huu. Sura hii iliangazia usuli wa utafiti ambao uliuwekea msingi utafiti huu kwa kuonyesha nafasi ya mazingira na mielekeo katika kuathiri uandishi wa riwaya teule. Aidha, ilibainisha mitindo ya uchimuzi na ukiushi na jinsi mtindo hii inaweza kuathiri riwaya hizi.

Isitoshe, sura hii imejadili suala la utafiti na sababu ambazo zilisababisha mada hii ya utafiti kuchaguliwa. Pia upeo na mipaka ya utafiti ilijadiliwa katika sura hii. Vilevile, yaliyoandikwa kuhusu mada hii yamejadiliwa katika sura hii ili kubainisha mchango na nafasi ya kazi za utafiti za awali ambazo zimetajwa katika utafiti huu.

Sura hii ya kwanza pia imejadili nadharia zilizotumika kuuongoza utafiti huu. Nadharia zenyewe ni; nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na nadharia ya Kimtindo. Utafiti katika sura hii uliangazia waasisi na waitafaki wa nadharia hizi na kubainisha wazi mihimili ambayo ilifaa utafiti huu. Hali kadhalika, mbinu ya utafiti ya usomaji maktabani ilijadiliwa. Pia, sampuli na namna ya kuteua sampuli ilijadiliwa katika sura hii.

Sura ya pili imechaganua mazingira na mielekeo ya mtunzi katika riwaya teule kwa lengo la kubainisha mazingira ya mwandishi yalivyoathiri mielekeo yake kwa jumla alipoziandika riwaya teule. Aidha, kubainisha jinsi mazingira na mielekeo ilivyomsaidia kubuni maudhui yake. Mazingira na mielekeo ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi yalichanganuliwa katika riwaya hizo ambazo zilidhirisha kuwepo kwa mazingira na mielekeo ya mwandishi alipoziandika.

Sura ya tatu imejadili athari za mitindo ya ukiushi na uchimuzi. Mwandishi ametumia mazungumzo kama mbinu ya ubunifu wa kukiuka mfuatano wa masimulizi, jambo

linalomtia ari msomaji. Pia, mwandishi anadhihirisha usanii kwa habari kutoelezwa kwa msomaji moja kwa moja kama ngano. Kwa hivyo, uchimuzi wa kimakusudi humpa msomaji nafasi ya kujua sehemu muhimu katika ujumbe.

Aidha, mtunzi ametumia mlazo kama mbinu ya ukiushi ili kuweza kujiondoa kutoka masimulizi, msomaji aweze kushiriki hisia za wahusika. Vilevile, amezitumia nyimbo ili kuelezea dhamira ya kimapenzi na hisia za mhusika ajengapo matumaini maishani. Wimbo pia unaweza kudhihirisha kejeli, mtu akiimba wakati wengine wana shida. Hapo uchimuzi hutokea kwa msomaji.

Mwandishi amedhihirisha ukiushi wa kimsamiati anapotumia maneno yaliyoandikwa kwa mlazo ili kubadilisha mtiririko. Vilevile, lafudhi ameitumia kumtambulisha mtu na jamii yake. Pia, mtunzi ametumia misemo na nahau ili kuficha maana na kuleta maana isiyo ya kawaida. Methali zimetumiwa na mwandishi ili kutoa maadili katika jamii, kufumba ujumbe, kuelimisha, kuburudisha na kuonya.

Mtunzi ametumia uradidi wa maneno ili kutoa msisitizo fulani utakaoleta uchimuzi. Katika ukiushi na uchimuzi wa kisintaksia mwandishi ametumia sentensi refu na fupi katika aya. Nao usambamba na uradidi umeutumia kupitisha ujumbe kwa jamii kupitia ukiushi na uchimuzi katika sentensi, vitenzi na maneno. Aidha, ameutumia kuonyesha uchimuzi wa mhusika anapokiri makosa yake mwenyewe.

Katika sura ya nne mwandishi alishughulikia athari za mitindo ya ukiushi na uchimuzi kupitia sitiari, tashbihi, tabaini, tanakali, tashihisi, jazanda na ishara.

Hatimaye, sura ya tano, utafiti uliangalia muhtasari wa kila sura ya utafiti huu na matokeo yake kwa kina. Katika kuelezea matokeo, kila lengo la utafiti lilichunguzwa na kukadiriwa iwapo lilitimizwa. Vilevile, sura hii ilijadili matatizo yaliyokumba utafiti huu, mchango na mapendekezo ya tafiti zaidi.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na uchaganuzi wa data iliyotokana na riwaya teule ambazo ni *Kuli na Haini*, imebainika kwamba mielekeo na mazingira ya mwandishi ina athari kubwa katika uandishi wa riwaya teule.

Mielekeo ya mwandishi kuhusu mazingira yake ina athari kubwa katika uandishi wa riwaya hizi. Pia, uteuzi wa mtindo wa uandishi wa mtunzi uliathiriwa na mielekeo na mazingira yake kwani alichota malighafi kutoka kwa jamii yake. Malengo ya utafiti huu yalikuwa; kuchanganua mazingira ya mwandishi yalivyoathiri utunzi wake, kuchanganua mielekeo ya mwandishi katika utunzi wake, hatimaye kuchambua mtindo wa mwandishi kupitia mbinu za uandishi za ukiushi na uchimuzi. Malengo mawili, la kwanza na la pili yalitimizwa wakati mazingira na mielekeo ya mwandishi ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi yalipodhihirika katika uchanganuzi. Nalo lengo la tatu la utafiti lilitimizwa kwa kuchunguza mbinu za uandishi za uchimuzi na ukiushi wa maneno katika sura ya tatu. Nayo sura ya nne ikabainisha matumizi ya mbinu za ukiushi na uchimuzi wa maana.

Utafiti huu ulibainisha kwamba mielekeo na mazingira ya mwandishi katika riwaya teule ni taathira ya maudhui katika riwaya zake. Mtunzi huyu amechukua mielekeo ya kijamii, kiuchumi, kihistoria na kimapinduzi kama msingi wa utunzi wake.

Uchaguzi wa mitindo ya ukiushi na uchimuzi ulimfaa mtunzi katika kuelezea maudhui na dhamira yake ya mambo muhimu yaliyojitokeza katika jamii husika. Ametumia ubunifu wake kuendeleza maudhui yake. Hali hii ilitokana na mhimili wa nne katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa unapopendekeza kuwa mtu atakuwa mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.

Katika riwaya ya *Kuli*, mwandishi ameangazia kazi ya ukuli iliyofanywa kule bandarini. Suala la majaliwa kufanya kazi ya ukuli hadi kufa kwake imejadiliwa. Pia, mwanawe Rashid alipokuwa yungali mtoto mchanga akaichagua kazi iliyofanywa na baba yake kwa kuwa hakuweza kwenda shule angalau apate elimu ambayo ingemwezesha kupata kazi yenye hadhi. Utafiti ulibainisha kuwa mtunzi alitumia masimulizi ya sira kwani ameyaelezea maisha ya Rashid tangu akiwa mtoto, malezi yake hadi akawa mtu mzima.

Alipopevuka kiurazini akaungana na wenzake kupigania nyongeza ya mshahara. Jambo lililomfanya kukabiliana na askari waliotaka kuuokomesha mgomo, wakamtia mbaroni akafungwa jela huku akimwacha mke wake Amina akiwa mjamzito bila wa kumsaidia.

Mtunzi anaelezea jinsi wafanyakazi bandarini walivyokufa wakiwa kazini na hawakufidiwa na waajiri kudhihirisha jinsi walivyowafanyia makuli ukatili. Walioumizwa wakiwa kazini walipelekwa nyumbani na wenzao bila kupewa pesa za kuhudumiwa hospitalini. Mwandishi anadhihirisha ukatili kule bandarini.

Aidha, katika riwaya ya *Haini* tunaona kwamba Hamza alipokuwa amestarehe na wenzake walisikia milio ya bunduki kila mmoja akatoroka kujitafutia usalama. Lakini

baadaye alitiwa baroni ikisemekana kwamba yeye alishirikiana na Hamduni ambaye alikuwa sahibu yake kumuua Kiongozi Kigogo. Jambo ambalo halikuwa la ukweli.

Baadaye, alipofungwa jela aliteseka sana akiwa na wenzake. Walipigwa vibaya sana wakateswa na kudhalilishwa utu wao. Naye mkewe Khadija na mwanawe Subira wakapatwa na shida nyingi ikamlazimu kukopa majirani pia, kupiga foleni siku ya ukoo ili apate chakula.

Wafungwa nao waliteswa kwa makosa ambayo hayakuwa yao. Kama vile, mhusika Haramia alipoachwa katika chumba chenye chatu akang'ang'ana naye hadi akamuua. Naye Hamza akatumbukizwa katika kisima huku amesokomekwa matambara mdomoni. Isitoshe, wahusika wote walichimbiwa makaburi na kila mmoja kusimama akingojea apigwe risasi kisha atumbukizwe kaburini. Sasa siyo kuchungulia kaburi tena, ni kuingia hasa ndani ya hilo kaburi.

Mwandishi vilevile, ameelezea jinsi Hamza alivyotiwa katika chumba cha kiza. Chumba hiki kilikuwa baina ya chumba cha kunyongea na jiko. Joto lilitokana na kuni zilizoteketea jikoni. Mchanganyiko wa joto la moto wa jikoni na joto la jua linalopiga juu ya ule mlango wa chuma mchana kutwa ndio unaotengeneza hali ya hewa ya chumba cha kiza. Joto kali hufukuta chumbani humo kutwa, kucha na inapofika usiku, mbu huminimika humo utadhani wamemiminwa makusudi. Mhusika Hamza akiegemea, kuta zinaunguza. Akikaa, sakafu inaunguza. Vile alivyosimama, nyayo nazo zinaungua. Afanye nini? Yumo katika nakama. Jahanamu ya hapa duniani. Mwisho alikaa, mwili wake ukalizoea joto taratibu. Mwandishi anadhihirisha mateso waliopitia wafungwa gerezani.

Mtunzi anaelezea jinsi Mazuruku alivyotwangwa, akafundafundwa, wakamning'iniza kwenye kitazi mavi mabichi yakamtoka. Huu ni ukatili wa hali ya juu gerezani.

Utafiti ulibaini kwamba mtindo wa ukuishi na uchimuzi katika riwaya teule umetumiwa ili kupamba lugha itakayomvutia msomaji na kufurahia kusoma riwaya teule.

5.4 Changamoto ya Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadha. Kulikuwa na changamoto ya kutofautisha kati ya matumizi ya mbinu za ukiushi na uchimuzi. Hata hivyo, tafiti za awali zilitusaidia kupata mwelekeo ili kubainisha sifa za kimtindo katika utafiti wetu.

5.5 Mchango

Kutokana na utafiti huu imebainika kwamba fasihi hususan riwaya inaweza kutumiwa kuyaangazia masuala ibuka katika jamii ya kisasa. Mtunzi wa riwaya teule amejikita katika uhalisia. Anaibua masuala ya wakati wetu yanayohusu hali halisi ya maisha ulimwenguni kote. Masuala haya ni kama vile ufisadi, ubaguzi, ndoa, ukiukaji wa haki za kibinadamu hasa watoto, uongozi wa kiimla, magonjwa kama Saratani na Ukimwi. Utafiti huu unaelimisha jamii kuhusu vyanzo na athari za masuala hayo. Kwa hivyo, wanapokumbana nayo wanaweza kuyakabili kupitia kwa utafiti huu wanajamii wataadilika na kuupinga uovu katika jami. Walimu watanufaika katika ufundishaji wa masuala ibuka kama inavyopendekezwa katika silabasi mpya.

5.6 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza mielekeo na mtindo katika riwaya mbili za Shafi. Hata hivyo, kuna mambo mengine ambayo utafiti haujashughulikia na yanaweza

kushughulikiwa na watafiti wengine. Mtafiti anaweza kulinganisha na kulinganua wahusika katika za *Kuli* na *Haini***.** Pia, tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusu taharuki katika riwaya hizi za *Kuli* na *Haini*.

5.7 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari, matokeo, changamoto, mchango na mapendekezo umefanywa. Mapendekezo yametolewa kwa nia ya kufanya na kuendeleza tafiti nyingine zaidi.

MAREJELEO

Ahmed, E. B. H. (2015). *Kamusi Teule ya Kiswahili, Kilele cha Lugha*. (uk. 804).

Aries, P. (1962). *Centuries of Childhood; A Social History of Family Life*. Tran. Robert Baldic: Newyork vintage.

Althusser, L. (1968). *Reading Capital*. Paris: Librairie Francois Maspero.

Bakhtin, M. M. (1981). "*Discourse in the Novel*," in M. M. Bakhtin, The Dialogic Imagination: four essays by M. M. Bakhtin, Austin, TX: University of Texas Press.

Baxandall, L. (1972). *Radical Perspectives in the Arts*. Middlesex: Penguin Books.

Berman, M. (2011). *The Communist Manifesto*. London: Penguin Books.

Bisztray, G. (1978). *Marxist Models of Literary Realism*. Newyork: Colombia University press.

Buffon, G. (1930). *Buffon"s Discourse on Style*. Paris: Librairie Hatier Publishers.

Clysenaar, A. (1976). *Introduction to Literary Stylistics*. London: B. T. Batsford Limited.

Chinua, A. (1983). *The Trouble with Nigeria*. Heineman: Amazon.

Daiches, D. (1981). *Critical Approaches to Literature*. Chicago: University of Chicago Press.

Doris, Ken na Norah. (2016). *Kielelezi cha Marudio ya Kiswahili*: Nairobi; Mentor Publishing Co.Ltd.

Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism*, London: Methuen.

Fowler, R. (1975). *Style and structure in Literature*: Essays in the new stylistics. Oxford, Blackwell.

Gitonga, O. (2011). *"Taathira ya Dhuluma kwa Mtindo katika Hadithi Fupi Teule za Kiswahili."* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Habwe, J na P. Karanja, (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publisher Ltd.

Haynes, J. (1995). *Style*. London and New York: Routledge.

Hunt, P. (1994). *An Introduction To Childrens Literature*. Oxford University Press.

Hussein, E. (1971). "Ufundi wa Abdulla" Katika Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili. Nairobi: OUP.

Jabir, H. M. (1977). "*The plantation Economy During the Protectorate period in Zanzibar (1890-1964)."* Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu cha Dar-es-salam.

James, C. V. (1973). *Soviet Socialist Realism*: Origins and Theory. London: Macmillan Press.

Jameson, F. (1981). *The Political Unconscious*: Narrative as a Socially Symbolic Act. London: Methuen.

Kairu, W. M. (2005). "*Uhalisia na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto."* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar-es-Salaam. Oxford University Press.

Kamau, M. (1992). *"Ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdalla"*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Kamunde, M. E. (1983). *"Kilio cha Wanyonge Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed"*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Karuga, M. N. (2005). "*Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto Katika Shule za Msingi Nchini Kenya*." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Kazungu, K. (1982). *"Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Literary Texts.*" Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi

Khaemba, S. S. (1999). "*Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi katika Dunia mti Mkavu na Kiza katika Nuru"***.** Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kimani, N. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar.* Nairobi: Nairobi University Press.

King'ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi, Acacia Stantex.

Leech, G. H. na Short, M. H. (1981). *Style in Fiction. A Linguistic Introduction to English Fiction Prose.* England: Longman Group Limited.

_____ (1969). *A linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.

Lodge, D. (1972). *20th Century Literary Criticism*. London: Longman.

Lukacs, G. (1971). *Studies in European Realism*: A Sological Survey of writings of Balzac, Stredhal, Zola, Tolistoy, Gorki and others.London: Merlin Press.

Maitaria, J. M. (2012). "*Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili*. Dhima ya Methali." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Masinde, E. W. (1992). "*Mashairi. Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo*." M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Materu, M. I . (1987). "*Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*." Mulika Na. 19. TUKI. Dar es Salaam.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Kwa Sekondari, Vyuo Vya Kati na Vyuo Vikuu. Mwanza: Serengeti Educational Publisher.

Mazrui, A. (1984). *Kilio Cha Haki*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, S. M. (1972). *Kiu*. Nairobi: East African Publishing House.

Musembi, N. N. (2008). *"Matumizi ya Taswira na Ukinzano Kama Kichocheo cha Zinduko katika Riwaya za G. K. Mkangi Mafuta (1984) na Walenisi (1995)."* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwangi, J (2005). "*Ufundishaji wa Shairi Katika Shule za Upili*." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwania, J. (2006). *"Usambamba katika Ushairi huru."* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu, K. na Chimera, R (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*, *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njuguna, H. (2015). *"Ukiushi katika Ushairi wa Amri Abedi na Kithaka wa Mberia."* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Nyanchama, M. (2004). *"Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhiki",* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Okello, J. (1967). *The Zanzibar Revolution*. Nairobi: East African Publishing House.

Osore, K. M.(1994). *"Uhakiki wa Kiisimu wa Riwaya za Suleiman Mohamed"*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Popkin, H. R. and Stroll, A. (1993). *Philosophy Made Simple*. Newyork: Three Rivers Press.

Radbill, S. Y. (1968). *A History of Child Abuse and Infanticide*. In R. E. Helfer & C. H. Kempe (Eds.) The Battred child, Chicago. University of Chicago.

Scocpol, T. (1979). *State and Social Revolution*. Cambridge: Cambridge University Press

Shafi, A. S. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Kolemuwa.

_____ (1979). Kuli. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

_____ (1998). *Vuta n" kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

_____ (2003). *Haini*. Dar es Salaam: Longhorn.

Taiwo. O. (1984). *Female Novelist of Modern Africa*. London : Maxmillan.

Thiong'o, N. (1981). *Writers in Politics*. Nairobi: Heneman.

_____ (1986). *Decolonising the Mind*. The politics of the language in African literature. London : James Curry Limited.

Turner, G. W. (1984). *Stylistics*. Harmondsworth: Penguin.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: JKF.

Wamitila K. W. (2003). *ISTILAHI na NADHARIA*. Nairobi; Focus Publication Limited.

Wamitila K. W. (2008). *Kazi ya Fasihi Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Viole Muwa, Daisy Printers.

Wanyama, A. (2007). *"Maudhui na Mtindo katika Utendi wa Khuswala Kumuse."* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Weche, M. O. (2000). *"Children`s Literature as an Image Force."* A case study of Ezekiel Alembi's books," M. A . Thesis, Kenyatta University.

Wekesa, A. (2008). *"Matumizi ya Taswira Katika Ushairi Huru wa Kiswahili".* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

William, E. (1958). *Marxist and Literature*. Oxford: Oxford University Press.